OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI
S.L.P 258, Maisara - Zanzibar, Simu: +255 24 2234009, Nukushi: +255 24 2234009
Baruapepe: info@ocagz.go.tz, Tovuti: www.ocagz.go.tz

DIRA

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi

DHAMIRA

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa

Katika kuhakikisha uwazi na uwajibikaji unapatikana katika matumizi mazuri ya rasilimali za umma Afisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:-

Uaminifu

Kuhakikisha Ofisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia sheria.

Uadilifu

Kuwa ni Ofisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

Kuwa Huru

Kuwa ni Ofisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa sheria

Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi

Kuwa ni Ofisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

Kutunza Siri

Kuwa ni Ofisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

Uwazi na Uwajibikaji

Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma.

YALIYOMO

SURA YA KWANZA.....1

1.0 UTANGULIZI.....1

1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.....1

1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI.....2

1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI.....3

1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA.....4

1.5 UTENDAJI WA MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.....5

1.6 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI.....6

1.7 SHUKURANI.....6

SURA YA PILI.....8

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI KWA MWAKA 2019/2020.....8

2.1 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA 2019/2020 KWA AJILI YA UKAGUZI.....8

2.2 HATI ZA UKAGUZI.....9

2.3 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020.....10

SURA YA TATU.....13

3.0 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR.....13

3.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO).....13

3.2 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) 21

3.3 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB).....28

3.4 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC).....33

3.5 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR 46

3.6 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) 60

3.7 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR.....86

3.8 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF).....89

3.9 MFUKO WA BARABARA 93

3.10 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) 99

3.11 SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC).....100

3.12 KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO).....105

3.13 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR.....106

3.14 SHIRIKA LA MAGAZETI.....108

3.15 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA).....110

3.16 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA).....122

3.17 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA).....124

3.18 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA).....136

3.19 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)...141

3.20 MAMLAKA YA UDHIBITI, UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI ASILI ZANZIBAR (ZPRA).....143

3.21 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA).....147

3.22 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA).....149

3.23 MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE ZANZIBAR....162

3.24 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR....165

3.25 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA).....166

3.26 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA.....166

3.27 CHUO CHA UANDISHI WA HABARI.....169

3.28 TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA.....170

3.29 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA.....171

VIAMBATISHO.....173

RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI 2020

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kukagua fedha zote zinazotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya ukaguzi wa hesabu angalau mara moja kwa mwaka. Ukaguzi wa hesabu unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ana wajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 Kifungu cha 112 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma kifungu namba 123(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016 , Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na sheria nyenginezo.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

"a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. "

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za umma.

1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ambazo zimeelezwa kwenye taarifa za ukaguzi zilizotumwa kwa Taasisi husika.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya taasisi kuu za ukaguzi (ISSAIs) ili kutoa uhakika iwapo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi zilizokaguliwa zinaonyesha sura halisi. Taratibu za ukaguzi zinajumuisha uchambuzi na kumbukumbu za taarifa mbali mbali, mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya taarifa za kisheria zinazosimamia uendeshaji wa taasisi zilizokaguliwa.

Taarifa hizo zinaonesha kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi uliofanyika kwa misingi ya sampuli, kwa hivyo matokeo ya ukaguzi kwa kiasi kikubwa yalitegemea kumbukumbu za taarifa na nyaraka tulizoziomba na kuwasilishwa kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbali mbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Miongoni mwa taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

I. Taarifa ya Mizania ya Hesabu
II. Taarifa ya Mapato na Matumizi
III. Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji
IV. Taarifa ya mtiririko wa fedha
V. Taarifa ya uwiano na bajeti na kiasi halisi cha matumizi
VI. Sera za uhasibu na maelezo ya taarifa za fedha

Mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa kumepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa Sheria mbalimbali zikiwemo sheria za fedha, Sheria ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, pamoja na Sheria nyenginezo na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Katika kufanya ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali tulizingatia taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

i. Kutoa barua za kuanza ukaguzi kwa taasisi inayokaguliwa kabla ya kuanza kazi za ukaguzi inayoeleza madhumuni na upeo wa ukaguzi, maeneo yanayotarajiwa kufanya ukaguzi na kuelezea majukumu ya ukaguzi kwa mkaguzi (Engagement Letter).
ii. Kuandaa mkakati na ujumla wa ukaguzi unaonesha muelekeo mzima wa ukaguzi, vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinazokaguliwa.
iii. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) ambapo katika kikao hicho uongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa kabla ya kuanza kazi za ukaguzi.
iv. Kujadiliana na uongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali kuhusu utekelezaji na utendaji kwa kipindi cha mwaka husika.
v. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kupata uelewa wa shughuli za Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali.
vi. Kutumia njia na mbinu nyingine za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Regularity Audit Manual).
vii. Kutoa ripoti ya ukaguzi na mapendekezo kwa uongozi ambayo yatakuwa yanaonyesha kilichobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa maelezo kuhusu ripoti hiyo.

viii. Kutoa rasimu ya ripoti ya ukaguzi kwa uongozi inayoeleza hoja za ukaguzi zilizobainishwa na kutoa muda kwa uongozi kuweza kujibu hoja hizo.

ix. Kufanya kikao cha mwisho (Exit Meeting) na mkaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.

x. Kutoa ripoti ya mwisho kwa uongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali inayoonesha matokeo ya ukaguzi ikiwemo hoja za ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi na mkaguliwa kuweza kujibu hoja hizo.

xi. Kutoa ripoti ya ukaguzi kwa uongozi inayoonesha hati ya ukaguzi aliyopata mkaguliwa kuhusiana na taarifa za fedha.

Aidha mbinu za kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali zilizokaguliwa zilitumika katika ukaguzi ambapo mbinu hizi za ukaguzi zinasisitiza haja ya kuelewa kwa kina mazingira ya taasisi inayokaguliwa ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani, kutathmini vihatarishi na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani.

Mbinu za ukaguzi zinatekelezwa kwa kutumia muongozo na utaratibu wa ukaguzi, ili kuhakikisha kwamba mbinu za ukaguzi zinaenda na wakati ambapo Ofisi inafanya mapitio ya muongozo wa utaratibu na ukaguzi kila mwaka kwa kuimarisha ukaguzi na kuhakikisha kwamba mabadiliko yoyote muhimu yanajitokeza katika fani ya ukaguzi na uhasibu pamoja na mabadiliko ya mifumo ya sheria yanazingatiwa ipasavyo.

Aidha utendaji wa Mashirika ya Umma na taasisi za Serikali zilizokaguliwa umeangaliwa na kuonesha viwango vya kiutendaji kifedha na kiuendeshaji. Utendaji wa kifedha umepimwa kwa kuangalia faida au hasara iliyopatikana kwa kipindi cha mwaka husika. Utendaji wa kiuendeshaji umepimwa kwa kuangalia ni kwa kiasi gani taasisi imeweza kufikia malengo yake ya msingi.

1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za Umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka na kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na kufanikiwa kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbali mbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

1.5 UTENDAJI WA MASHIRIKA NA TAASISI ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kumebainika dosari mbalimbali za kiutendaji kwa baadhi ya mashirika na taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika usimamizi wa ukusanyaji mapato pamoja na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma ukilinganisha na mwaka wa fedha 2018/2019.

Uwasilishaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka umeimarika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali hesabu hizo zimewasilishwa kwa wakati na kupelekea kuanza kwa kazi za ukaguzi kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za ukaguzi tulizojipangia.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka umekuwa na dosari kwa baadhi ya mashirika na Taasisi za Serikali kutokana na dosari zilizobainika katika mfumo wa udhibiti wa ndani katika usimamizi wa fedha.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 kumekuwa na dosari kubwa katika uendeshaji na utendaji kwa Mashirika ya Umma na Taasisi za Serikali ambapo hati mbali mbali za ukaguzi zimetolewa kwa Mashirika ya Umma na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni,2020 zimepata aina tofauti ya hati za ukaguzi, zilizotolewa kulingana na hali halisi ya taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua jitihada mbali mbali katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimepelekea kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa uwajibikaji katika utendaji wa shughuli za Serikali na kupelekea kuimarika kwa taasisi za Serikali.

Katika kuimarisha Utawala Bora kwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza maoni na ushauri unaotolewa na kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi ikiwemo Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma (LAAC), Kamati ya Kudhibiti na Kuchunguza Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Bajeti.

Kutokana na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika utendaji na nidhamu katika matumizi ya rasilimali za Umma kumepelekea kuongezeka kwa kasi ya maendeleo nchini na kuimarika kwa hali ya uchumi na kuleta tija kwa wananchi wa Zanzibar.

1.6 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI

Kamati za Baraza la Wawakilishi ni muhimu sana katika kuimarisha uwajibikaji na kuleta ufanisi katika kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia. Kamati hizi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya Utawala Bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma.

Kutokana na umuhimu mkubwa wa Kamati za Baraza la Wawakilishi, Ofisi imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoanishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Aidha Kamati hizo zimekuwa zikitoa mchango mkubwa katika kusimamia uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma kwa kutoa ushauri na mapendekezo mbali mbali kwa Serikali kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji kwa matumizi ya rasilimali hizo kwa maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Tunatoa shukurani za dhati kwa wenyeviti na wajumbe wa kamati zote za Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zao wanazochukuwa katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Shukurani za pekee zimuendee Mwenyekiti pamoja na wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti na kuchunguza Hesabu za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma (LAAC) kwa kutoa maelekezo,ushauri,maoni na michango kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi pamoja na Serikali kwa ujumla.

1.7 SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani kwa wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi ya mwaka 2019/2020.

Nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein A. Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katikamatumizi ya rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.

Natoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada mbali mbali zinazochukuliwa katika kuimarisha Ofisi hii kiutendaji na watendaji kwa

ujumla. Vile vile napenda kuwapongeza na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa juhudi zao walizochukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Aidha, ninawashukuru viongozi na watendaji wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na watendaji wa taasisi mbalimbali za Serikali kwa mashirikiano mazuri waliyotupatia hadi kukamilika kwa kazi za ukaguzi.

Ni imani yangu kwamba ushirikiano utaendelea kutolewa kwa madhumuni ya kufanikisha malengo na kukuza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma ili kuimarisha Utawala Bora kwa taasisi za Serikali.



.....

Dkt. OTHMAN ABBAS ALI

KAIMU MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

SURA YA PILI

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI KWA MWAKA 2019/2020

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka 2019/2020 imebainika kwamba uwekaji wa kumbukumbu na taarifa mbali mbali za hesabu ikiwemo fedha na rasilimali za umma pamoja na udhibiti wa ndani umeimarika.

2.1 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA 2019/2020 KWA AJILI YA UKAGUZI

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha sheria ya usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na matumizi ya Taasisi husika. Aidha kifungu Namba 119(2) cha sheria hiyo, kinawataka wasimamizi wa fedha katika Taasisi za Serikali kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu zao za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kukamilika kipindi cha mwaka wa fedha.

Tunatoa pongezi kwa Mashirika na Taasisi mbali mbali za Serikali kwa jitihada walizochukuwa za kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa sheria.

Uwasilishwaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa ajili ya ukaguzi kutoka kwa Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama ifuatavyo: -

Jadweli Nambari 1: Uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka 2019/2020

Namba	Fungu	Shirika/Taasisi	Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi	
			2018/2019	2019/2020
Mashirika ya Serikali				
1.	Linajitegemea	Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)	27/09/2019	30/09/2020
2.	Inajitegemea	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)	15/05/2019	06/01/2020
3.	Inajitegemea	Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)	30/09/2020	30/09/2020
4.	Inajitegemea	Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)	15/06/2020	-
5.	Linajitegemea	Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)	30/09/2019	29/09/2020
6.	Linajitegemea	Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC)	30/09/2019	30/09/2020
7.	Ruzuku	Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar	30/09/2019	30/09/2020
8.	Unajitegemea	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)	30/09/2020	30/09/2020
9.	Ruzuku	Mfuko wa Barabara Zanzibar	29/09/2019	29/09/2020
10.	Ruzuku	Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)	30/09/2019	30/09/2020
11.	Linajitegemea	Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)	27/09/2019	28/09/2020
12.	Inajitegemea	Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO)	28/09/2019	30/09/2020
13.	Ruzuku	Shirika la Huduma za Maktaba	27/09/2019	30/09/2020
14.	Ruzuku	Shirika la Magazeti	30/09/2019	30/09/2020

Mamlaka za Serikali				
15.	Ruzuku	Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)	27/09/2019	30/09/2020
16.	Inajitegemea	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)	30/09/2019	30/09/2020
17.	Inajitegemea	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA)	28/09/2019	17/09/2020
18.	Ruzuku	Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)	28/09/2019	28/09/2020
19.	Ruzuku	Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)	30/09/2019	29/09/2020
20.	Ruzuku	Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPRA)	20/09/2019	22/09/2020
21.	Inajitegemea	Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA)	30/09/2019	30/09/2020
22.	Ruzuku	Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo ya Amali	27/09/2019	30/09/2020
23.	Ruzuku	Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe	20/09/2019	26/08/2020
Taasisi za Serikali				
24.	Ruzuku	Mamlaka Ya Kuzuia Rushwa Na Uhujumu Wa Uchumi Zanzibar	25/09/2019	17/09/2020
25.	Ruzuku	Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar	30/09/2019	30/09/2020
26.	Ruzuku	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	30/09/2019	30/09/2020
27.	Ruzuku	Chuo cha Uandishi wa Habari (ZJMMC)	27/09/2019	27/09/2020
28.	Ruzuku	Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST)	23/09/2019	30/09/2020
29.	Ruzuku	Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Mawada ya Kulevya.	26/09/2019	30/09/2020

2.2 HATI ZA UKAGUZI

2.2.1 UTANGULIZI

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Namba 200 (ISA 200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumwezesha Mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi inayoeleza iwapo hesabu zinaonyesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na kama zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika. Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumuongezea imani mtumiaji wa hesabu husika kwamba zimetengenezwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hivyo, kumfanya Mkaguzi kupata sababu za uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina makosa na pia kutoa taarifa ya matokeo ya ukaguzi.

2.2.2 AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

2.2.2.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu au viwango vingine vya utoaji wa taarifa za fedha vinavyokubalika.

Kama mkaguzi ataona umuhimu wa kuvuta umakini wa wasomaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, na ambalo limeonekana kuwa ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo kwa ajili ya kufanya maamuzi yenye tija atatoa **Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo**.

Aya hii itawekwa tu pale ambapo mkaguzi amepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa kwa kiasi kikubwa na inatakiwa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za hesabu pekee.

2.2.2.2 Hati zisizoridhisha

Hati hizi hutolewa pale ambapo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zimeshindwa kuthibitishwa kutokana na athari zilizobainika na hivyo kupelekea taarifa hizo kutoonesha sura sahihi na halisi. Baadhi ya hati zilizotolewa katika kundi hili ni kama inavyoonekana hapo chini.

(i) Hati yenye shaka

Aina hii ya hati hutolewa pale (a) mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuhitimisha ukaguzi na kuona athari lakini si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha; au (b) mkaguzi anapokuwa ameshindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumuwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho kwa ujumla wake si za kimsingi katika usahihi wa taarifa za fedha.

(ii) Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha inatolewa pale Mkaguzi anapoona kuwa, taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa, na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

(iii) Hati mbaya

Hati hii hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hali hiyo inaathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa za fedha hizo.

2.3 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya hati za ukaguzi ishirini na tisa (29) zimetolewa kwa Mashirika na Mamlaka za Serikali kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi. Kati ya hati ishirini na tisa zilizotolewa taasisi ishirini na moja (21) zimepata Hati zinazoridhisha , taasisi tatu (3) zimepata Hati zisizoridhisha, taasisi nne (4) zimepata Hati zenye shaka na taasisi moja (1) imepata Hati mbaya kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020.

Mchanganuo wa Hati za ukaguzi zilizotolewa ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 2: Hati zilizotolewa kwa mwaka 2019/2020

Namba	Fungu	Shirika/Taasisi	Hati zilizotolewa	
			Aina ya Hati iliyotolewa 2018/2019	Aina ya Hati iliyotolewa 2019/2020
Mashirika ya Serikali				
1.	Linajitegemea	Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
2.	Inajitegemea	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
3.	Inajitegemea	Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)	Hati Isiyoridhisha	Hati Isiyoridhisha
4.	Inajitegemea	Shirika la Bima Zanzibar (ZIC)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
5.	Linajitegemea	Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC)	Hati Inayoridhisha	Hati Isiyoridhisha
6.	Linajitegemea	Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC)	Hati Inayoridhisha	Hati yenye shaka
7.	Ruzuku	Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
8.	Unajitegemea	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
9.	Ruzuku	Mfuko wa Barabara Zanzibar	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
10.	Ruzuku	Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
11.	Linajitegemea	Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC)	Hati Inayoridhisha	Hati yenye shaka
12.	Inajitegemea	Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
13.	Ruzuku	Shirika la Huduma za Maktaba	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
14.	Ruzuku	Shirika la Magazeti	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
Mamlaka za Serikali				
15.	Ruzuku	Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)	Hati Inayoridhisha	Hati yenye shaka
16.	Inajitegemea	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
17.	Inajitegemea	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA)	Hati Inayoridhisha	Hati Isiyoridhisha
18.	Ruzuku	Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
19.	Ruzuku	Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha

20.	Ruzuku	Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPRA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
21.	Inajitegemea	Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
22.	Ruzuku	Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo ya Amali	Hati Inayoridhisha	Hati yenye shaka
23.	Ruzuku	Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
24.	Ruzuku	Mamlaka Ya Kuzuia Rushwa Na Uhujumu Wa Uchumi Zanzibar	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
Taasisi za Serikali				
25.	Ruzuku	Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA)	Hati Mbaya	Hati Mbaya
26.	Ruzuku	Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
27.	Ruzuku	Chuo cha Uandishi wa Habari (ZJMMC)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
28.	Ruzuku	Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST)	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha
29.	Ruzuku	Tume ya Kitaifa ya Kuratibu Udhibiti wa Mawada ya Kulevya.	Hati Inayoridhisha	Hati Inayoridhisha

SURA YA TATU

3.0 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Ukaguzi uliofanyika katika Mashirika na Taasisi mbali mbali zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebainika kujitokeza kwa dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi hizo ambapo hoja mbali mbali za ukaguzi ziliainishwa katika ripoti za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika na Taasisi hizo na baadhi ya hoja hizo zilipatiwa maelezo na vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi.

Aidha ukaguzi wa hesabu za mwisho wa mwaka 2019/2020 umebaini kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa katika uwekaji wa kumbukumbu za hesabu pamoja na udhibiti wa rasilimali za umma, hata hivyo kumejitokeza dosari za kiutendaji kwa baadhi ya mashirika na taasisi zinazojitegemea katika uandaaji na ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

Matokeo ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali pamoja na maoni ya ukaguzi wa hesabu hizo ni kama ifuatavyo:-

3.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umefanya uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Umeme Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka hadi kufikia 120,870,387,033 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 114,591,339,203 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 6,279,047,830 sawa na asilimia 5.5 ya ongezeko.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 101,007,122,054 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 95,776,615,528 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 5,230,506,526 sawa na asilimia 5.5.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

(a) Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika (Operating Performance)

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa shirika kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kwanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini kutokana na uchambuzi wa taarifa ya faida/hasara (Statement of Profit and Loss Account).

Jadweli Nambari 3: Taarifa ya faida na hasara kwa mwaka 2019/2020

	2019/2020 TZS	2018/2019 TZS
Income:		
Energy Sales	102,849,319,228	96,600,518,340
Less: Cost of Sales	(87,290,554,204)	(83,630,587,072)
Gross Profit/(Loss)	15,558,765,024	12,969,931,268
Other Income	18,021,067,805	17,990,820,863
Total Operating Income	**33,579,832,829**	**30,960,752,131**
Operating Expenses:		
Personnel Expenses	6,560,314,335	6,012,987,854
Utility and Services	1,918,878,444	2,800,582,832
Repair and Maintenance	178,057,192	78,402,650
Office Expenses	970,914,050	1,974,966,301
Materials Cost	1,601,879,104	267,352,574
Advertising	54,286,308	51,891,775
Financial cost	7,360,596	22,294,572
Loss on Disposal	584,355,200	18,163,333
Customer Services	772,511,756	632,998,898
Depreciation	164,302,638	286,387,667
Bad Debts	903,708,227	0
Total Operating Expenses	**13,716,567,850**	**12,146,028,456**
Operating Profit/(Loss)	19,863,264,979	18,814,723,675
Less: Provision for Taxation	(2,912,287,122)	2,632,365,891
PROFIT/(LOSS) FOR THE YEAR	**16,950,977,857**	**16,182,357,784**

Uchambuzi wa jadweli linaloonekana hapo juu linaonesha ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Umeme Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka kutoka shilingi 30,960,752,131 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 33,579,832,829 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,619,080,698 ikiwa sawa na asilimia 8.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 13,716,567,850 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 12,146,028,456 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 1,570,539,394 sawa na asilimia 12.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Shirika la Umeme limepata faida ya shilingi 19,863,264,979 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni shilingi 18,814,723,675 kukiwa na ongezeko la shilingi 1,048,511,304 sawa na asilimia 5.27 , faida iliyoonekana hapo ilipatikana kabla ya kulipa ushuru.

Shirika la Umeme limefanya malipo ya kodi kwa mujibu wa sheria ya kodi yenye thamani ya shilingi 2,912,287,122 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo Shirika limefanya malipo ya shilingi 2,632,365,891 malipo hayo yanalipwa kulingana na faida inayopatikana.

Kwa upande wa faida baada ya tozo ya kodi iliyoripotiwa katika jadweli hapo juu imeonekana kuongezeka na kufikia shilingi 16,950,977,857 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na faida ya shilingi 16,182,357,784 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambapo imefanya ongezeko la shilingi 768,620,073 sawa na asilimia 4.

(b) Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Shirika la Umeme kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 4: Taarifa ya utendaji wa kifedha

	2019/2020 TZS	2018/2019 TZS
Total Current Assets	69,684,788,818	56,678,567,109
Total Current Liabilities	30,764,511,144	32,700,145,804
Working Capital (CA – CL)	38,920,277,674	23,978,421,305
Net Worth (Total Asset – Total Liabilities)	313,736,374,568	299,737,486,965
Ratio: Current Ratio (CA/CL)	2.27:1	1.73:1
NORMAL CURRENT RATIO	**2:01**	**2:01**

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika utendaji wa kifedha wa Shirika la Umeme umeimarika na kufikia uwiano wa mtaji wa 2:1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na uwiano wa mtaji wa kifedha 1.73:1 kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kutokana na ongezeko hilo ukaguzi umebaini kuna ongezeko la mwenendo mzuri wa uwiano wa mtaji uliofikia vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu wa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa Shirika kwa muda mfupi .

Kutokana na uchambuzi huo, ukaguzi umeweka alama ya msisitizo kwamba shirika limefikia kiwango kinachotakiwa ingawa inawezekana uwiano huo ukawa na makosa kwa kuzingatia Shirika kushindwa kuonesha madeni ambayo yalilipwa kwa mwaka wa fedha ilioishia 2018/2019 na kusababisha kutokuonekana kwa madeni ambayo yatapaswa kulipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.1.1 Mapungufu katika daftari la kuhifadhia Mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme Zanzibar limenunua mali za kudumu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020. Katika ukaguzi huo imebainika daftari la mali za kudumu halijafanyiwa maboresho ya kuziingiza mali mpya na kuzitoa zilizochakaa au kuharibika, jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa ugumu wa kutambua mali zillizokosekana, mali zilizoharibika, mali zilizopo na hali ya uchakavu au uzima wa mali zenyewe pamoja na kutokufahamika nambari za utambulisho wa mali hizo, kutokana na dosari hizo kumepelekea kujitokeza kwa udhaifu katika udhibiti wa mali za Shirika.

Katika kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa mali za kudumu, ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe katika kulifanyia maboresho daftari la kuhifadhia mali za kudumu kwa kuingiza taarifa zilizo sahihi kwa mujibu wa usahihi wa mali zilizopo.

3.1.2 Madeni ya muda mrefu shilingi 40,872,991,281

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Shirika kujiendesha kiufanisi. Kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.

Aidha, ukaguzi umebaini baina ya kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2018 hadi 30 Juni 2020 madeni hayo yameongezeka kutoka asilimia 10 hadi kufikia asilimia 24, mwenendo wa ukusanyaji wa madeni hayo unaonesha kuwa kati ya shilingi 78,456,504,879 zinazodaiwa hadi tarehe 30 Juni 2020 ni shilingi 37,583,513,598 zilizolipwa sawa na asilimia 47.9 na kusalia kwa deni la jumla ya shilingi 38,807,510,305 sawa na asilimia 52.1 ambazo hazijalipwa hadi ukaguzi unakamilika. Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyooneka kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 5: Madeni ya muda mrefu

	Mwaka wa fedha		
Maelezo	**30.06.2020**	**30.06.2019**	**30.06.2018**
	(Shs).	**(Shs).**	**(Shs).**
Mwenendo wa Madeni	38,807,510,305	36,188,845,046	33,105,814,933

Aidha, ukaguzi umebaini Shirika la Umeme limeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa madeni ambapo sehemu kubwa ya wanaodaiwa madeni hayo ni wadau wa Serikali kupitia Wakala ambao wanachangia uwepo wa deni la shilingi 38,807,510,305 ya jumla ya mapato yanayotokana na biashara sawa na asilimia 95.0 jambo ambalo linadhoofisha uwezo wa Shirika kufikia malengo yake.

Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyoneka katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 6: Mchanganuo wa madeni ya muda mrefu

Wadaiwa	Unguja (Shs.)	Pemba (Shs.)	Jumla(Shs.)	Asilimia
Mamlaka ya Maji Zanzibar	19,266,965,539	15,520,864,159	34,787,829,698	85
JWTZ	1,240,277,216	430,516,034	1,670,793,250	4
Idara ya Anga/Mamlaka ya Viwanja vya Ndege	883,091,173	-	883,091,173	2
Sauti ya Tanzania Zanzibar(ZBC)	438,976,830	-	438,976,830	1
Jeshi la Polisi	400,403,738	-	400,403,738	1
Wizara ya Afya	40,511,118	332,971,752	373,482,870	1
Kikosi cha KMKM	252,932,746	-	252,932,746	1
Jumla	**22,523,158,360**	**16,284,351,945**	**38,807,510,305**	**95**

Kutokana na mchanganuo wa maelezo ya jadweli lilokuwepo hapo juu jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha ukusanyaji wa madeni kutoka kwa taasisi na wakala wa Serikali ili Shirika kuweza kujiendesha kwa ufanisi na tija.

Ukaguzi unashauri Shirika la Umeme Zanzibar, kuandaa mikakati na mbinu madhubuti zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni.

3.1.3 Kutokuthibitishwa kwa deni la shilingi 14,993,787,676

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizoripotiwa na Shirika la Umeme Zanzibar, imebainika uwepo wa deni la shilingi 14,993,787,676 zinazodaiwa na Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) linalotokana na huduma ya kuuziwa umeme ambayo ni tofauti ya thamani ya kila kipimo cha umeme (unit price) na thamani halisi ya fedha.

Ukaguzi ulipitia taarifa za kikao cha Bodi ya Wakurugenzi, kikao nambari 7/2019 kilichofanyika tarehe 28 Disemba 2019 pamoja na mambo mengineyo yaliyojadiliwa maazimio ya kikao hicho yalieleza wazi wazi kwamba kiasi cha fedha kinachotakiwa kulipwa kwa TANESCO bado kipo kwenye mzozo, ambapo pande zote mbili (TANESCO na ZECO) zimeshindwa kufikia makubaliano juu ya bei kuuza kwa kila kiwango (unit) ambacho kinapaswa kulipishwa kwa ZECO.

Aidha, ukaguzi ulitumia juhudi mbali mbali ikiwemo ya kuwaandikia barua Shirika la Umeme la Tanzania (TANESCO) yenye kumbukumbu ZECO/CONF.2TNS./VOL.II/60 ya tarehe 28 Januari 2021 inayowataka kuthibitisha uwepo wa deni hilo na kujua bakaa ya deni lililolipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020.

Kutokana na hali hiyo ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi na majibu ya barua hiyo na kupelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa deni hilo. Ukaguzi unapendekeza busara na jitihada za makusudi zichukuliwe baina ya pande mbili hizo ili kutatua mgogoro kuhusu uuzwaji wa umeme kwa kila kipimo cha umeme (unit price) na thamani halisi ya fedha ili kuepuka kujitokeza kwa deni kubwa ambalo halitoweza kulipika.

3.1.4 Hali ya upotevu wa Nishati ya Umeme

Ukaguzi umefanya tathmini ya hali ya upotevu wa nishati ya umeme kwa mujibu wa taarifa za uzalishaji na usambazaji wa nishati ya umeme iliyotolewa na Idara ya Biashara ya Shirika la Umeme Zanzibar inaonesha kwamba kwa wastani kiwango cha (unit) 6,910,041 zinapotea kila mwezi ambayo ni sawa na asilimia 18.2. Upotevu huo unatokana na hali za kiufundi na hali zisizokuwa za kiufundi.

Ukaguzi umebaini kiwango cha upotevu wa nishati ya umeme ni kikubwa jambo ambalo litapelekea shirika la umeme kukosa ufanisi katika utendaji wake. Hali halisi ya upotevu huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 7: Upotevu wa nishati ya umeme

Namba	Mwezi	Kiwango cha Umeme kinachonunuliwa TANESCO (Unit)	Kiwango cha Umeme kinachouzwa na ZECO (Unit)	Kiwango cha Umeme kinachopotea (Kiufundi/ Kibiashara)	Asilimia ya Upotevu
1	Julai,2019	36,521,000	29,672,532	6,848,468	18.8
2	Agosti,2019	38,284,000	31,209,910	7,074,090	18.5
3	Septemba,2019	36,740,000	29,894,691	6,845,309	18.6
4	Oktoba,2019	38,314,000	31,192,839	7,121,161	18.6
5	Novemba,2019	40,257,000	32,713,155	7,543,844	18.7
6	Disemba ,2019	42,523,000	34,801,957	7,721,043	18.2
7	Januari,2020	44,927,000	36,674,570	8,252,429	18.4
8	Febuari,2020	44,854,000	36,599,868	8,254,131	18.4
9	Machi,2020	41,860,000	34,269,787	7,590,213	18.1
10	April,2020	29,886,000	24,746,641	5,139,358	17.2
11	Mei,2020	30,305,000	24,999,412	5,305,588	17.5
12	Juni,2020	29,586,000	24,361,141	5,224,858	17.7
Jumla		**454,057,000**	**371,136,505**	**82,920,494**	**18.6**
Wastani kwa Mwezi		**37,838,083**	**30,928,042**	**6,910,041**	**18.2**

Kutokana na mchanganuo wa hali ya upotevu wa umeme kama ilivyooneshwa katika jadweli la hapo juu, ukaguzi umebaini mwenendo wa upotevu wa nishati ya umeme umefikia asilimia 18.2 kwa vipindi vya miaka mitatu mfululizo na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ili kupunguza upotevu wa nishati hiyo jambo ambalo limepelekea Shirika kutokuwa na ufanisi katika utendaji wake.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe na uongozi wa Shirika la Umeme ili kuweza kupunguza kiwango cha upotevu wa nishati ya umeme pamoja na kuwachukulia taratibu za kisheria wale wote watakaobainika wanafanya vitendo vya uhujumu wa kujiungia umeme bila kufuata sheria.

3.1.5 Kushindwa kufanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme lilifanya makubaliano na Kampuni ya M/s Trace Associate Ltd kwa ajili ya kufanya tathmini ya thamani ya mali za kudumu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 lakini ukaguzi umeshindwa kupata ripoti ya tathmini ya thamani ya mali za kudumu ambazo hazikuwahi kufanyiwa tathmini kwa kipindi hicho na zinahitaji muendelezo wa tathmini hiyo iweze kufanyika ambapo hadi ukaguzi unakamilika ripoti ya tathmini ya mali zifuatazo hazikupatikana kwa ukaguzi.

Mchanganuo wa mali hizo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 8: Thamani ya mali za kudumu

Aina ya Mali za Kudumu	Thamani (Shs) 30.06.2020	Thamani ya Uchakavu (Shs) 30.06.2020	Thamani Halisi ya Sasa (Shs) 30.06.2020
Ardhi	249,678,000	-	249,678,000
Majengo	2,631,511,402	1,222,349,756	1,409,161,646
Mitambo/Vifaa	139,729,355	8,150,879	131,578,476
Jumla	**3,020,918,757**	**1,230,500,635**	**1,790,418,122**

Kutokana na mchanganuo unao onekana hapo juu, jumla ya thamani halisi ya mali za kudumu za shilingi 1,790,418,122 zimekosa ripoti ya tathmini hiyvo kupelekea thamani ya jumla ya mali za kudumu ya shilingi 274,648,029,694 iliyopelekea hesabu za mwisho wa mwaka kuripotiwa kimakosa.

3.1.6 Dosari katika mfumo wa urejeshwaji wa mikopo kwa wateja wapya

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Umeme limeandaa sera ya utoaji wa huduma ya nishati ya umeme kwa wateja wapya kwa njia ya mikopo ambapo wateja hao hutakiwa kulipa mikopo hiyo kwa muda kati ya miezi sita, miezi kumi na mbili na miezi kumi na nane kulingana na makubaliano yaliyoingiwa baina ya Shirika na wateja waliokopeshwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya orodha ya wateja wapya waliounganishiwa umeme kwa njia ya mkopo na kubainika kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020 Shirika la Umeme lilitoa mkopo wenye thamani ya shilingi 300,941,190. Ukaguzi ulibaini mwenendo wa urejeshwaji wa mikopo hiyo hauridhishi baada ya kukosa taarifa za urejeshwaji wa mikopo hiyo kutoka katika mfumo unaotumiwa na shirika (SUPREMA SYSTEM) ambapo mfumo huo umeshindwa kuonyesha deni la mteja mmoja mmoja, kiwango anachodaiwa, kiwango kilicholipwa na bakaa ya deni lililobakia, jambo ambalo limepelekea kusababisha ugumu wa kujiridhisha uwepo wa kiwango sahihi kinachodaiwa, kilicholipwa na kilichobakia kutokana na taarifa hizo kurikodiwa katika madaftari.

Kutokutumika kwa mfumo kwenye ukusanyaji wa madeni kunapelekea kushindwa kujiridhisha kwa uwepo na ulipwaji wa madeni hayo na hivyo kunaweza kulipelekea shirika kulikosesha mapato.

3.1.7 Kushindwa kutumika kwa Mfumo wa Uhasibu wa Kielektroniki wa USD 65,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Umeme lilifanya malipo ya jumla dola za kimarekani 65,000 kwa ajili ya kununua mfumo wa Kielektroniki (SAP) ulionunuliwa Juni 2005 ambao umekusudiwa kushughulikia kazi za uhasibu, rasilimali watu, uhifadhi wa mali za kudumu na kazi za manunuzi. Ukaguzi umebaini shirika la umeme bado linaendelea kufanya shughuli za uhasibu ikiwemo utayarishaji wa hati za malipo, uwekaji wa taarifa za fedha kwenye madaftari ya kumbukumbu za fedha (manual system).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na mwongozo wa uhasibu wa Shirika la Umeme (Corporation Accounting Manual) kifungu nambari 17.1 ambapo kinaelezea utengenezaji wa taarifa za kifedha zifanyike kwa kutumia njia ya mfumo wa kielektroniki (SAP Package).

Maoni ya Ukaguzi

Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Umeme Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonyesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Umeme Zanzibar limepata Hati inayoridhisha yenye aya za msisitizo yaliyotajwa hapo juu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.2 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA PBZ KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2019.

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinavyotumiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar vilivyowekwa na msimamizi wa Taasisi za Kifedha Tanzania (BOT), Benki ya Watu wa Zanzibar inafunga hesabu zake kwa kutumia mwaka wa fedha unaoanzia Januari hadi Disemba. Kutokana na hali hiyo hesabu zilizofungwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2019 hesabu hizo huwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu tarehe 30 Machi 2020 kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 na ripoti ya ukaguzi huo huonekana katika kitabu cha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinachowasilishwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Muundo wa Mtaji (Capital Structure)

Kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba, 2019 Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa na mtaji wa hisa ulioidhinishwa unaofikia hisa za kawaida 600,000,000 (ordinary shares) ambapo kwa kila hisa moja ilikuwa na thamani ya shilingi 100. Kiwango cha hisa killichotolewa na kulipwa na mmiliki wa benki ambae ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kilikuwa ni idadi ya hisa 310,000,000 kwa thamani ya shilingi 100 kwa hisa.

Taarifa ya mapato

Ukaguzi umebaini mapato yatokanayo na riba yameongezeka kutoka shilingi milioni 52,255 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi milioni 48,435 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018, kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 3,820 sawa na asilimia 8. Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na riba kumepelekea kuongezeka kwa mapato ya mikopo.

Baina ya mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 na 2019 mapato yasiyo ya riba yamepungua kutoka shilingi milioni 2,944 na kufikia milioni 22,046 ukilinganisha na shilingi milioni 24,990 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018.

Kupungua kwa mapato yasiyokuwa na riba kumetokana na faida ndogo ya ubadilishwaji wa fedha za kigeni ukilinganisha na kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018.

Taarifa ya matumizi

Ukaguzi umebaini kuongezeka kwa gharama za matumizi ya riba kutoka shilingi milioni 11,769 kwa mwaka unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi milioni 9,898 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018, kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 1,871 sawa na asilimia 19 ya ongezeko. Kuongezeka kwa gharama za matumizi ya riba kumetokana na kuongezeka kwa gharama kubwa ya Amana (higher cost of deposit), kuanzishwa kwa Viwango vya Uhasibu (IFRS 16) na kupelekea kuongezeka kwa gharama za malipo ya riba (Interest charge expenses on lease payable). Kwa hivyo kiasi cha riba kilipungua kutoka asilimia 79 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 na kufikia asilimia 78 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, imebainika gharama za uendeshaji zimeongezeka kutoka shilingi milioni 30,968 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 hadi kufikia shilingi milioni 36,907 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 5,939 sawa na asilimia 19 ya ongezeko.

Ongezeko la gharama za uendeshaji limetokana na uwepo wa gharama za uchakavu wa Mali za kudumu, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kunatokana na uwepo wa miradi mipya (VISA Card, Bureau de change nk). Kutokana na hali hiyo kumepelekea kuongezeka kwa uwiano wa mapato ya gharama (cost-income ratio) na kufikia asilimia 63 ukilinganisha na asilimia 62 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA BENKI YA WATU WA ZANZIBAR

Ufanisi katika Uendeshaji wa Benki

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Benki kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 na Disemba 2019.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 Benki ya Watu wa Zanzibar imepata faida ya shilingi milioni 32,066 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambayo ni shilingi milioni 27,564 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 4,502 sawa na asilimia 16.33, faida iliyoonekana hapo ilipatikana kabla ya kulipa kodi.

Gawio la Benki ya Watu wa Zanzibar

Kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2019 Benki ya Watu wa Zanzibar ilipata faida ya shilingi 32,066 milioni ukilinganisha na shilingi 27,564 milioni kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018, faida hiyo ilipatikana kabla ya tozo ya kodi. Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, Benki ya Watu wa Zanzibar kupitia kikao cha Bodi ya Wakurugenzi kiliidhinisha malipo ya mgao wa gawio la shilingi 4,518 milioni ukilinganisha na mwaka wa fedha 2018 ambapo iliidhinishwa malipo ya mgao wa gawio la shilingi 3,718 milioni, malipo hayo ni kutokana na sera ya gawio la Benki ya PBZ.

Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 9: Mchanganuo wa Gawio

Mgawanyo uliopendekezwa kwa kila hisa	Mwaka wa Fedha, Disemba, 2019	Mwaka wa Fedha Disemba, 2018
Mgawanyo wa gawio (Shs '000)	4,518,290	3,717,796
Idadi ya hisa	310,000,000	310,000,000
Gawio kwa kila hisa (Shs)	14.6	12
Gawio kwa kila hisa iliyotanganzwa na kulipwa :		
Mgawanyo wa gawio (Shs '000)	3,717,796	2,625,110
Idadi ya hisa	310,000,000	310,000,000
Gawio kwa kila hisa	12	8.45

Kwa upande wa faida baada ya tozo ya kodi imeonekana kuongezeka na kufikia shilingi milioni 26,892 kwa mwaka wa fedha 2019 ukilinganisha na faida ya shilingi milioni 18,588 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2018 ambapo imefanya ongezeko la shilingi milioni 8,304 sawa na asilimia 45. Mchanganuo wa maelezo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 10: Taarifa ya faida na hasara

	2019 "000,000" Shs.	2018 "000,000" Shs.	increase/ (decrease) "000,000" Shs.	% change
Interest income	52,255	48,435	3,820	8%
Interest expenses	(11,769)	(9,898)	1,871	19%
Net interest income	**40,486**	**38,537**	**1,949**	**5%**
Fees and commission income (Net)	7,276	5,796	1,480	26%
Income from Financing and Investment receivable	5,862	5,662	200	4%
Foreign Currency exchange income (Net)	6,048	8,467	(2,419)	(29%)
Other operating income	2,860	5,065	(2,205)	(44%)
Net non-interest income	**22,046**	**24,990**	**(2,944)**	**(12)**
Net operating income before impairment charge	**62,532**	**63,527**	**(995)**	**(2%)**
Expected Credit Loss - loan and financing	4,428	(4,548)	8,976	97%
Provision for probable loss of other assets	2,898	-	2898	100%
Non-performing Assets written off	(885)	(447)	438	98%
Net operating income	**68,973**	**58,532**	**10,441**	**18%**
Personnel/Staff cost	(13,504)	(11,811)	1,693	15%
General and administration costs	(15,215)	(12,594)	2,621	21%
Other operating expenses	(8,188)	(6,563)	1,625	25%
Total operating expenses	**(36,907)**	**(30,968)**	**5,939**	**19%**
Profit before tax	**32,066**	**27,564**	**4,502**	**16%**

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukaguzi umebaini kwamba jumla ya mali za Kudumu za Benki (Total Asset) zimeongezeka kutoka shilingi milioni 658,420 kwa mwaka wa fedha 2018 na kufikia shilingi milioni 723,686 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 65,266 sawa na asilimia 10. Ongezeko hilo limesababishwa na uwepo wa kiwango kikubwa cha mikopo.

Ukaguzi umebaini mikopo na malipo ya awali yameongezeka kutoka shilingi milioni 274,692 kwa mwaka 2018 na kufikia shilingi milioni 331,953 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 57,261 sawa na asilimia 21. Ongezeko hilo limesababishwa kutokana na mipango mikakati ya benki na muelekeo wa kufikia vipaumbele vya Benki ya Watu wa Zanzibar.

Kiwango cha fedha taslimu na bakaa la fedha zilizopo Benki kuu ya Tanzania zimeongezeka kutoka shilingi milioni 111,012 kwa mwaka wa fedha 2018 na kufikia shilingi milioni 143,698 kwa mwaka wa fedha 2019 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 32,686 sawa na asilimia 30. Ongezeko hilo linachangiwa na ongezeko la Akiba iliyohifadhiwa BOT (Statutory Minimum Reserves - SMR) kwa fedha za kigeni na za ndani.

Aidha, ukaguzi umebaini uwekezaji katika dhamana za serikali (Investment in Government Securities) umepungua kutoka shilingi milioni 130,983 kwa mwaka wa fedha 2018 hadi kufikia shilingi milioni 89,683 kwa mwaka wa fedha 2019 kukiwa na upungufu wa shilingi milioni 41,300 sawa na asilimia 32. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa riba inayotokana na dhamana (Interest offered in the securites).

Kwa mwaka wa fedha 2019, ukaguzi umebaini deni la amana za wateja (customer deposit liability) limeongezeka kutoka shilingi milioni 526,046 kwa mwaka wa fedha 2018 na kufikia shilingi milioni 574,826 kwa mwaka wa fedha 2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 46,780 sawa na asilimia 9. Aidha, ukaguzi umebaini mapato yatokanayo na akiba nyenginezo (Retained earnings and other reserves) yameongezeka kutoka shilingi milioni 79,664 kwa mwaka wa fedha 2018 na kufikia shilingi milioni 102,803 kwa mwaka wa fedha 2019 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 23,139 sawa na asilimia 30.

Ukaguzi umebaini utendaji wa kibiashara wa Benki ya Watu wa Zanzibar umezidi kuimarika ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioishia Disemba 2018.

Ukaguzi umebaini uwekezaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar katika dhamana za Serikali (Bank's Investment in Government Security) imeongezeka na kufikia shilingi milioni 61.9 kwa mwaka wa fedha 2019 ukilinganisha na shilingi milioni 26.6 kwa mwaka wa fedha 2018 kukiwa na ongezeko la shilingi milioni 33.3 sawa na asilimia 125.

Mtiririko wa hali ya kifedha

Kwa mwaka 2019, imebainika uwekezaji wa Benki katika dhamana za Serikali umeongezeka na kufikia shilingi bilioni 33.3 ukilinganisha na kupungua kwa uwekezaji huo kwa shilingi bilioni 61.9 kwa mwaka 2018.

Aidha, dhamana ya mikopo ya wateja imebainika kupungua na kufikia shilingi bilioni 43.9 ukilinganisha na upungufu uliobainika mwaka 2018 wa shilingi bilioni 7.5.

Hata hivyo imebainika amana za wateja (deposit from customers) zimeongezeka na kufikia shilingi bilioni 55.1 ukilinganisha na ongezeko la shilingi bilioni 23.1 kwa mwaka 2018. Kutokana na mchanganuo huo wa fedha imebainika uwekezaji wa amana za wateja ndio lengo kuu linalopelekea mtiririko wa fedha unaotokana na shughuli za benki.

Ukaguzi umebaini kwamba, Benki ya Watu wa Zanzibar inaendelea kuwa na msimamo mzuri wa hali ya kifedha na ukwasi katika kutimiza malengo ya uanzishwaji wa benki hiyo.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.2.1 Kutokutekeleza muongozo wa Benki Kuu (BOT)

Kutokana na muongozo wa BOT juu ya utekelezaji wa mfumo wa uhasibu (IFRS 9) unaeleza kwamba, mfumo wa upoteaji wa mkopo unaotarajiwa (expected credit loss - ECL) chini ya IFRS 9 kwa madhumuni ya udhibiti wa vifungu vya uhasibu, benki na taasisi za fedha zinahitajika kufanya ukaguzi wa mkopo na kusahihisha kasoro zao angalau mara moja kwa kila robo mwaka ili kuweza kuakisi viashiria hatarishi vya mikopo tangu mkopo ulipotoka.

Benki pamoja na taasisi za kifedha zinatakiwa kuhakikisha kwamba taratibu zote za kibenki zinafuatwa katika kuamua kiwango cha upotevu wa mkopo na kuhakikisha kuwa nyaraka zinahakikiwa na kusainishwa mara kwa mara.

Ukaguzi umebaini kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar, bado haijaandaa kielelezo cha nyaraka kinachohusiana na hali hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba inatekeleza miongozo iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Benki ya Watu wa Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 31 Disemba, 2019 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Benki ya Watu wa Zanzibar limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba, 2019.

TAARIFA ZA UKAGUZI WA HESABU ZA PBZ KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA 31 DISEMBA, 2020.

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinavyotumiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar vilivyowekwa na msimamizi wa Taasisi za Kifedha Tanzania (BOT), Benki ya Watu wa Zanzibar inafunga hesabu zake kwa kutumia mwaka wa fedha unaoanzia Januari hadi Disemba. Kutokana na hali hiyo hesabu zilizofungwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2020 hesabu hizo huwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu tarehe 6 Januari 2020 kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016

Taarifa ya mapato

Ukaguzi umebaini mapato yatokanayo na riba yameongezeka kutoka shilingi 52,254,999,740 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 62,726,498,962 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, kukiwa na ongezeko la shilingi 10,471,499,222 sawa na asilimia 16.7 ya ongezeko. Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na riba kumepelekea kuongezeka kwa mapato makubwa ya mikopo.

Taarifa ya matumizi

Ukaguzi umebaini kupungua kwa gharama za matumizi ya riba kutoka shilingi 11,769,476,447 kwa mwaka unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 10,918,994,250 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, kukiwa na upungufu wa shilingi 850,482,197 sawa na asilimia 7.8 ya upungufu. Hali hii imetokana na kupungua kwa gharama kubwa ya Amana.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, imebainika gharama za uendeshaji zimeongezeka kutoka shilingi 36,906,940,131 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 hadi kufikia shilingi 39,363,545,784 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020, kukiwa na ongezeko la shilingi 2,456,605,653 sawa na asilimia 6.2 ya ongezeko.

Hali hii imebainika kutokana na uwepo wa gharama kubwa za uchakavu wa mali za kudumu.

Ufanisi katika Uendeshaji wa Benki

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Benki kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 na Disemba 2020.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2020 Benki ya Watu wa Zanzibar imepata faida ya shilingi 18,712,542,933 ukilinganisha na faida ya shilingi 32,066,230,084 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 kukiwa na upungufu wa shilingi 13,353,687,151 sawa na asilimia 71.4.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.2.2 Mapato ya ujira ambayo hayakupokelewa shilingi 395,889,294.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Mapato imeingia mkataba na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na walipa kodi. Kwa mujibu wa kifungu 8.2 cha makataba kimebainisha asilimia 0.1 ya kodi ilipaswa kukusanywa na kuwa ujira kwa PBZ.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 PBZ ilistahiki kulipwa jumla ya shilingi 395,889,294 kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA) kupitia Benki kuu Tanzania (BOT). kutokana na hadi ukaguzi uliofanyika imebainika kujitokeza kwa kasoro mbali mbali za utekelezaji wa mkataba huo kama ifuatavyo:-

Kubainika kwa kumalizika muda wa makubaliano ya mkataba wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ujira tokea Februari.

Benki ya Watu wa Zanzibar kuendelea kukusanya mapato hayo bila ya makubaliano ya mkataba kwanzia Febuari 2019 hadi 30 Juni, 2020 bila ya kupokea ujira kutoka TRA.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuhakikisha fedha hiyo inalipwa ikiwemo na kufunga makubaliano ya mkataba mpya ambao utaleta tija kwa pande zote mbili.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Benki ya Watu wa Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Benki ya Watu wa Zanzibar limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba, 2020.

3.3 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Taarifa ya Mapato

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 mapato ya Bodi ya Mapato Zanzibar yameonekana kupungua kutoka shilingi 18,718,463,125 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 13,346,730,968 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 5,371,732,157 sawa na asilimia 28.7.

Aidha Bodi ya Mapato Zanzibar ikiwa ni wakala wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato katika mwaka wa fedha 2019/2020 Bodi ya mapato Zanzibar ilikadiriwa kukusanya mapato ya shilingi bilioni 605.32 kutoka katika vyanzo mbali mbali vya kodi na tozo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi bilioni 463.73 zimekusanywa sawa na asilimia 76.71 ya makadirio.

Mapato ya Bodi ya Mapato Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi bilioni 439.08 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi bilioni 463.73 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi bilioni 24.65 sawa na asilimia 5.61.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 wastani wa makusanyo kwa mwezi yameongezeka hadi kufika shilingi bilioni 38.64 ikilinganishwa na wastani wa shilingi bilioni 36.59 kwa mwaka 2018/2019.

Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 11: Mapato ya ZRB kwa mwaka 2019/2020

Namba	Chanzo cha Mapato	Makadirio ya Mapato 2019/2020 (Shs. Bilioni)	Mapato Halisi 2019/2020 (Shs. Bilioni)	Asilimia
1	Kodi ya Ongezeko la thamani	203.65	148.92	73.13
2	Ushuru wa bidhaa	36.95	28.63	77.48
3	Ushuru wa Hoteli	48.48	26.99	55.67
4	Ushuru wa Mgahawa	7.95	5.74	72.2
5	Ushuru wa waendesha huduma ya Kitalii	2.19	1.47	67.12
6	Ushuru wa Stempu	13.24	10.06	75.98
7	Malipo ya Kiwanja cha Ndege	52.57	41.06	78.11
8	Malipo ya Bandari	6.46	4.38	67.8
9	Mfuko wa maendeleo ya barabara	15.47	10.14	65.55
10	Ushuru wa Mafuta	53.94	41.07	76.14
11	Makusanyo ya Wizara	116.81	109.47	93.72
12	Usajili wa magari	1.74	1.65	94.83
13	Leseni ya barabara	5.88	3.9	66.33
14	Leseni ya udereva	2.01	1.45	72.14
15	Ada ya usalama wa raia Uwanja wa ndege	12.06	9.13	75.7
16	Kodi ya Miundombinu	25.92	19.67	75.89
	Jumla	**605.32**	**463.73**	**76.61**

Kutokana na mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo juu, ukaguzi umebaini Bodi ya Mapato Zanzibar imeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 23.39.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Bodi ya Mapato Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi katika kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwa wafanyabiashara pamoja na kuweka udhibiti mzuri wa mifumo hiyo ili Bodi kupunguza na kuondosha mianya ya uvujaji wa mapato na ukwepaji wa kodi.

Taarifa ya Matumizi

Kwa mwaka fedha 2019/2020 Bodi ya Mapato ya Zanzibar ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 16,504,633,531 Kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Bodi ya mapato ya Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 13,971,951,102 kwa ajili ya kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 85 ya makadirio.

Matumizi ya Bodi ya Mapato Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 11,381,939,963 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 13,971,951,102 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,590,011,139 sawa na asilimia 22.75. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 12: Matumizi ya ZRB kwa mwaka 2019/2020

Aina ya Matumizi	Makadirio (Shs)	Matumizi Halisi (Shs)	Asilimia
Matumizi ya utawala	13,820,082,751	11,358,261,215	82
Matumizi ya Uajiri na Mafunzo	1,245,960,000	403,346,923	32
Matumizi ya Ukarabati na Matengenezo	257,610,000	223,178,423	87
Matumizi mengineyo	1,180,980,780	877,616,449	74
Uchakavu wa Mali za Kudumu	-	1,109,548,092	(100)
Jumla	**16,504,633,531**	**13,971,951,102**	**85**

MATOKEO YA UKAGUZI

3.3.1 Kushindwa kutenganisha Ardhi na Majengo katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,530,308,731

Katika hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia 30 Juni, 2020 imebainika Bodi ya Mapato imeripoti thamani ya ardhi na majengo jumla ya shilingi 7,530,308,731, zinazomilikiwa Unguja na Pemba.

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vya kimataifa (IPSAs 17) aya ya74 inaeleza ya kwamba "Ardhi na majengo ni mali zinazoweza kutenganishwa na kuhesabiwa kwa thamani tofauti, hata kama uwepo wa mali hizo zinapatikana kwa pamoja".

Kiwango cha mali za kudumu za muda mrefu kilichoanishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia 30 Juni, 2020 hakikuzingatia matakwa ya viwango vya ufungaji wa hesabu vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

3.3.2 Taarifa za fedha ambazo hazikufanyiwa usuluhishi wa kibenki kwa muda mrefu.

Katika ukaguzi uliofanywa kwenye taarifa za usuluhishi wa benki ilibainika uwepo wa taarifa za kibenki ambazo hazikufanyiwa usuluhishi (reconcilliation) kwa muda mrefu kama inavyoonekana hapo chini:-

(a) Uwepo wa Madeni yanayodaiwa benki kwa muda mrefu hesabu nambari 021103000475 shilingi 127,887,545

Katika kufanya mapitio ya hesabu nambari 021103000475 (retention account) inayomilikiwa na Bodi ya Mapato iliyopo Benki ya Watu wa Zanzibar ilibainika uwepo wa deni la muda mrefu tangu mwaka, 2018 yenye thamani ya shilingi 138,108,385 ambayo yamepungua hadi kufikia shilingi 127,887,545 katika mwaka wa fedha 2020.

Kutokana na uwepo wa taarifa hiyo ukaguzi haukuweza kuona jitihada zilizochukuliwa na Bodi ya Mapato katika kuhakikisha kuwa fedha hizo zinafanyiwa usuluhishi wa kibenki, ambapo katika taarifa ya hesabu hazikuweza kuonekana.

Kutokana na dosari zilizobainika ni vyema Uongozi wa Bodi kufanya jitihada za makusudi katika kuhakikisha kasoro zilizobainishwa zinafanyiwa kazi kwa haraka ili kuweza kuonesha sura sahihi na halisi katika ufungaji wa hesabu.

(b) Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uwepo wa deni la wadai shilingi 4,520,873,299

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa deni la shilingi 4,520,873,299 ambalo limeripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka lakini vielelezo vya kuweza kuthibitisha uwepo wa deni hilo havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha ukweli na usahihi wa kiasi kinachodaiwa.

Orodha ya wadai hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 13: Madeni ya wadai yaliyokosa vielelezo

Namba	Maelezo	Mwaka wa fedha 2019/2020 (Shs)
1	Rahisi Solutions Ltd	71,486,995
2	Advent Construction Ltd	1,200,000,000
3	BITZ Company Ltd	49,386,304
4	Norway Registers Devas	3,200,000,000
Jumla		**4,520,873,299**

3.3.3 Taarifa ya Madeni ya Kodi

(a) Madeni ya kodi ya muda mrefu shilingi 27,322,335,187

Ukaguzi ulipitia taarifa za madeni iliyoandaliwa na kitengo cha usimamizi wa madeni katika kipindi cha miaka miwili iliyoisha 2018/2019 na 2019/2020. Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 27,322,335,187 ni madeni ya muda mrefu ya walipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT). Kati ya deni hilo shilingi 26,384,159,034 ni fedha zililipwa na walipakodi kimakosa kwenda katika hesabu za TRA Dar es Salaam badala Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na shilingi 938,176,153 ni deni ambalo halijalipwa.

Kushindwa kukusanya madeni ya kodi kunapelekea Serikali kukosa mapato yanayotokana na kodi.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Bodi ya Mapato kuhakikisha kuwa juhudi zaidi zinafanywa za kulipwa kwa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni husika ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 14:Madeni ya kodi ya muda mrefu

Namba	Jina la Mlipa Kodi	Tarehe ya Ukaguzi wa Kodi	Deni Halisi la Kodi Ambalo Halijalipwa (Shs)	Fedha Zilizolipwa Kimakosa TRA (Shs)	Maelezo ya Deni
1	Dezo Construction	Tathmini nambari 13 ya tarehe 19/12/2019	897,388,659	-	Deni Halijalipwa
2	Dullah Motors Limited	Tathmini nambari 36 ya tarehe 20/05/2019	40,787,494	-	Deni Halijalipwa
3	MIC (Tigo)	2011-2015	-	14,500,000,000	Kodi ya VAT iliolipwa TRA DSM kimakosa
4	VAT	2015-2017	-	11,884,159,034	Kodi ya VAT iliolipwa TRA DSM kimakosa
Jumla			**938,176,153**	**26,384,159,034**	

(b) Madeni ya Kodi ya muda mrefu ambayo hayajasuluhishwa shilingi 20,515,860,319 na dola za kimarekani USD 4,110,033

Ukaguzi ulipitia taarifa za madeni iliyoandaliwa na kitengo cha usimamizi wa madeni kutoka mwaka 2013/2014 hadi 2019/2020. Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 20,927,104,389 na dola za Kimarekani 4,135,033 ikiwa ni madeni ya muda mrefu ya walipa Kodi ambayo yapo katika malalamiko.

Aidha katika ufuatiliaji wa ulipaji wa madeni hayo jumla ya shilingi 411,244,070 na dola za Kimarekani 25,000 zililipwa na wadaiwa hao. Hata hivyo tathmini ilionesha kwamba jumla ya shilingi 20,515,860,319 na dola za kimarekani 4,110,033 ikiwa ni bakaa la deni ambalo limeshindwa kulipwa na walipa kodi kwa wakati.

Kushindwa kukusanya madeni ya kodi ambayo yapo kwa muda mrefu kunapelekea Serikali kukosa mapato yanayotokana na kodi na kusabibisha upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Bodi ya Mapato kuhakikisha kuwa juhudi zaidi zinachukuliwa ili kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati. Mchanganuo wa madeni husika ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 1.**

Maoni ya Ukaguzi

Hati Isiyoridhisha

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Bodi ya Mapato Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Bodi ya Mapato Zanzibar limepata hati isiyoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.4 SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR (ZIC)

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinavyotumiwa na Shirika la Bima la Zanzibar vilivyowekwa na msimamizi wa mashirika ya bima Tanzania (TIRA), Shirika la Bima linafunga hesabu zake kwa kutumia mwaka wa fedha unaoanzia Januari hadi Disemba. Kutokana na hali hiyo hesabu zilizofungwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2019 hesabu hizo huwasilishwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu tarehe 30 Machi 2020 kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016 na ripoti ya ukaguzi huo huonekana katika kitabu cha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinachowasilishwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umefanya uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Bima la Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka hadi kufikia 19,853,482,000 kwa mwaka wa fedha unaioshia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 19,220,931,000 kwa mwaka wa fedha unaioshia Disemba 2018 kukiwa na ongezeko la shilingi 632,551,000 sawa na asilimia 3.29 ya ongezeko.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji zimepungua hadi kufikia shilingi 16,914,971,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 17,109,002,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambayo ni upungufu wa shilingi 194,031,000 sawa na asilimia 1.13.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR

(a) Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika (Operating Performance)

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa shirika kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 na Disemba 2019 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini kutokana na uchambuzi wa taarifa ya faida/hasara (Statement of Profit and Loss Account).

Jadweli Nambari 15: Taarifa ya faida na hasara.

	2019 Shs. '000'	2018 Shs. '000'
Gross Written Premium	23,185,279	21,187,222
Reinsurance premium in ward	136,233	-
Outward Reinsurance	(4,729,487)	(3,548,530)
Net Written Premium	18,592,025)	17,638,692
Change in Gross Unearned Premium Reserve (UPR)	(1,214,485)	(183,303)
Reinsurers' Share of UPR	712,496	(271,948)
Net Earned Premium	18,090,036	17,183,441
Other Income	1,316,426	1,372,132
Foreign Exchange Gain/(Loss)	(8,824)	57,695
Commissions Earned	455,844	607,663
Net Income	**19,853,482**	**19,220,931**
CLAIMS AND OTHER OPERATING EXPENSES		
Claims Incurred	6,683,702	6,117,494
Commission Incurred	2,285,514	3,680,879
Staff Costs	2,615,075	2,317,651
Directors 'Remuneration	183,901	244,939
Depreciation and Amortization	281,404	374,431
Auditors' Remuneration	60,000	60,000
Premium Tax and License	265,538	4,360
Provision for Impairment Losses	-	231,324
Operating and Other Expenses	4,539,335	4,077,924
TOTAL EXPENSES	**16,914,469**	**17,109,002**
Pretax Profit	2,939,013	2,111,929
Tax Expense	(420,000)	(570,248)
Profit For the Year	**2,519,013**	**1,541,681**
Proposed/Paid Dividend	**(406,069)**	**(348,336)**
Total Comprehensive Income	**2,112,944**	**1,193,345**

Uchambuzi wa jadweli linaloonekana hapo juu linaonesha ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Bima la Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka kufikia shilingi 19,853,482,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 19,220,931,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 kukiwa na ongezeko la shilingi 632,551,000 sawa na asilimia 3.29 ya ongezeko.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji zimepungua hadi kufikia shilingi 16,914,971,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na shilingi 17,109,002,000 kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 2018 ambao ni upungufu wa shilingi 194,031,000 sawa na asilimia 1.13.

Kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 Shirika la Bima Zanzibar limepata faida ya shilingi 2,939,013,000 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambayo ni shilingi 2,111,929,000 kukiwa na ongezeko la shilingi 827,084,000 sawa na asilimia 28 ya ongezeko, faida iliyoonekana hapo ilipatikana kabla ya kulipa kodi.

Shirika la Bima la Zanzibar limefanya malipo ya kodi kwa mujibu wa sheria ya kodi yenye thamani ya shilingi 406,069,000 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambapo Shirika limefanya malipo ya shilingi 348,336,000 malipo hayo yanalipwa kulingana na faida inayopatikana.

Kwa upande wa faida baada ya tozo ya kodi iliyoripotiwa katika jadweli hapo juu imeonekana kuongezeka na kufikia shilingi 2,112,944,000 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na faida ya shilingi 1,193,345,000 iliyopatikana kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018 ambapo imefanya ongezeko la shilingi 919,599,000 sawa na asilimia 43.5.

Angalizo:

Ikiwa vyanzo vya mapato havikubainishwa vizuri na Shirika kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima kunaweza kupelekea Shirika kushindwa kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

(b) Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Shirika la Bima la Zanzibar kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 16: Taarifa ya Utendaji wa kifedha

	Mwaka wa Fedha 31.12.2019 Shs.	**Mwaka wa Fedha 31.12.2018 Shs.**
Mali za muda mfupi (Total current Assets)	23,556,995,000	21,010,451,000
Dhima za muda mfupi (Total Current Liabilities)	22,223,005,000	17,775,232,000
Mali Halisi za muda mfupi (Working Capital)	1,333,990,000	3,235,219,000
Mtaji (Net Worth)	14,566,000,000	15,080,517,000
UWIANO:		
Uwiano (current ratio)	1.06:1	1.2:1
Kipimo cha Uwiano (Normal Current Ratio)	**2:01**	2:01

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi umepungua kufikia uwiano wa 1.06:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 ukilinganisha na uwiano wa 1.2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2018, kutokana na upungufu huo, ukaguzi umebaini kuna upungufu wa uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi.

Hali hii kama ikiendelea Shirika linaweza kushindwa kumudu madeni ya muda mfupi na kupelekea kushindwa kulipa madai ya bima (Insurance Claims) kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu vya uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupini uwiano wa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuboresha uwiano wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupikwa kuzingatia Mawakala na Madalali kuweza kufuata Sheria za Bima ikiwemo kuwasilisha malipo yaliyokusanywa kwa wakati.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.4.1 Kuchelewa kuwasilishwa kwa taarifa za hesabu kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha Za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu cha 119(1) kinaeleza wajibu wa taasisi kufunga na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha husika.

Shirika la Bima Zanzibar limefunga hesabu zake za mwisho wa mwaka na hazikuwasilishwa kwa wakati. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 119(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

3.4.2 Kushindwa kufanya ufuatiliaji wa malipo kwa wakati kutoka kwa Mawakala na Madalali

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kupitia kitengo cha masoko kwamba makusanyo makubwa ya fedha bado yanabakia mikononi mwa Madalali na Mawakala wa bima katika matawi yote ya Shirika la Bima la Zanzibar, jambo ambalo linaweza kupelekea kushindwa kulipa madeni ya muda mfupi na hatimae kushindwa kulipa madai ya bima kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha masoko hakikuchukua jitihada kuhakikisha kwamba fedha zote zilizopo mikononi mwa Mawakala na Madalali zinawasilishwa kwa wakati kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Bima la Zanzibar kupitia kitengo cha masoko kuhakikisha kinatekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwemo kufuatilia na kuhakikisha Mawakala na Madalali wanazingatia sheria na kanuni za Shirika la Bima pamoja na kuwasilisha mapato yao kwa wakati.

3.4.3 Malipo ya madai yaliyolipwa kinyume na sera ya madai ya Shirika la Bima shilingi 87,613,000

Katika ukaguzi uliofanyika tumefanya tathmini ya madai yaliolipwa na Shirika la Bima la Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, ukaguzi umebaini kwamba malipo ya madai yaliyolipwa na Shirika kwa wateja mbali mbali waliopata ajali yalifanyika kinyume na sera ya bima ya magari.

Aidha, imebainika Shirika limefanya malipo kwa mtu aliyepata ajali (Third party injuries/ death to a pedestrian) ambayo hayakuoneshwa kwenye sera ya bima ya magari. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli nambari 17: Malipo yaliyolipwa kinyume na sera ya madeni

Namba	Nambari ya Hati	Nambari ya Madai	Nambari ya Hundi	Jumla ya Fedha (Shs)	Maelezo	Tawi Husika
1	075341/2019	020/080/9/ 162070/2019	977277	57,500,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uharibifu wa gari na ukokotaji gari nambari T218 CVF	DSM-Lumumba
2	075331/2019	020/088/9/ 157856/2019	977276	25,113,000	Ikiwa ni malipo ya madai baina ya Grace Sumailai V/S Taqwa bus Service kesi nambari 326 ya mwaka 2018.	DSM - Lumumba
3	067177/2019	050/088/9/ 132317/2017	997876	5,000,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kifo cha Abdoni Joviti Kalinjuna , kilichotokana na ajali ya gari nambari T181CEK	Mwanza
Jumla				**87,613,000**		

Ukaguzi unashauri Shirika la Bima la Zanzibar kufanya mapitio na maboresho ya sera zake ili ziweze kuendana na ushindani wa soko la Bima Tanzania.

3.4.4 Madai yatokanayo na wabia wengine wa Bima (Due to other reinsurance and treaty) shilingi 1,784,659,276

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia kumbukumbu za Shirika kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019 imebainika kuwepo kwa madai yatokanayo na wabia wengine wa shughuli za bima kama ifuatavyo:-

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 18: Madai yatokanayo na wabia wengine wa Bima

Namba	Wabia wa Shirika la Bima Zanzibar	Jumla yafedha (Shs)
1.	Due to other Facultative Reinsurers	533,631,579
2.	Due to JB Boarder	1,209,017,677
3.	Due to Afro-Asian Treat Reinsurance	42,010,020
Jumla		**1,784,659,276**

Taarifa za hesabu za Shirika kwa mwaka wa fedha unaioshia Disemba 2019 ziliripoti uwepo wa madai kama inavyonekana hapo juu, madai ambayo yameonekana kuwa na dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa taarifa za usuluhishi na uthibitisho wa uwepo wa usahihi wa salio la madai lililoripotiwa mwisho wa mwaka.
- Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha madai hayo ikiwemo Ankara (invoice), taarifa ya madai (debit notes), stakabadhi ili kuweza kuthibitisha uwepo wa usahihi wa salio la madai.
- Madai yanayotokana na mkataba wa Afro-Asian ni ya muda mrefu na ambayo yamekosa uthibitisho halali kwa zaidi ya kipindi cha miaka mitatu , ambayo yanatia shaka juu ya uwepo wake.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa Shirika la Bima uchukue jitihada za makusudi ili kuweza kutatua dosari zilizobainishwa na ukaguzi.

3.4.5 Madai ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) yaliyokosa uthibitisho shilingi 772,343,656

Kwa mujibu wa taarifa za fedha za Shirika la Bima, imebainika jumla ya shilingi 772,343,656 ikiwa ni madai yanayohusiana na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mwaka wa fedha unaoishia Disemba 2019, hata hivyo mchanganuo wa kina kuhusu madai ya kodi ya ongezeko la thamani yaliopaswa kulipwa kwa mwezi husika hayakuwasilishwa kwa ajili ya uthibitisho.

Ukaguzi umebaini kwamba gharama za kodi ya ongezeko la thamani na madai hayakuoonyeshwa katika taarifa za kila mwezi, badala yake yameorodheshwa kiujumla katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ambapo maelezo na muda wa madeni ya kodi ya ongezeko la thamani haukuonyeshwa.

Kwa mujibu wa mapitio ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT returns) kwa mwezi wa Disemba 2019 yaliyowasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalionyesha Shirika lilikuwa na deni la kodi ya ongezeko la thamani la shilingi 279,442,395 kwa matawi ya shirika la Bima Tanzania Bara na kupelekea tofauti ya kiwango kilichoonekana katika taarifa za hesabu za Shirika.

Mchanganuo wa deni la kodi ya ongezeko la thamani inaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 19: Madeni yatokanayo na Kodi ya Ongezeko la thamani

Namba	Jina la Tawi	Deni la VAT kwa mujibu wa Hesabu (Shs)	Deni la VAT kwa mujibu wa Marejesho ya TRA (Shs)	Tofauti iliyobainika (Shs)
1	Dar es Salaam	328,341,931	202,806,232	125,535,699
2	Mbeya	90,264,875	16,742,490	73,522,385
3	Arusha	128,547,106	19,447,260	109,099,846
4	Mwanza	102,480,286	22,235,191	80,245,095
5	Kijitonyama	2,796,853	1,964,663	832,190
6	Mtwara	8,856,849	6,950,825	1,906,024
7	Dodoma	58,197,171	9,295,733	48,901,143
	Jumla	**719,485,071**	**279,442,395**	**440,042,382**

Aidha, ukaguzi ulichunguza zaidi na kubaini tofauti ya madai ya kodi ya ongezeko la thamani isiyo ya kawaida yenye jumla ya shilingi 79,483,826 kwa tawi la Mbeya, shilingi 402,544 kwa tawi la Mtwara na shilingi 1,122,595 kwa tawi la Dodoma, ambapo maelezo ya kina pamoja na vielelezo vya kuthibitisha madai hayo havikuweza kupatikana kwa ukaguzi.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa shirika la Bima uhakikishe kwamba madeni na madai ya kodi ya ongezeko la thamani linaendana na marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT Returns) ili kuhakikisha kunakuwepo na usahihi wa taarifa hizo.

3.4.6 Malipo yasiyokua na tija kwa shirika la Bima shilingi 141,369,500

Jumla ya shilingi 141,369,500 zimeonyeshwa katika hesabu ya madeni ya Shirika la Bima. Ukaguzi ulipitia taarifa ya madeni na kubaini kuwa shirika kwa tarehe tofauti lilikataa madai yaliyowasilishwa na wadai ambayo yalilazimisha wadai kuwapeleka mahakamani, aidha ukaguzi ulibaini kuwa Mahakama iliamuru kwa upande wa wadai kulipwa fidia kwa sababu ya shirika la Bima kutohudhuria mahakamani wakati wote tarehe za kesi ziliposikilizwa.

Kwa upande wa wadai, madai yao ya awali yalikua na jumla ya shilingi 1,800,000. Kutokana na Shirika la Bima kushindwa kuhudhuria vikao vya Mahakama, Mahakama iliamuru jumla ya shilingi 50,181,500 zilipwe kwa wadai na kupelekea shirika kupata hasara kubwa kwa kulipa zaidi ya madai yaliyodaiwa hapo awali.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba kesi nambari 23/2016 iliyopelekea Mahakama kuamuru Shirika la Bima kufanya malipo ya shilingi 26,523,000 na shilingi 64,665,000 kwa hesabu ya Mahakama ya Iringa kupitia hesabu nambari 01J1040000100 CRDB. Ukaguzi haukuweza kupatiwa ufafanuzi wa uwepo wa deni hilo pamoja na vielelezo vilivyothibitisha Mahkama kuamuru malipo ya fedha hizo.

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi wa Shirika la Bima la Zanzibar kupitia kitengo cha sheria kinapaswa kutumia busara, hekima na tahadhari wakati wa kushughulikia madai ili kupunguza malipo ya ziada yanayoweza kujitokeza ambayo husababisha hasara kwa shirika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 20: Malipo yasiyokuwa na tija

Namba	Tarehe ya Uhaulishaji	Fedha zilizohaulishwa (Shs)	Fedha zilizodaiwa na Mlalamikaji (Shs)	Nambari ya Hesabu	Aliyelipwa
1	13/05/2019	50,181,500	1,800,000	01J1040000100 CRDB Moshi Branch	Nickson Mutabirwa
2	11/12/2019	26,523,000		-	Iringa Judicial Deposit Account
3	11/12/2019	64,665,000		-	Iringa Judicial Deposit Account
Jumla		**141,369,500**			

3.4.7 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 83,884,000

Kifungu cha 83A na Aya 4(c) ya jadweli la kwanza kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2014 kinataka makato ya kodi yazuio ya asilimia 5 kwa huduma zinazotolewa na asilimia 2 kwa manunuzi ya bidhaa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bima la Zanzibar limefanya malipo ya shilingi 83,884,000 kwa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya kazi za ushauri na huduma za kisheria walizotoa watoa huduma kwa shirika bila kukatwa kodi ya zuio.

Kukata kodi ya zuio kunapunguza gharama za ukusanyaji wa kodi; kunasaidia kuzingatia sheria na kupunguza kukwepa kodi; vile vile kunasaidia Serikali kukusanya kodi mapema, kitu ambacho hakikufanyika.

Kushindwa kuzuia kodi kwa huduma mbali mbali zinazotolewa kunaweza kupelekea kuisababishia shirika hasara zisizo za lazima zinazotokana na malipo ya adhabu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 21: Malipo ambayo hayakukatwa kodi

Namba	Tarehe	Nambari ya Hundi	Jumla ya Fedha (Shs)	Maelezo	Tawi lililofanya malipo
1	13/09/2019	936707	6,000,000	Ikiwa ni malipo ya Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuboresha tozo za Bima (Premium Rate Proposal)	Dar-es-Salaam
2	23/08/2019	977146	21,911,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya TANSCAR ATTORNEYS	Dar-es-Salaam
3	16/05/2019	936490	7,150,000	Ikiwa ni mlaipo kwa ajili ya TANSCAR ATTORNEYS	Dar-es-Salaam
4		977323	10,000,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Wakili Chanjarika & Company Advocates	Dar-es-Salaam
5		977334	8,275,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya usimamizi wa kesi nambari 169 ya mwaka 2017	Dar-es-Salaam
6		977299	14,300,000	Ikiwa ni malipo ya huduma za usimamizi wa kesi nambari 68 ya mwaka 2019 kwa Tanscar Attorneys	Dar-es-Salaam
7	20/02/2019	000009	4,680,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya Pango la Nyumba za wafanyakazi wa Shirikal la Bima	Kituo cha Mauzo, Kijitonyama
8	13/02/2019	001380	2,365,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari nambari Z 868 GZ	Makao Makuu, Zanzibar
9	03/04/2019	001429	3,903,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari nambari SLS 104 A.	Makao Makuu, Zanzibar
10	24/09/2019	001936	5,300,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari nambari Z 164 JV	Makao Makuu, Zanzibar
Jumla			**83,884,000**		

3.4.8 Uwepo wa tuhuma za madai ya bima kwa muda mrefu shilingi 104,300,000

Kwa mujibu wa taratibu za madai zilizowekwa na Shirika la Bima, uchunguzi wa tuhuma za madai zinapaswa kushughulikiwa na Idara ya Madai pamoja na Kitengo cha Sheria kwa kufanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha uthibitisho wa madai yanaweza kufanyiwa kazi kwa haraka kwa lengo la kupunguza nafasi ya wadai kuweza kulishtaki Shirika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa madai ya muda mrefu ikiwemo madai ya tuhuma, madai yaliyokosa uthibitisho wa kutosheleza ambayo yanahitaji uchunguzi zaidi ili kuepusha shirika kufanya malipo kinyume na utaratibu.

Mchanganuo wa madai hayo ambayo ukaguzi umekosa vielelezo na uthibitisho wa kutosheleza wa uwepo wa madai hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 22: Madai ya bima yaliyokosa uthibitisho

Namba	Nambari ya Madai	Jina la Mdai	Jumla ya fedha inayodaiwa (SHS)	Maelezo
1	010/070/9/168527/2019	Mr. Ramadhan Haji Juma	13,500,000	Ikiwa ni malipo ya madai ya tuhuma ya ajali wakati muda wa Bima umeshamaliza (expiry of the insurance policy)
2	010/070/9/165958/2019	Mr. Omar Juma Budda	5,800,000	Ikiwa ni malipo ya madai ya tuhuma ya ajali wakati ajali haikutokezea (Non occurrence of an accident)
3	010/070/9/165104/2019	Mr. Nassor Said Mohamed	85,000,000	Ikiwa ni malipo ya madai ya tuhuma ya ajali wakati ajali haikutokezea (Non occurrence of an accident)
Jumla			**104,300,000**	

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Bima kuhakikisha kuwa malipo ya wadai yanafanywa kwa wakati ili kuweza kuepusha shirika kupelekwa mahakamani, kusababisha hasara ya zaidi ya kinachodaiwa pamojana kufanya uchunguzi wa kina juu ya madai yanayojitokeza ili kuepusha uwepo wa viashiria vya ukiukwaji wa maadili ikiwemo kulipa madai yasiyostahili.

3.4.9 Kuchelewa kupelekwa fedha benki shilingi 186,637,556

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 186,637,556 kuwa ni mapato yanayokusanywa na madalali pamoja na mawakala wa matawi ya Dar-es-Salaam na Arusha kwa niaba ya Shirika la Bima hayakuwasilishwa benki kwa wakati. Kutokupeleka benki fedha za mapato zilizokusanywa kwa wakati ni kwenda kinyume na Kanuni za Mdhibiti wa Biashara za Bima Tanzania (TIRA).

Mchanganuo wa mapato hayo pamoja na majina ya mawakala na madalali waliokusanya fedha hizo kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 2.**

3.4.10 Uwepo wa mikopo ya muda mrefu na mapato ya ada ya bima (Premium) yaliyokuwa hayajakusanywa kutoka kwa Mawakala na Madalali shilingi 648,891,615.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa jumla ya shilingi 531,526,363 za mapato ya ada ya bima ambayo hayakukusanywa na Shirika la Bima kwa muda mrefu, pia imebainika uwepo wa jumla ya shilingi 117,365,252 ya mikopo ambayo haikukusanywa kutoka kwa mawakala.

Katika kupitia vitabu vya mawakala imebainika kwamba mikopo na mapato mengineyo hayakupatikana kwa wakati na kupelekea baadhi ya hesabu za mawakala kuonekana kuwa hazifanyi kazi kwa zaidi ya kipindi cha miaka mitatu.

Ukaguzi umeshindwa kuona jitihada zozote zilizochukuliwa na uongozi wa Shirika la Bima katika kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwa wakati. Uwepo wa madeni ya muda mrefu yanatia shaka juu ya uwepo wa mawakala, aidha kushindwa kupata malipo kutoka kwa mawakala kunaweza kusababisha hasara kwa hatua ambazo zitachukuliwa na uongozi wa Shirika la Bima katika kuyafuta madeni hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 72 (2) na 137(2) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Shirika la Bima Zanzibar. **Kiambatisho Nambari 3 kinahusika**.

3.4.11 Uwepo wa wadaiwa wa malipo ya bima Tawi la Arusha shilingi 55,721,830.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa wadaiwa wanaotokana na sera za bima (Insurance Policy) zinazouzwa kwa mkopo katika ofisi ya tawi la Arusha yenye jumla ya shilingi 55,721,830ambazo bado hazijalipwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2019. Kwa vile wadaiwa hao ni wengi, ukaguzi umeonesha baadhi ya wadaiwa hao kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 23: Wadaiwa wa malipo ya Bima

Namba	Tarehe	Jina la Mteja/ Mdaiwa	Jumla ya fedha (Shs)
1	24/12/2019	Daruni Delivers &Transport Ltd.	590,000
2	27/12/2019	Daruni Delivers &Transport Ltd.	590,000
3		Machame Safari Express Ltd.	8,070,500
4	1/7/2019	Mary Paul Mushi	1,020,110
5	24/7/2019	Sherali O. Mbowe	295,000
6	12/4/2019	Fausta Valeria/ Machame	1,517,775
7	9/8/2019	Gideon Alfred Mwakibinga	531,000
8	16/8/2019	Charles N. Swai	531,000
9	6/12/2019	Christina S. Lukumay	413,000
Jumla			**13,558,385**

3.4.12 Kukatiwa bima kwa chombo kilichokuwa katika hali isiyoridhisha

Kwa mujibu wa sera ya Shirika la Bima, ili chombo kiweze kuandikishwa kukatiwa bima inapaswa kuwa katika hali nzuri.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bima lilipokea maagizo ya kukatia bima MT. Mkombozi ambayo haipo katika hali ya kuridhisha kwa barua yenye kumbu kumbu namba MOICT/M.120/C.2/VOL VIII/115 ya tarehe 9/05/2019 kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Ukaguzi umebaini ya kwamba Shirika lililazimika kuikatia bima MT. Mkombozi wakijua ya kwamba MT. Mkombozi haina sifa ya kukatiwa bima kwa mujibu wa Sera ya Shirika la Bima na kwa kuzingatia chombo hicho kilipata ajali ya moto mnamo tarehe 10/10/2019 na hakuna vielelezo vilivyopatika na ukaguzi vinavyothibitisha ya kwamba chombo hicho kiliwahi kufanyiwa ukarabati, au kulipwa fidia kutokana na ajali hiyo ya moto na kwamba kipo katika hali ya kuridhisha kwa mujibu wa sera ya Shirika, hali ambayo imepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa kufanya maamuzi hayo jambo ambalo huenda likapelekea hasara kubwa kwa Shirika kwani ukizingatia Shirika halina uwezo wa kukikatia bima chombo hicho peke yake ililazimika kumtafuta mbia wakushirikiana nae katika kukikatia bima chombo hicho.

Kukikatia bima chombo ambacho hakina sifa kunaweza kupelekea Shirika la Bima kupoteza sifa yake ya kuwa ni Shirika la kibiashara badala yake huenda likawa Shirika la huduma jambo ambalo ni kinyume na sheria na kanuni za biashara za bima.

Ukaguzi unatoa ushauri ya kwamba Shirika linapaswa kujitahidi kuwa na mwelekeo zaidi wa biashara badala ya huduma kulingana na sheria na kanuni zinazosimamia biashara ya bima.

3.4.13 Dosari katika ukataji wa Bima kwa vyombo vikubwa

Kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba SMU/UU/3/7VOL.II/36 ya tarehe 27/01/2020 kutoka Shirika la Meli Zanzibar waliwataka shirika la Bima Zanzibar kuikatia bima meli ya MV. Mapinduzi II ambayo ilimaliza muda wakewa matumizi mnamo tarehe 14/02/2020. Kwa mujibu wa barua hiyo Shirika la Meli lilijikubalisha kulipa jumla ya dola za Kimarekeni (USD) 248,843.85 kwa vipindi vya awamu tatu tofauti kama inavyoonekana.

Jadweli Nambari 24: Dosari katika ukataji wa Bima za vyombo vikubwa

Namba	Awamu za malipo	Kiwango cha malipo (USD)	Tarehe ya Malipo
1	Malipo ya awamu ya kwanza	100,000	13/02/2020
2	Malipo ya awamu ya pili	100,000	13/04/2020
3	Malipo ya awamu ya tatu	48,844	13/06/2020
	Jumla	**248,844**	

Pamoja na barua za ukumbusho za kulitaka Shirika la Meli kufanya malipo ya Bima kwa meli yake, Shirika lilishindwa kufanya malipo hayo kwa mujibu wa Sera na badala yake ombi hilo la kuikatia bima MV Mapinduzi II lilikubaliwa na Shirika la Bima kupitia barua yenye kumbukumbu nambari ZIC / A.482 / MTU.II / 09/2020 ya tarehe 04/02/2020.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba Shirika la Bima liliamua kuikatia bima meli hiyo kabla ya malipo hayo kukamilika jambo ambalo ni kinyume na Sera, sheria na kanuni zinazosimamia biashara ya bima.

3.4.14 Bakaa ya Fedha katika hesabu ya FBME shilingi 90,830,291

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu vya Shirika la Bima la Zanzibar imebainika uwepo wa bakaa la fedha katika hesabu za benki ya FBME ambapo bakaa hiyo ipo kwa muda mrefu na hakuna jitihada zozote zilizobainishwa na Shirika hilo juu ya ufuatiliaji wa bakaa hiyo ili iweze kupatikana jambo ambalo huenda likapelekea fedha hiyo kukosekana na kulisababishia Shirika hasara kubwa. Mchanganuo wa bakaa hiyo ya fedha ambayo haijulikani hatima yake ni kama ifuatavyo;-

Jadweli Nambari 25: Bakaa ya Fedha katika hesabu ya FBME

Nambari ya hesabu	Kiwango cha fedha kilichopo (Shs)	Jina la tawi la Shirika
030653 TZS. FBME	6,149,799	Makao Makuu (Unguja)
FBME Account	2,797,613	Tawi la Mwanza
FBME Account	5,547,046	Tawi la Arusha
Account number 030653 TZS –TCA-002	47,824,787	Tawi la DSM
Account number 030653USD	28,511,053	Tawi la DSM
Jumla	**90,830,291**	

Kutokana na mchanganuo wa uwepo wa bakaa hiyo ya fedha inayodaiwa na Shirika la Bima ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bima kuzidi kufanya vikao vya mara kwa mara na Benki ya Tanzania ya kuwataka wakae pamoja kulitathmini uwepo wa bakaa hiyo kwenye hesabu zilizonakiliwa hapo juu ikiwa pamoja na kulifanyia malipo liweze kulipwa kwa wakati ili kuepusha matatizo ya baadae ambayo yanayoweza kujitokeza ikiwemo matatizo ya kiutendaji.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Bima Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 31 Disemba, 2019 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Bima Zanzibar limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba, 2019.

3.5 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Shirika la Bandari Zanzibar yameonekana kupungua kutoka shilingi 37,506,713,124 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 36,216,887,383.9 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 1,289,825,740.1 sawa na asilimia 3.4 . Vyanzo vya mapato hayo ni kama inavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 26: Mchanganuo wa mapato

Namba	Chanzo cha Mapato	Makadirio ya Mapato (Shs)	Mapato halisi (Shs)	Tofauti (Shs)	Asilimia
1	Mapato ya uendeshaji	29,183,146,425	27,100,747,874	(2,082,398,551.30)	(7.14)
2	Mapato ya Vyombo vya baharini	5,798,450,160	7,222,362,250	1,423,912,089.60	24.56
3	Mapato mengineyo	1,199,251,342	813,367,563	(385,883,779.40)	(32.18)
4	Riba ya kibenki	61,406,808	66,928,104	5,521,296.10	8.99
5	Ongezeko/ Upungufu wa ubadilishaji wa fedha za kigeni	-	(711,805,594)	-	
6	Ruzuku	-	1,658,359,083	-	-
	Jumla	**36,242,254,735**	**36,216,887,384**	**(1,038,848,945)**	

Kutokana na mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo juu, ukaguzi umebaini Shirika la Bandari limeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za uendeshaji kwa asilimia 7.14, aidha ukusanyaji wa mapato mengineyo imebainika kutokufikia kwa lengo la ukusanyaji wa mapato hayo kwa asilimia 32.18.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo husika kwa mujibu wa makadirio ikiwemo na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili Shirika kuweza kujiendesha kwa ufanisi na tija.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Shirika la Bandari Zanzibar yameonekana kupungua kutoka shilingi 31,129,110,374.66 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 29,801,710,959 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 1,327,399,415.66 sawa na asilimia 4.3.

Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama unavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 27: Mchanganuo wa matumizi

Aina ya matumizi	Makadirio ya matumizi (Shs.)	Matumizi halisi (Shs.)	Tofauti ya matumizi (Shs.)	Asilimia
Matumizi ya uendeshaji	12,595,217,507.40	10,256,086,544.72	2,339,130,962.68	18.57
Matumizi ya utawala	11,835,215,654.60	8,801,120,254.29	3,034,095,400.31	25.64
Matumizi mengineyo	11,582,049,068.00	10,032,698,567.12	1,549,350,500.88	13.38
Jumla	**36,012,482,230.00**	**29,089,905,366.12**	**6,922,576,863.87**	

Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika la Bandari Zanzibar (Operating Performance)

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Shirika la Bandari Zanzibar kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 na 2018/2019 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini kutokana na uchambuzi wa taarifa ya faida/hasara (Statement of Profit and Loss Account).

Jadweli Nambari 28: Taarifa ya faida na hasara

Maelezo	Namba ya marejeo	2019/2020 (Shs)	2018/2019 (Shs)
Total Port Income	1	34,323,110,123.27	33,313,879,874
Less. Cost of sales	2	(19,057,206,799)	(18,833,992,848.6)
Gross Profit		15,265,903,324.3	14,479,887,026
Other Income		947,223,698,567.1	1,136,032,569.36

Less. Other expenses		(10,032,698,567)	(12,295,117,526)
Proit before tax		6,180,428,527.9	3,320,802,069
Income Tax expenses		(1,854,128,558.4)	(996,240,620.82)
Profit for the year		4,326,299,969.5	2,324,561,448.58
Other Comprehensive Income			
Exchange differences on translating Foreign operation		(711,805,593.64)	1,398,441,597
Armotization of Grants	3	1,658,359,083.5	1,658,359,083.5
Total Comprehensive Income for the year		5,272,853,459.4	5,381,362,129.2

Uchambuzi wa jadweli linaloonekana hapo juu unaonesha ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Bandari na kubaini kuwa mapato yanayotokana na Shughuli za Bandari (Port Income) yameongezeka kutoka 33,313,879,874 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi shilingi 34,323,110,123.27 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 1,009,230,249.27 sawa na asilimia 3. Kwa ujumla mapato ya Shirika la Bandari kwa vyanzo vyote vya mapato yamepungua kutoka shilingi 37,506,713,123.20 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukilinganisha na shilingi 36,216,887,383.90 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji zimepungua kutoka shilingi 31,129,110,374.7 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ukilinganisha na shilingi 29,089,905,366 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo gharama zimepungua kwa shilingi 2,039,205,008.70 sawa na asilimia 6.5.

Katika tathmini iliyofanyika kwa vipindi vya miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo juu, Shirika la Bandari limeendelea kujiendesha kwa faida, ingawa faida hiyo imeonekana kupungua kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo Shirika la Bandari lilipata faida ya shilingi 5,272,853,459.4 ukilinganisha na faida iliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ya shilingi 5,381,362,129.2 kukiwa na tofauti ya pungufu ya faida ya shilingi 108,508,669.80.

Kutokana na tathmini iliyobainika hapo juu, ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato sambamba na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kufikia dhana na malengo ya uanzishwaji wa Shirika hilo.

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa mali za muda mfupi pamoja na madeni ya muda mfupi ya Shirika la Bandari kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 29: Ufanisi katika utendaji wa kifedha

	30.6.2020	30.6.2019
Jumla ya mali za muda mfupi (Shs.)	26,232,871,647.4	23,876,974,398.6
Jumla ya madeni ya muda mfupi (Shs.)	2,883,110,402	3,419,186,375.3
Tofauti ya mali na madeni ya muda mfupi (CA-CL) (Shs.)	23,349,761,245.40	20,457,788,023.30
UWIANO:		
Uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi (CA/CL)	9:1	6.9:1
Vigezo vya uwiano vinavyotakiwa	2:01	2:01

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi umeongezeka na kufikia uwiano wa 9:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020 ukilinganisha na uwiano wa 6.9:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2019, uwezo wa Shirika kumudu madeni ya muda mfupi ni mkubwa zaidi ya kiwango kinachohitajika uwiano ambao si mzuri sana kifedha, fedha hizi zingeweza kuwekezwa katika hesabu za amana za kibenki na Shirika kuweza kupata faida ya malipo ya riba.

Kwa mujibu wa vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu vya uwezo wa shirika kumudu dhima za mpito ni uwiano wa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa shirika kumudu madeni ya muda mfupi.

Ukaguzi unalishauri Shirika la Bandari kuwekeza fedha za ziada katika hesabu za amana ili ziweze kufaidika na gawio la riba.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.5.1 Madeni yasiyolipwa kwa muda mrefu shilingi 467,856,819.73

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu jumla ya shilingi 467,856,819.73 fedha ambazo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa, jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Shirika kujiendesha kiufanisi. Aidha kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa Shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.
Ukaguzi unashauri Shirika la Bandari Zanzibar, kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni.
Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 30: Madeni ya muda mrefu

Namba	WADAIWA	Madeni yaliyoripotiwa 2019/2020 (Shs.)	Madeni yaliyoripotiwa 2018/2019 (Shs.)
1	B.P Limited	37,608,470.35	37,608,470.35
2	Bachaa Trader Travelling	2,257,200.00	2,257,200.00
3	Bao Bao Beach	3,247,627.50	3,247,627.50
4	Global Marine Company	4,541,888.00	4,541,888.00
5	Group Five Buliding	11,850,000.00	11,850,000.00
6	H Young Pemba	2,344,462.00	2,344,462.00
7	Idara ya Mali Asili na Uvuvi	1,053,976.00	1,053,976.00
8	Idara ya Upigaji Chapa	6,118,572.74	6,118,572.74
9	Inten Group	17,000,000.00	17,000,000.00
10	Island Mash	14,800,000.00	14,800,000.00
11	Island Marine Services	4,795,367.66	4,795,367.66
12	Jack Enterprises	154,608,868.00	154,608,868.00
13	Kamal Marine	57,537,105.75	57,537,105.75
14	Katibu/Tume ya Mabadiliko ya Katiba	5,075,328.00	5,075,328.00
15	Mamlaka ya Mji Mkongwe	39,900,000.00	39,900,000.00
16	Mecco	6,970,035.00	6,970,035.00
17	Ministry of Communication	15,101,112.48	15,101,112.48
18	Ministry of Information & Heritage	1,770,189.00	1,770,189.00
19	Oryx Zanzibar	44,671,072.90	44,671,072.90
20	Pemba Rural Project	17,375,989.80	17,375,989.80
21	Puma Energy Tanzania Ltd	7,806,126.00	7,806,126.00
22	Sea Express Ltd	5,508,935.55	5,508,935.55
23	Shirika La Posta Tanzania	2,403,943.00	2,403,943.00
24	Zawiya Tanzania Traders	3,510,550.00	3,510,550.00
	Jumla	**467,856,819.73**	**467,856,819.73**

3.5.2 Kukosekana kwa uhalisia wa bajeti

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari katika uhalisia wa bajeti ya mapato yaliyokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Makadirio hayalingani na mapato halisi ya fedha yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa uhalisia wa makadirio ya bajeti na kupelekea uwepo wa tofauti kubwa iliiyobainika.

Ukaguzi ulifanya uchambuzi wa makadirio ya vyanzo vya mapato vya Shirika la Bandari na kubaini kuwepo kwa makadirio madogo ya makusanyo kulingana na uwezo wa Shirika katika kukusanya mapato hayo kwa kigezo cha mapato ya mwaka uliopita wa 2019, jambo ambalo limepelekea kwa baadhi ya vyanzo vya makadirio ya mapato kuwa madogo kwa zaidi ya asilimia mia moja.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Bandari kutengeneza bajeti zinazozingatia uhalisia na kuweka mbinu madhubuti na endelevu zitakazotuhakikishia kupanda kwa makusanyo ya mapato. Mchanganuo wa bajeti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 31: Taarifa ya bajeti

Vyanzo vya mapato	Makadirio ya mapato kwa 2019/2020 (Shs.)	Mapato halisi kwa 2018/2019 (Shs.)	Tofauti ya Mapato (Shs.)	Asilimia
Labour Charge	1,156,411,500.00	1,242,384,215.91	85,972,715.91	7.43
Lifting	420,285,750.00	506,397,557.23	86,111,807.23	20.49
Storage	427,042,000.00	448,459,870.00	21,417,870.00	5.02
Wharfage Dhow	390,951,875.00	408,974,524.91	18,022,649.91	4.61
Dockage	2,203,866,660.00	2,689,142,499.47	485,275,839.47	22.02
Port dues	353,910,000.00	375,173,506.17	21,263,506.17	6.01
Tug Services	947,181,600.00	1,076,719,764.17	129,538,164.17	13.68
Navigation Dues	1,968,219,000.00	2,794,250,112.67	826,031,112.67	41.97
Weighing Charges	80,000,000.00	111,581,363.00	31,581,363.00	39.48
Gate Pass	16,000,000.00	35,220,158.13	19,220,158.13	120.13
Hire of Equipment	56,071,000.00	124,824,937.60	68,753,937.60	122.62
House Rent - Income	33,840,000.00	33,930,720.00	90,720.00	0.27
Water Income	65,761,600.00	84,781,620.00	19,020,020.00	29.1

3.5.3 Kutokufuatwa kwa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu kwa kipengele cha sera ya uhasibu (IAS 8)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Bandari limefanya mabadiliko kadhaa katika Sera ya uhasibu kuhusu tathmini ya mali zake za kudumu. Katika mabadiliko hayo Shirika limebadilisha mfumo wa gharama na kwenda kwenye mfumo wa uhakiki kutokana na zoezi la uhakiki lililofanywa na Mthamini wa Mali za Kudumu. Kulingana na mahitaji ya viwango vya uhasibu, mabadiliko yoyote katika sera ya uhasibu yanapaswa kuhesabiwa kwa kuzingatiwa mwaka wa fedha uliopita.

Ukaguzi umebaini Shirika la Bandari limekiuka utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa viwango vya uhasibu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka (IAS 8).

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Bandari kufuata viwango vya kimataifa vya uhasibu ili taarifa za hesabu ziweze kuonesha sura halisi na sahihi.

3.5.4 Kutokufuatwa kwa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu kuhusu mahusiano ya pande mbili za mkataba (IAS 24)

Katika ukaguzi uliofanyika kumejitokeza dosari mbali mbali juu ya ujenzi na usimamizi wa mikataba ya ujenzi iliyofungwa baina ya Shirika la Bandari na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) dosari hizo zimebainika kuhusiana na mkataba wa ujenzi wa Uzio pamoja na Ghala la kuhifadhia bidhaa Saateni kukosa kuweka wazi taarifa ya mahusiano ya karibu ya pande mbili za mkataba, ujenzi uliogharimu jumla ya shilingi 746,249,910.

Dosari zilizobainika katika ukaguzi ni kwamba Uongozi wa juu wa Shirika la Bandari unatokana na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) na mkataba uliofungwa juu ya ujenzi huo kutoka kwa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM), kwa mujibu wa taratibu za mikataba kumekosekana utowaji wa taarifa ya mahusiano ya ukaribu baina ya pande mbili zilizoingia mkataba (Disclosure for the related party).

Aidha, kukosekana kwa utowaji wa taarifa ya mahusiano baina ya pande mbili kunapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uwepo wa Mgongano wa Kimaslahi baina ya pande mbili na kujitokeza kwa usimamizi usioridhisha wa utekelezaji wa mkataba ikiwemo uchelewaji wa utekelezaji wa mkataba wa ujenzi huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu (IAS 24). Mchanganuo wa malipo ya mikataba hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 32: Malipo ya mikataba

Namba	Aina ya Mkataba	Malipo (Shs)
1	Mkataba wa Ujenzi wa Uzio	71,300,000
2	Mkataba wa Ujenzi wa Ghala	674,949,910
Jumla		**746,249,910**

3.5.5 Mapungufu katika kuzingatia Utaratibu wa Ununuzi wa Umma katika ujenzi wa ghala Saateni shilingi 674,949,910

Ukaguzi umebaini Shirika la Bandari Zanzibar liliingia Mkataba na Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Ghala la kuhifadhia bidhaa Saateni kwa gharama za shilingi 674,949,910. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokufuatwa kwa taratibu za ushindani za kumtafuta mzabuni wa kazi hiyo, pamoja na dosari hiyo ukaguzi umebaiwni kutokufikiwa kwa viwango vya ujenzi wa ghala na kupelekea kutumika kwa gharama kubwa ukilinganisha na hali halisi ya ujenzi huo na kupelekea thamani halisi ya fedha (VFM) kushindwa kupatikana. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Nambari 11 ya mwaka 2016.

3.5.6 Thamani ya mali za kudumu ambazo hazikuoneshwa katika hesabu ya Mwisho wa mwaka za Shirika la Bandari

Kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinafafanua juu ya kuripoti mali za kudumu katika ufungaji wa hesabu ikiwemo majengo, ardhi na vyenginevyo. Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba Shirika la Bandari limeshindwa kuonyesha umiliki na thamani ya ardhi katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji na Utayarishaji wa Taarifa za Hesabu.

SHIRIKA LA BANDARI - PEMBA

3.5.7 Malipo kinyume na taratibu za utumishi 55,944,292.3

Jumla ya shilingi 55,944,292.3 zimelipwa kwa siku za mapumziko na muda baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi wa Shirika la Bandari – Pemba.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakuzingatia taratibu za utumishi wa umma juu ya uwepo wa barua ya kufanya kazi siku za mapumziko na muda baada ya saa za kazi kwenda kwa Mkurugenzi pamoja na uwepo wa fomu maalum ya malipo (overtime sheet) kwa wafanyakazi wa Shirika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 57 cha Sheria ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar nambari 2 ya mwaka 2011.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 33 : Malipo yaliyofanywa kinyume na utaratibu

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundni	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Melezo
1	40/8, 19/07/019	2007	9,978,320.20	Shirika la bandari tawi la pemba	Malipo ya overtime kwa wafanyakazi wa shirika Mkoani ,Wete na Wesha kwa mwezi wa Juni 2019
2	84/9, 21/08/019	2041	7,675,416.40	Shirika la Bandari	Malipo ya Overtime kwa wafanyakazi wa Shirika Wete, Mkoani, na Wesha kwa mwezi wa Julai 2019.
3	127/10, 20/09/019	2071	9,664,824.70	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za overtime kwa wafanyakazi wa shirika Wete, Mkoani na Wesha kwa mwezi wa Agosti, 2019
4	140/10, 22/10/019	2078	260,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za posho maalum kwa siku za ziada kwa wafanyakazi wali-oshiriki katika operation maboya
5	165/11, 21/10/019	2098	9,491,755	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za overtime kwa wafanyakazi wa Shirika Wete, Mkoani na Wesha kwa mwezi wa Septemba 2019
6	242/1, 16/1/020	2158	4,572,160.90	Shirika la bandari pemba	Malipo ya fedha za overtime kwa wafanyakazi wa shirika wete, Mkoani na Wesha kwa mwezi wa Disemba 2019
7	261/1, 13/1/020	2167	4,360,998.40	Shirika la bandari pemba	Malipo ya fedha za overitime kwa wafanyakazi wa shirika wete, Mkoani na Wesha kwa mwezi wa Novemba 2019
8	416/5, 11/05/020	2274	4,933,143	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za Overtime kwa wafanyakazi wa Shirika Wete, Mkoani, na Wesha kwa mwezi wa Aprili 2020
9	455/6, 16/06/020	2307	5,007,673.70	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za posho maalum kwa siku za ziada kwa wafanyakazi wa Mkoani, Wete na Wesha kwa mwezi wa Mei, 2020
Jumla			**55,944,292.30**		

3.5.7 Malipo yaliyokosa kukatwa kodi ya zuio shilingi 17,040,000

Jumla ya shilingi 17,040,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari – Pemba kwa wafanya biashara tofauti.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio za Mamlaka ya mapato Tanzania na Bodi ya mapato Zanzibar na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hiyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016 na Sheria ya Kodi ya Mapato. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 34: Malipo yaliyofanywa bila ya kodi

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	66/8 21/8/019	002028	2,480,000	Miradi ya JKU Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi katika ofisi ya shirika Kigomasha mnarani kwa mwezi wa Agosti 2019
2.	102/9 17/09/019	002051	2,400,000	MIRADI YA JKU – PEMBA	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za ulinzi katika Ofisi ya shirika Kigomasha Mnarani kwa mwezi wa Septemba 2019.
3.	142/10 18/10/019	002080	2,480,000	Miradi ya JKU –Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za ulinzi K/Masha Mnarani kwa mwezi wa Octoba, 2019
4.	181/11 20/11/019	002113	2,400,000	Miradi ya J.K.U Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi katika ofisi ya Shirika Kigomasha kwa mwezi wa Novemba 2019
5.	377/4 17/4/020	002245	2,400,000	Miradi ya J.K.U Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi katika ofisi ya Shirika Kigomasha kwa mwezi wa Aprili, 2019
6.	442/5 27/05/020	002295	2,480,000	Miradi ya JKU	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi katika ofisi ya shirika kigomasha mnarani kwa mwezi wa wa Mei 2020
7.	462/6 15/6/019	002308	2,400,000	Miradi ya JKU –Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za ulinzi K/Masha Mnarani kwa mwezi wa Juni, 2020
Jumla			**17,040,000**		

3.5.7 Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 55,356,201

Jumla ya shilingi 55,356,201 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Bandari – Pemba kwa wafanyabiashara tofauti. Ukaguzi umebaina kwamba wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manununzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. ili kuweza kufanya biashara na taasisi za serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 35: Malipo kwa watia huduma waliokuwa hawakusajiliwa

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Alielipwa	Maelezo
1.	44/8 9/8/2019	002011	663,480	Ali Hemed Ali	Malipo ya fedha kwa kazi ya kuondoa na kurudisha umeme pamoja na kazi ndogo ndogo
2.	76/9 23/08/2019	002033	230,375	Suleiman Zahor Suleiman	Malipo ya fedha za gharama za utengenezaji Gari SLS 161B ya Shirika la Bandari Pemba
3.	78/9 22/08/2019	002035	623,280	Mbarouk Salim Ali	Malipo ya fedha za ununuzi wa vifaa kwa ajili ya matengenezo ya ofisi ya Shirika
4.	85/9 23/08/2019	002040	709,555	Ali Hemed Ali	Malipo ya fedha kwa kazi ya kuweka uzio katika eneo la kisima na mahodhi pamoja na kazi nyengine ndogo ndogo Bandari Mkoani
5.	149/10 23/10/2019	002088	2,834,556.15	Mbarouk Salim Ali	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa milango ya mageti na vifaa kwa ajili ya matengenezo ya Beacon Bandarini Mkoani, Pemba.
6.	178/11 21/11/2019	002109	2,764,500	Ali Mohammed Khamis	Malipo ya fedha za mwisho kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika eneo la workshop ya Shirika

7.	470/6 17/06/2020	002316	2,948,800	Burhan Mohammed Burani	Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya utiaji rangi katika majengo ya kuhifadhia wagonjwa wa corona bandarini Mkoani, Wesha na Wete
8.	356/4	9/4/2020 002230	1,843,000	Ali Mohammed Khamis	Malipo ya fedha za mwanzo kwa ajili ya ujenzi wa banda la kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Wesha
9.	357/4 9/4/2020	002231	1,843,000	Suleiman Shaban Shamte	Malipo ya fedha za mwanzo kwa ajili ya ujenzi wa banda la kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Wete
10.	381/4 8/4/2020	002249	737,200	Miraji Ali Mohammed	Malipo ya fedha kwa ajili ya kufanya fitting za maji katika ofisi za bandari Mkoani, Wete na Bomani G. House
11.	387/4 24/4/2020	002255	4,315,211	Hamad Said Bakari	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuezekea banda la kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Mkoani
12.	389/4 17/4/2020	002257	7,516,600	Hamad Said Bakari	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuezekea banda la kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Wesa
13.	390/4 17/4/2020	002258	9,113,020	Hamad Said Bakari	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuezekea banda la kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Wete
14.	391/4 17/4/2020	002259	3,793,384	Mbarouk Salim Ali	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya fitting ya maji kwenye majengoya kuhifadhia wagonjwa wa Corona bandari ya Mkoani, Wesha, Wete na Bomani G. House

15.	15/5/2020 420/5	002278	1,796,925	Zahor Suleiman Said	Malipo ya fedha kwa kazi ya uendelezaji wa jengo la kuhifadhia wagonjwa wa corona bandari Mkoani kwa kuweka dari, fitting ya maji umeme, fiiting ya maji kuweka sakafu na kuchimba shimo la karo.
16.	24/4/2020 422/5	002280	1,843,000	Suleiman Shaaban Shaame	Malipo ya fedha za mwisho kwa kazi ya ujenzi wa kibanda cha kuhifadhia wagonjwa wa corona katika bandari ya wete.
17.	15/5/2020 423/5	002281	3,916,375	Ali Mohammed Khamis	Malipo ya fedha kwa kazi ya kuweka milango, fitting ya umeme, kuweka sakafu, kuchimba karo, kazi ya kuweka konaiz na kupaka rangi katika jengo la kuhifadhia wagonjwa wa corona bandari ya wesha
18.	15/15/2020 424/5	002285	1,290,100	Mussa Bakari Mjaka	Malipo ya fedha kwa kazi ya kupaka rangi katika jengo la kuhifadhia wagonjwa wa corona bandarini Mkoani.
19.	475/6 14/05/2020	002321	1,678,250	Mbarouk Salim Ali	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi jengo ya kuhifadhia wagonjwa wa corona bandarini Mkoani.
20.	476/6 14/05/2020	002322	4,895,590	Tahfif Alluminium & Glass workshop	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa milango na madirisha 7 ya alluminium kwa jengo ya kuhifadhia wagonjwa wa corona bandarini Mkoani.
Jumla			**55,356,201**		

3.5.8 Masurufu yasiokuwa na marejesho shilingi 25,220,260

Jumla ya shilingi 25,220,260 zimelipwa kwa mtumizi madogo madogo ya Shirika la Bandari-Pemba kupitia masurufu mbali mbali. Ukaguzi umebaini kwamba kutokuambatanishwa kwa baadhi ya marejesho ya masurufu katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo ya masurufu hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 36: Masurufu yasiyokuwa na marejesho.

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	47/8 14/8/2019	002012	2,000,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za masurufu kwa ununuzi wa vifaa na matengenezo ya gari pamoja na forklift ya Shirika
2.	59/8 30/8/2019	002021	2,500,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha kwa ajili ya kugharamia chakula
3.	112/9 20/9/2019	002062	1,996,260	Makame Juma Mohammed	Malipo ya fedha kwa dereva amabae alikodisha gari la crene kwa kubebea maboya ya Shirika kutoka Mkoani hadi Wesha na Mkoani hadi Wete.
4.	114/9 17/9/2019	002064	900,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za imprest kwa ajili ya kufanyia matengenezo ya Fork lift ya Shirika
5.	153/10 22/10/2019	002092	1,300,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za IMPREST kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuifanyia matengenezo gari SLS 161B
6.	154/10 22/10/2019	002092	1,324,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za IMPREST kwa ajili ya matumizi madogo madogo
7.	156/10 28/10/2019	002094	1,200,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula kilichotumika katika kikao
8.	189/11 29/11/2019	002121	7,000,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za Imprest kwa kazi ya uwekaji wa becon maeneo ya bandari za Pemba pamoja na usafi wa eneo la contena Mkoani
9.	243/1 22/1/2020	002159	4,000,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za imprest kwa matumizi ya ununuzi wa vipuri na matengenezo ya crane kongwe ya shirika

10.	354/4 6/4/2020	002229	1,000,000	Shirika la Bandari	Malipo ya fedha za Imprest kwa ajili ya matumizi madogo madogo
11.	361/4 7/4/2020	002235	2,000,000	Shirika la Bandari	Malipo ya edha za Imprest kwa ununuzi wa fusi, mchanga, mawe na vifaa vya ujenzi kwa ajili ya kujaza ghala na sehemu za vyoo
Jumla			**25,220,260**		

Maoni ya Ukaguzi

Hati Isiyoridhisha

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Bandari Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Bandari Zanzibar limepata hati isiyoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.6 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Taarifa za mapato

Mapato ya Shirika la Biashara la Taifa yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 10,021,596,610.44 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 56,795,231,494.32 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na ongezeko la mapato ya shilingi 46,773,634,883.88 sawa na asilimia 467.

Taarifa za matumizi

Matumizi ya Shirika la Biashara la Taifa yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 20,582,313,713.76 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 84,638,754,140.61 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na ongezeko la matumizi ya shilingi 64,056,440,426.85 sawa na asilimia 76.

Ufanisi katika Uendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa (Operating Performance)

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Shirika la Biashara la Taifa kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini kutokana na uchambuzi wa taarifa ya faida/hasara (Statement of Profit and Loss Account).

Jadweli Nambari 37: Taarifa ya faida/hasara

Maelezo	Mwaka wa Fedha		Tofauti (Shs)	Asilimia (%)
	2019/2020 (Shs)	2018/2019 (Shs)		
Mapato	56,795,231,494.32	10,021,596,610.44	46,773,634,883.88	466.73
Matumizi	84,638,754,140.61	20,582,313,713.76	64,056,440,426.85	311.22
Faida/ (Hasara)	**(27,843,522,646.29)**	**(10,560,717,103.32)**	**(17,282,805,542.97)**	**163.65**

Uchambuzi wa jadweli linaloonekana hapo juu linaonesha ukusanyaji wa mapato ya Shirika la Biashara la Taifa na kubaini mapato hayo yameongezeka na kufikia shilingi 56,795,231,494.32 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 10,021,596,610.44 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 46,773,634,883.88 sawa na asilimia 467.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 84,638,754,140.61 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 20,582,313,713.76 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 64,056,440,426.85 sawa na asilimia 76.

Katika tathmini iliyofanyika kwa vipindi vya miaka miwili, kwa mujibu wa taarifa za ufungaji wa hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi imebainika kwamba Shirika la Biashara la Taifa limeendelea kujiendesha kwa hasara, na hasara hiyo imeonekana kuongezeka kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo Shirika la Biashara la Taifa lilijiendesha kwa hasara ya shilingi 27,843,522,646.29 ukilinganisha na hasara iliyopatikana ya shilingi 10,560,717,103.32 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na tofauti ya hasara ya shilingi 17,282,805,542.97 sawa na asilimia 163.65.

Kutokana na tathmini iliyobainika hapo juu, ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kuchukua jitihada za makusudi kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato sambamba na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kufikia dhana na malengo ya uanzishwaji wa Shirika hilo.

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Shirika la Biashara la Taifa kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 38: Ufanisi katika utendaji wa kifedha

Mwaka wa Fedha	2019/2020 (Shs)	2018/2019 (Shs)
Mali za muda mfupi (Current Assets)	2,045,842,083.10	18,911,801,200.23
Madeni ya muda mfupi (Current Liabilities)	12,501,044,314.64	3,143,285,234.55
Mali za muda mfupi (Working Capital)		
Mali za muda mfupi – Madeni ya muda mfupi	(10,455,202,231.54)	15,768,515,965.68
Uwiano (Current ratio) =		
Mali za muda mfupi**/** Madeni ya muda mfupi	**0.16 :1**	**6:1**

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika utendaji wa kifedha wa Shirika umedhoofika na kufikia uwiano wa mtaji 0.16:1 na kutokufikia uwiano wa 2:1 kama unavyohitajika na vigezo (Benchmark) vya uwiano wa mtaji kiuhasibu.

Katika mchanganuo, ukaguzi umebaini uwiano wa mtaji umepungua na kufikia 0.16:1 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na uwiano wa mtaji wa 6:1 kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kutokana na tathmini hiyo ndani ya kipindi cha miaka miwili ya fedha inaonekana Shirika la Biashara la Taifa limedhoofika na halina uwezo wa kujiendesha kibiashara. Katika mchanganuo huo imebainika uwiano wa Shirika la Biashara la Taifa umedhoofika sana na kufikia 0.16:1 ambapo Shirika halina uwezo wa kulipa madeni ya muda mfupi. Kutokana na hali hiyo, inaonesha kuwa kwa kipindi hichi Shirika halina uwezo wa kulipa madeni ya muda mfupi.

Ukaguzi unashauri kwamba jitihada za makusudi zichukuliwe na Serikali kuhakikisha kwamba inalipatia ufumbuzi suala la uwepo wa madeni makubwa yanayolikabili Shirika la Biashara ili kuweza kutoa sura nzuri kwa Shirika hilo kuweza kufanya shughuli zake za kibiashara kiufanisi na hatimae kuleta tija kwa Serikali na kwa wananchi wa Zanzibar.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.6.1 Taarifa za wadaiwa na wadai wa Shirika

(a) Wadaiwa, shilingi 1,661,915,698.87

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambapo inaonekana jitihada hafifu zinachukuliwa na kupelekea deni hilo kupugua kwa kiwango kidogo jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa shirika kujiendesha kibiashara.

Aidha kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba deni linalodaiwa limepungua kwa kiwango kidogo kutoka shilingi 1,682,589,595.63 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 1,661,915,698.87 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 20,673,896.76 sawa na asilimia moja ya deni hilo.

Ukaguzi unashauri Shirika la Biashara la Taifa kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni kwa lengo la kupunguza idadi kubwa ya kiwango cha fedha kinachodaiwa na Shirika ambacho kinaathiri sura halisi ya mali za mpito za Shirika ukizingatia deni hilo ni la muda mrefu. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 39: Wadaiwa wa Shirika la Biashara

Namba	Wanaodaiwa na Shirika la Biashara	Jumla (Shs.)
1.	Rental Debtor-Rent Receivable Kitega Uchumi	426,920,461.54
2.	Provision for Trade Doubtful Debts	(263,084,994.91)
3.	Dar- es- Salaam Trade Receivable	38,460,475.37
4.	Staff Loan	792,707,060.48
5.	Collies Loan	90,046,496.30
6.	General Receivable	339,092,443.72
7.	Loan ZSTC - Dar- es- Salaam	347,593,866.68
8.	Loan Cloves For Farmers	21,312,584.40
9.	Vespa Loan	189,320,005.21
10.	ZSTC- Receivable Control	(320,452,699.92)
Jumla		**1,661,915,698.87**

(b) Wadai, shilingi 25,671,454,180

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika Shirika la Biashara la Taifa linadaiwa na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na watoa huduma mbali mbali wa shirika na kupelekea uwepo wa jumla ya shilingi 25,671,454,180 ambazo zimeripotiwa katika taarifa ya hesabu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 jambo ambalo ukaguzi haukuweza kuona jitihada zinazochukuliwa na Shirika la Biashara katika kuhakikisha deni hilo linalipwa na kupelekea taaswira nzuri ya kuweza kujiendesha kibiashara.

Aidha kutokuwepo kwa jitihada zinazochukuliwa kuhakikisha kunakuwepo na ulipwaji wa madeni kunaweza kupelekea kujitokeza kwa hasara kubwa kwa shirika kadri linavyochelewa kulipa deni hilo kwa kujitokeza kupata tozo ya adhabu na riba ya ucheleweshaji wa ulipaji wa deni hilo.

Mchanganuo wa madeni yanayodaiwa Shirika la Biashara la Taifa ni kama unavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 40: Wadai wa Shirika la Biashara la Taifa

Namba	Wadai	Jumla ya Fedha (Shs)
1	Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF)	5,000,000,000.00
2	Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ)	8,067,331,747.83
3	Wanunuzi wa Karafuu	10,550,155,699.42
4	Kampuni ya ZECON Construction	708,000,000
5	Salem Consctruction	1,120,966,733
6	Wizara ya Vijana	377,000,000,
7	Madeni ya Kiinua Mgongo kwa Wastaafu	225,000,000
Jumla		**25,671,454,180**

Ukaguzi unaishauri Serikali kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kulisaidia Shirika la Biashara kulipa madeni yake ili kuepuka Shirika kupoteza hadhi na uaminifu kwa watoa huduma pamoja na taasisi za Serikali wanaolidai Shirika na hatimae kupelekea Shirika la Biashara la Taifa kushindwa kukopesheka na kusababisha dhamira ya uanzishwaji wa Shirika hilo kukosekana.

3.6.2 Ucheleweshwaji wa fedha za mapato kupelekwa benki shilingi 140,565,900 na dola 20,783

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 140,565,900 na dola za Kimarekani (USD)20,783 zimekusanywa na Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) katika vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na bidhaa za maduka yanayofanya biashara ya uuzaji wa aina mbali mbali za bidhaa zinazozalishwa na Shirika hilo. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa fedha hizo kwa muda mrefu baina ya siku tatu hadi mwezi mmoja bila ya kupelekwa benki kwa wakati jambo ambalo linatoa sura isiyoridhisha ya utumiaji wa fedha hizo kwa malengo yaliyokuwa hayajakusudiwa.

Kutokupeleka fedha za mapato benki ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 41: Mapato ya mauzo yatokanayo na bidhaa zilizopo katika duka la maisara

Mwezi	Tarehe iliyokusanya fedha.	Tarehe zilizopelekwa bank	Idadi ya fedha (Shs.)	Idadi ya siku zilizokaa
Julai	1-12/7/2019	12/07/2019	1,936,500	11
	15-31/7/2019	31/07/2019	4,202,000	16
	15-31/7/2019	31/07/2019	586,200	16
	1-11/7/2019	12/07/2019	296,200	11
Agosti	1-20/8/2019	20/08/2019	139,500	19
	21-30/8/2019	30/08/2019	888,000	9
	1-20/8/2019	20/08/2019	1,971,200	19
21-30/8/2019		30/f08/2019	1,766,000	8
Septemba	02-10/09/2019	10/09/2019	1,689,500	8
	10-30/09/2019	30/09/2019	3,274,000	19
	02-10/09/2019	10/09/2019	672,000	8
	9-30/09/2019	30/09/2019	1,121,500	20
Oktoba	1-3/10/2019	04/10/2019	448,400	3
	4-10/10/2019	11/10/2019	163,000	6
	11-30/10/2019	31/10/2019	984,900	19
	4-10/10/2019	11/10/2019	2,287,000	6
	11-30/10/2019	31/10/2019	2,737,500	19
Novemba	1-28/11/2019	29/11/2019	1,496,300	28
	1-28/11/2019	29/11/2019	3,322,500	28
Disemba	02- 11/12/2019	13/12/2019	448,000	9
	12-30/12/2019	31/12/2019	477,500	18
	02- 11/12/2019	13/12/2019	1,316,500	9
	12-27/12/2019	31/12/2019	2,809,500	15
Januari	02-28/01/2020	31/01/2020	2,106,500	22
	02-28/01/2020	31/01/2020	2,372,500.00	26
Februari	07-25/02/2020	28/02/2020	319,400	18
	07-25/02/2020	28/02/2020	3,067,500	18
Machi	2-25/3/2020	31/03/2020	941,000	22
	2-11/03/2020	13/03/2020	2,420,000	9
	13-26/03/2020	31/03/2020	396,000	13
April	1-30/4/2020	30/04/2020	495,500	29
	1-30/4/2020	30/04/2020	3,996,000	29
Mei	3-7/5/2020	08/05/2020	122,500	5
	8-27/5/2020	29/05/2020	246,100	19
	3-7/5/2020	08/05/2020	2,549,500	5
	8-27/5/2020	29/05/2020	2,078,000	19
Juni	5-30/6/2020	30/6/2020	589,400	25
	5-30/6/2020	30/6/2020	2,616,500	25
Jumla ndogo			**59,350,100**	

Jadweli Nambari 42: Mapato ya mauzo yatokanayo na bidhaa zilizopo katika duka la Uwanja wa ndege (Airport)

Mwezi	Tarehe iliyokusanya fedha.	Tarehe zilizopelekwa Benki	Jumla ya fedha (USD)	Idadi ya siku zilizokaa
Julai	1-29/7/2019	31/7/2019	267	29
	1-29/7/2019	31/7/2019	759	29
	1-29/7/2019	31/7/2019	808	29
Agosti	1-29/08/2019	30/08/2019	497	29
	3-21/08/2019	30/08/2019	753	18
	1-29/08/2019	30/08/2019	1,067	28
Septemba	01/09/2019	30/09/2019	412	29
	01/09/2019	30/09/2019	766	29
	01/09/2019	30/09/2019	837	29
Oktoba	1-30/10/2019	31/10/2019	361	30
	1-29/10/2019	31/10/2019	949	30
	1-30/10/2019	31/10/2019	911	30
Novemba	1-28/11/2019	30/08/2019	370	28
	1-29/11/2019	30/08/2019	951	29
	1-28/11/2019	30/08/2019	874	29
Disemba	1-28/12/2019	31/12/2019	468	29
	1-29/12/2019	31/12/2019	1,332	30
	20-28/12/2019	31/12/2019	1,433	8
Januari	1-28/01/2020	31/01/2020	381	30
	1-30/01/2020	31/01/2020	816	30
	1-27/01/2020	31/01/2020	1,552	28
Februari	2-27/02/2020	28/02/2020	356	22
	1-27/02/2020	28/02/2020	772	27
	1-27/02/2020	28/02/2020	1,118	27
Machi	01-24/3/2020	26/03/2020	258	25
	01-23/3/2020	26/03/2020	764	25
	01-22/3/2020	26/03/2020	920	25
Aprili	01/04/2020	08/04/2020	7	4
	01/01/2020	03/04/2020	24	3
Jumla Ndogo (USD)			**20,783**	

Jadweli Nambari 43: Mapato ya mauzo yatokanayo na bidhaa zilizopo katika duka la Malindi

Mwezi	Tarehe iliyokusanya fedha.	Tarehe zilizopelekwa bank	Idadi ya fedha (Shs.)	Idadi ya siku zilizokaa
Julai	1-15/7/2019	16/07/2019	439,500	15
	16-23/7/2019	23/07/2019	38,000	7
	24-31/7/2019	31/07/2019	423,250	7
	1-15/7/2019	16/07/2019	3,651,500	15
	16-23/7/2019	23/07/2019	991,500	7
	24-31/7/2019	31/07/2019	3316500	7
Agosti	1-8/8/2019	09/08/2019	98,000	7
	10-19/8/2019	19/08/2019	164,000	9
	20-31/8/2019	31/08/2019	93,500	11
	1-8/8/2019	09/08/2019	2,214,500	7
	10-19/8/2019	19/08/2019	1,992,500	9
	20-31/8/2019	31/08/2019	1,810,500	11
Septemba	1-17/9/2019	18/09/2019	202,900	17
	18-30/9/2019	01/10/2019	245,500	13
	1-17/9/2019	18/09/2019	3,915,000	17
Oktoba	1-11/10/2019	12/10/2019	366,200	11
	12-31/10/2019	02/11/2019	296,400	19
	1-11/10/2019	12/10/2019	2,228,500	11
	12-23/10/2019	24/10/2019	2,420,500	11
	24-31/10/2019	02/11/2019	1,719,500	7
Novemba	1-30/11/2019	02/11/2019	372,000	30
	1-30/11/2019	02/11/2019	4,118,500	30
Disemba	1-13/12/2019	14/12/2019	296,500	13
	14-24/12/2019	25/12/2019	917,000	11
	25-31/12/2019	04/01/2020	9,500	10
	1-13/12/2019	14/12/2019	4,193,500	13
	13-24/12/2019	25/12/2019	3,241,000	12
	24-31/12/2019	04/01/2020	528,500	11
Januari	1-31/1/2020	01/02/2020	176,000	31
	1-24/1/2020	25/01/2020	3,362,000	24
	25-31/1/2020	01/02/2020	556,000	7
Februari	1-29/2/2020	02/03/2020	233,250	30
	1-14/2/2020	15/02/2020	3,090,000	15
	15-29/2/2020	02/03/2020	2,943,000	19

Machi	1-10/3/2020	11/03/2020	124,500	10
	11-31/3/2020	01/04/2020	58,000	20
	1-10/3/2020	11/03/2020	2,729,000	11
	11-31/3/2020	01/04/2020	1,498,000	20
Aprili	4-30/4/2020	01/05/2020	154,500	26
	4-30/4/2020	01/05/2020	4,845,500	26
Mei	1-12/5/2020	13/05/2020	391,300	12
	13-20/5/2020	21/05/2020	215,000	7
	21-30/5/2020	31/05/2020	37,000	9
	1-6/5/2020	07/05/2020	5,488,000	6
	7-12/5/2020	13/05/2020	3,342,000	5
	13-19/5/2020	20/05/2020	1,971,500	6
	20-30/5/2020	31/05/2020	992,000	10
Juni	1-23/6/2020	24/06/2020	214,500	23
	24-30/6/2020	01/07/2020	107,500	6
	1-23/6/2020	24/06/2020	4,312,500	23
	24-30/6/2020	01/07/2020	1,996,500	6
Jumla ndogo			**79,141,800**	

Jadweli Nambari 44: Mapato ya mauzo yatokanayo na bidhaa zilizopo katika duka la Malindi

Mwezi	Tarehe ya makusanyo	Tarehe ya kuwasilishwa benk	Kiasi Kilichokusanywa (Shs.)	Idadi ya siku alikaanazo fedha
Julai	1-29/7/2019	31/7/2019	228,500	30
Agosti	5-29/08/2019	31/08/2019	119,500	24
Septemba	02-30/09/2019	30/09/2019	153,500	28
Oktoba	1-31/10/2019	31/10/2019	126,000	30
Novemba	1-26/11/2019	29/08/2019	224,500	27
Disemba	06-30/12/2019	31/12/2019	133,000	24
Januari	2-30/01/2020	31/01/2020	170,000	28
Februari	3-27/02/2020	28/02/2020	170,500	24
Machi	02-30/3/2020	31/03/2020	171,000	28
Aprili	02-29/04/2020	30/04/2020	141,500	27
Mei	06-28/05/2020	29/05/2020	126,500	22
Juni	02-24/06/2020	25/06/2020	309,500	22
Jumla			**2,074,000**	

3.6.3 Fedha zilizokopwa na Shirika kutoka kwa watu binafsi shilingi 6,771,848,000

Ukaguzi wa hesabu za mwisho wa mwaka 2019/2020 umebaini kwamba Shirika limepokea fedha jumla ya shilingi 6,771,848,000 kutoka kwa wafanya biashara wa nchi tofauti kwa lengo la kununua karafuu. Ukaguzi umebaini fedha hizo hazikutumiwa kwa shughuli iliyokusudiwa, na wala wafanya biashara hao hawajapatiwa bidhaa inayolingana na uhalisia wa kima cha fedha kilichozuiliwa na Shirika la Biashara.

Orodha ya baadhi wanunuzi wanaoodai karafuu kwa Shirika, ambao tayari wameshalipa malipo kamili ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 45: Fedha zilizokopwa na Shirika

Namba	Mnunuzi	Nchi anayotoka	Idadi ya tani za karafuu anazodai	Bei ya kununulia kwa tani (USD)	Jumla ya fedha (USD)	Jumla ya fedha (Shs.)
1.	Unique Traders	India	132	5,200	686,400	1,592,448,000
2.	Rashwell	Dubai	75	4,750	352,500	817,800,000
3.	Afcom Traders	Dubai	200	4,700	940,000	2,180,800,000
4.	Atban	Tanzania	200	4,700	940,000	2,180,800,000
Jumla			**607**	**19,350**	**2,918,900**	**6,771,848,000**

Kutokana na mchanganuo unaonekana katika jadweli hapo juu wa uwepo wa deni la fedha linalotokana na wanunuzi wa karafuu, ukaguzi haukuweza kuthibitisha uhalali wa deni hilo kwa kukosekana kupatiwa vielelezo na nyaraka zinazothibitisha makabidhiano ya fedha hizo kwa ajili ya ununuzi wa karafuu kwa wafanyabiashara hao jambo ambalo limetia shaka juu ya uwepo wa taarifa hiyo.

Ukaguzi unashauri Shirika liwe na mikataba midogo midogo kwa wanunuzi wa karafuu ,na fedha inayokabidhiwa kwa Shirika itumike kwa lengo la kuwapatia huduma wafanya biashara ili kuweza kuondoa mizozo inayoweza kujitokeza.

3.6.4 Ulipaji wa Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda bila kupewa Mikataba

Ukaguzi umebaini Shirika la Biashara ZSTC kuwa na wafanyakazi wengi ambao wanafanyakazi kwa mikataba ya muda mrefu kinyume na taratibu za utumishi Serikalini. Kwa mujibu wa kanuni za Utumishi chini ya kifungu cha 37(4) cha sheria namba 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma, kifungu kidogo 135(1)(2) Taasisi ya Serikali hairuhusiwi kuwatumikisha watumishi wa muda (daily pay) kwa kipindi kirefu, ikiwa kutakuwa na ulazima wa kuwatumia basi Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuomba kibali cha ajira kwa wafanyakazi hao.

Hata hivyo imebainika Shirika limekuwa likiwatumia watumishi wa muda (daily pay) na kuwalipa kila mwezi bila ya kujazishwa mikataba ya ajira, aidha kukosekana kwa taarifa za idhini kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi zinazoruhusu uwepo wa waajiriwa wa mikataba kunaweza kupelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa uwajiri huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni za utumishi wa umma chini ya sheria namba 2 ya mwaka 2011.

Jadweli Nambari 46 : Orodha ya wafanyakazi wa muda ZSTC - Unguja

Namba	Jina	Umri	Elimu	Kitengo cha kazi
1	Asma Saleh Said	24	Form II	Saateni Eneo Tengefu
2	Arafa Suleiman Mwinyi	40	Form II	Saateni Eneo Tengefu
3	Bahati Said Nassor	40	Form II	Saateni Eneo Tengefu
4	Fatma Ali Hamad	37	Form II	Saateni Eneo Tengefu
5	Hussein Haji Ali	27	Form II	Saateni Eneo Tengefu
6	Leyla Omar Abdalla	39	Form II	Saateni Eneo Tengefu
7	Maryam Maulid Mussa	33	Form II	Saateni Eneo Tengefu
8	Mwajuma Khatib Juma	45	Form II	Saateni Eneo Tengefu
9	Zena Hussein Khamis	32	Form II	Saateni Eneo Tengefu
10	Zuwena Khamis Ussi	38	Form II	Saateni Eneo Tengefu
11	Rehema Juma Ramadhan	37	Form II	Saateni Eneo Tengefu
12	Bimkubwa Maisara Mahkoum	39	Form II	Saateni Eneo Tengefu
13	Mtumwa Mussa Zubeir	47	Form II	Gulioni ZSTC Jengo la Kitega Uchumi
14	Khadija Khamis Mohammed	41	Form II	Saateni Eneo Tengefu
15	Asma Jumbe Khamis	43	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
16	Mwanaisha Haji Sengeru	38	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
17	Maimuna Muhidin Mahmoud	27	Form IV	Gulioni ZSTC Jengo la Kitega Uchumi

18	Ajra Abdalla Ali	39	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
19	Nasra Ussi Mohammed	28	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
20	Suwad Mohammed Khamis	30	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
21	Aziza Said Mohammed	29	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
22	Dawa Makame Juma	29	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
23	Sada Issa Ismael	39	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
24	Salama Othman Khamis	37	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
25	Amina Ali Abdalla	41	Form IV	Saateni Eneo Tengefu
26	Asmahan Abdulkareem Suleiman	30	Cheti (Journalism)	Saateni Eneo Tengefu
27	Fatma Bakar Silima	40	Cheti (Insurance)	Gulioni ZSTC Jengo la Kitega Uchumi
28	Fatma Manzi Yussuf	41	Cheti (Record Mgt)	Gulioni ZSTC Jengo la Kitega Uchumi
29	Hadia Mohammed Ali	35	Cheti (Air Fair, & Food Prod.)	Saateni Eneo Tengefu
30	Nasra Mohammed Masoud	40	Cheti (Record Mgt)	Uwanja wa Ndege
31	Tabitha James Mbapula	33	DIPLOMA (Record Mgt)	Saateni Eneo Tengefu
32	Sneyuu Ali Hassan	29	DIPLOMA (Int. Relations)	Gulioni ZSTC Jengo la Kitega Uchumi
33	Ramla Subira Ali	37	DIPLOMA (Islamic Banking)	Saateni Eneo Tengefu

Jadweli Nambari 47: Orodha ya wafanyakazi wa muda ZSTC-Pemba

Namba	Jina	Umri	Elimu	Sehemu ya Kazi
1	Fatma Haji Habib	32	Form II	Kiwanda cha Makonyo
2	Muhamadi Ali Muhamadi	26	Form II	Mkoani
3	Mbarouk Shaaban Mbarouk	31	Form II	Chake Chake
4	Rashid Ali Ayoub	44	Form II	Shamba la Mtakata
5	Suleiman Ali Bakar	41	Form II	Shamba la Mtakata
6	Omar Said Bakar	31	Form II	Shamba la Mtakata
7	Omar Ali Omar	30	Form II	Shamba la Mtakata
8	Omar Khamis Ali	39	Form II	Shamba la Mtakata
9	Bimkubwa Ramadhan Nassor	46	Form II	Shamba la Mtakata

10	Khadija Ali Othman	45	Form II	Shamba la Mtakata
11	Aisha Juma Khamis	33	Form II	MAABARA
12	Tatu Ali Khamis	46	Form II	Shamba la Mtakata
13	Mgeni Mwalim Abdalla	36	Form II	Shamba la Mtakata
14	Mbaraka Juma Samwel	36	Form II	Shamba la Mtakata
15	Halima Juma Khamis	34	Form II	Shamba la Mtakata
16	Maryam Juma Hajji	41	Form II	Shamba la Mtakata
17	Sada Ali Maalim	39	Form II	Shamba la Mtakata
18	Iddi Abdalla Juma	40	Form II	Shamba la Mtakata
19	Fatma Ali Saleh	30	Form III	Chake Chake
20	Mariam Salim Suleiman	26	Form III	Mkoani
21	Salum Juma hamad	31	Form VI	Kiwanda cha Makonyo
22	Raya Khatib Faki	34	Form IV	Wete
23	Moh'd Ali Ussi	36	Form IV	Kiwanda cha Makonyo
24	Omar Khamis Said	27	Form VI	Kiwanda cha Makonyo
25	Juma Kassim Juma	27	Form VI	Kiwanda cha Makonyo
26	Wahida Abdalla Ali	24	Form IV	Kiwanda cha Makonyo
27	Rashid Juma Suleiman	29	Form IV	Kiwanda cha Makonyo
28	Yussuf Salim Ussi	30	Cheti (Welding & Fabrication)	Kiwanda cha Makonyo
29	Azra Abdulla Moh'd	28	Diploma (Record Mgt.)	Kiwanda cha Makonyo
30	Ummul-ayman Moh'd Ali	23	Diploma (Proc.& Supply)	Wete
31	Ali Khelef Abdalla	26	Diploma (Proc. & Supply)	Kiwanda cha Makonyo
32	Abdalla Suleiman Haji	53	FII	Kiwanda cha Makonyo
33	Siti Juma Abdalla	55	STD7	Kiwanda cha Makonyo
34	Issa Juma Khamis	56	FII	Shamba la Mtakata
35	Mwalim Yussuf Khamis	50	FII	Shamba la Mtakata
36	Moh'd Said Yussuf	54	FII	Shamba la Mtakata
37	Fatma Salim Khamis	54	FII	Shamba la Mtakata
38	Halima Juma Khamis	58	FII	Shamba la Mtakata
39	Mohd Amour Mohd	55	FII	
40	Tatu Ali Khamis	51	FII	Shamba la Mtakata
41	Bimkubwa S. Khamis	55	FII	Shamba la Mtakata
42	Mafunda Abdalla Omar	55	FII	Shamba la Mtakata
43	Asha Iddi Ali	55	FII	Shamba la Mtakata

3.6.5 Tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo

Katika kuhakikisha kwamba Shirika la Biashara linajiimarisha kibiashara pamoja na kuongeza mchango wake kwenye mapato ya Serikali limepanga kutekeleza miradi ifuatayo:-

- Ujenzi wa ofisi na kitega uchumi Malindi.
- Ujenzi wa maghala ya kununulia na kuhifadhia karafuu pamoja na kitega uchumi (Madungu) Pemba.
- Ujenzi wa Nyumba za kulala wageni Kiwanda cha Makonyo.
- Ujenzi wa kituo cha kisasa cha Organic Farming Processing – Saateni
- Ujenzi wa maduka katika maeneno ya Saateni Unguja na Kiwanda cha Makonyo – Pemba.
- Upandaji wa Mikaratusi katika maeneo ya Mamoja na Kishindeni kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi wa mafuta ya mimea.

Katika kupitia miradi hiyo na kujiridhisha hatua iliyofikiwa, ukaguzi umebaini baadhi ya miradi bado haijatekelezwa na baadhi ya miradi imeendelea kusimama na kuchelewa kutekelezwa kutokana na ukosefu wa upatikanaji wa fedha.

Hali halisi ya utekelezaji wa baadhi ya miradi iliyoweza kutekelezeka na dosari zilizobainika na wakaguzi ni kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi wa Ofisi na Kitega Uchumi Malindi

Shirika la Biashara la Taifa limeingia mkataba wa ukarabati wa jengo la zamani la Shirika hilo pamoja na ujenzi wa nyumba mbili zilizopo Malindi kupitia mkataba wenye kumbu kumbu namba ZSTC/W/CRMH/01/2016/2017 wa tarehe 10/6/2016 na kampuni ya ZECCOM kwa thamani ya shilingi 2,888,885,522.60.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 1,991,807,131.97 sawa na asilimia 69 zimeshalipwa kwa Mkandarasi huyo, ambapo ujenzi huo umeshakamilika na kukabidhiwa kwa Shirika la Biashara la Taifa ingawa kukiwa na deni la Shilingi 897,078,390.63 sawa na asilimia 31 ambazo hadi ukaguzi unakamilika fedha hizo bado hazijalipwa.

Dosari zilizobainika katika ujenzi huo ni kama zifuatazo:-

- Shirika la Biashara la Taifa kushindwa kulipa jumla ya shilingi 897,078,390.63 sawa na asilimia 31 kwa kandarasi huyo kwa wakati jambo ambalo huenda likapelekea kujitokeza uwepo wa deni kubwa ambalo litapelekea kuathiri mipango ya Shirika baadae.
- Ukaguzi haukupatiwa makubaliano yaliyofikiwa baina ya Shirika na Mkandarasi huyo juu ya uwepo wa deni hilo na namna au njia itakayotumika, na muda utakaotumika kuweza kulipa deni hilo.
- Kukosekana kwa ripoti ya awali ya utanuzi wa jengo hilo na namna ambavyo litakavyokuwa baada ya kukarabatiwa.

- Kukosekana kwa gharama halisi za fedha kwa mujibu wa makisio ya muhandisi katika ukarabati.
- Kufunga mkataba mmoja wenye aina mbili za kazi (ukarabati wa ujenzi na Ujenzi mpya) kwa mkandarasi mmoja jambo ambalo ingeliwezekana kuwepo kwa mikataba miwili tofauti na kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na mikato ya kodi kwa mkandarasi huyo.

(b) Ujenzi wa maghala ya kununulia na kuhifadhia karafuu pamoja na Kitega Uchumi (Madungu) Pemba

Shirika la Biashara la Taifa limeingia mkataba wa ujenzi wa jengo la kitega uchumi na kampuni SELECOM CONSTRUCTION LIMITED kwa thamani ya shilingi 6,923,355,649.

Kwa kupitia mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/FO121/W/ICB/2018/2019/01 wa tarehe 12/12/2019. Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 557,388,802.25 sawa na asilimia 8 zimeshalipwa kwa Mkandarasi huyo, kwa mujibu wa mkataba huo ujenzi huo ulikadiriwa kumalizika baada ya kipindi cha miaka mitatu tangu kusainiwa kwa mkataba huo.

Ukaguzi umebaini ujenzi huo bado haujafikia katika hali ya kuridhisha na umekwama kuendelea kutokana na kukosekana kwa jumla ya shilingi 6,365,966,846.75 sawa na asilimia 92 za kumalizia ujenzi huo.

Dosari zilizobainika katika ujenzi huo ni kama zifuatazo:-

- Shirika la Biashara la Taifa kushindwa kuendeleza ujenzi huo na kupelekea ujenzi kusimama kukiwa na upungufu wa fedha anazodai mkandarasi katika kumalizia ujenzi huo sawa na jumla ya shilingi 6,365,966,846.75 sawa na asilimia 92 za kumalizia ujenzi huo, jambo ambalo linaweza kupelekea gharama ya ujenzi huo kuongezeka mara dufu kila unapo endelea kuchelewa kukamilika kwake kutokana na tataizo la kupanda kwa gharama za ujenzi siku hadi siku.
- Ukaguzi umebaini Shirika la Biashara la Taifa limeingia makubaliano na mshauri elekezi (OGM Consultancy) kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi huo kwa thamani ya shilingi 322,944,679.95. Hadi ukaguzi unakamilika jumla ya shilingi 26,820,829.36 zimelipwa sawa na asilimia 8 ya malipo yote na kubakisha malipo ya shilingi 296,123,850.6 sawa na asilimia 92 ya malipo yote.

Dosari kubwa iliyobainika na ukaguzi katika miradi hii ni kuchelewa kukamilika kwa miradi iliyopangwa kwa muda na mengine kushindwa kufanyika, jambo ambalo linapelekea kuzikosesha jamii kupata huduma zinazotarajiwa na kupelekea uwezekano wa kujitokeza kutumika gharama kubwa ya umaliziaji wa miradi hiyo kutokana na kuongezeka kwa bei ya vifaa vya ujenzi.

Aidha kunaweza kupelekea Serikali kujibebesha mzigo mzito wa gharama za ujenzi kwa vile Mkataba huo utakuwa umemaliza muda na kupelekea Shirika kufunga mkataba mwengine ambao unaweza ukawa na gharama kubwa zaidi.

(c) Upandaji wa mikaratusi katika maeneo ya Mamaoja na Kishindeni kwa ajili ya upatikanaji wa malighafi ya mafuta ya mimea.

Katika kupitia mradi huu ili kuweza kujiridhisha juu ya hatua iliyofikiwa, ukaguzi umebaini Shirika la Biashara la taifa tayari imeshaanza hatua ya awali ya uwoteshaji wa miche na ipo katika hali ya nzuri na yakuridhisha.

Shirika limeshindwa kutekeleza baadhi ya miradi iliyotajwa hapo juu kutokana na ukosefu wa fedha unaolikabili Shirika, ukaguzi unashauri Shirika kubuni Miradi michache ambayo wataweza kuyatekeleza kwa wakati na kuleta ufanisi na tija kwa jamii.

Ukaguzi unaishauri Serikali kutafuta njia za kulisaidia Shirika kutekeleza miradi hiyo ikiwemo na ulipaji wa madeni unaolikabili Shirika la Biashara la Taifa kwani utekelezaji wa miradi hiyo utakapokamilika utaweza kuliingizia Shirika fedha nyingi na hivyo kuondosha utegemezi wa uuzaji wa zao la karafuu katika kuendesha shughuli zake.

3.6.6 Kutokuingizwa kwa taarifa za madeni katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 7,794,086,747.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa madeni mbali mbali yenye jumla ya shilingi 7,794,086,747.56 ambayo hayakuripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka na kupelekea hesabu hizo kutokuonesha uhalisia na usahihi wa hesabu hizo. Dosari hizo ni kama zifuatavyo:-

- Uwepo wa deni la shilingi 43,802,000 ambazo zimetumika kuwakopesha wafanyakazi mbali mbali wa Shirika ambao wamebainika kuwepo kwa dosari za upandishiaji wa mikopo mipya kabla ya mkopo wa mwanzo kulipwa na kumalizika, ambapo imepelekea kukosekana kwa taarifa za mikopo hiyo katika daftari lawadaiwa katika mfumo wa taarifa za fedha.
- Uwepo wa madeni kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi mbali mbali, washauri elekezi pamoja na tozo za kodi zenye juma ya shilingi 7,750,284,747.56 fedha hizo hazikuripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha.

Mchanganuo wa mikopo ya wafanyakazi wa ndani ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 48: Mikopo ya wafanyakazi wa ndani

Namba	Jina la Mfanyakazi	Jumla ya fedha (Shs.)	Tarehe ya Mkopo
1	Mwinyi Zubeir Marzouk	7,000,000	Disemba,2019
2	Abass Khalfan Masoud	7,000,000	Disemba,2019
3	Machano Kombo Haji	7,000,000	Disemba,2019
4	Ali Yussuf Mwinyi	4,000,000	Januari,2020
5	Said Muhiddin Khamis	6,802,000	Januari,2020
6	Fatma Hamad Mbarouk	5,000,000	Januari,2020
7	Idrisa Omar Ali	7,000,000	Februari,2020
Jumla		**43,802,000**	

Mchanganuo wa madeni yanayodaiwa na wakandarasi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 49: Madeni ya wakandarasi

Namba	Aina ya Kazi	Kampuni	Thamani ya Mkataba (Shs)	Fedha iliyolipwa (Shs)	Fedha iliyobakia (Shs)
1	Ujenzi wa Afisi Malindi	ZECCON	2,888,995,522.60	1,991,807,131.97	897,078,390.63
2	Matengenezo Jengo la Kitega Uchumi	Grasshopper	255,904,625.50	199,735,728.57	56,168,896.93
3	Ujenzi Jengo la Madungu-Pemba	Salem Consultancy	6,923,355,649	557,388,802.25	6,365,966,846.75
4	Mshauri Elekezi Jengo la Madungu-Pemba	OGM. Consultancy	322,944,679.95	26,820,829.36	296,123,850.60
5	Kodi(VAT) kwa Ajili ya Ujenzi Madungu-Pemba	ZRB	-	-	105,610,509.90
6	Zuwio la Kodi Ujenzi Madungu-Pemba	TRA	-	-	29,336,252.75
Jumla			**10,391,200,477.05**	**2,775,752,492.15**	**7,750,284,747.56**

3.6.7 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya shilingi 246,631,737

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika a Biashara limefanya uhaulishaji wa fedha kutoka katika hesabu 0404078000 yenye jumla ya shilingi 246,631,737 kwa ajili ya kumlipa mtoa huduma na msimamizi wa jengo la kitega uchumi ambae ni Kampuni ya Knight Frank lililokuwepo kinazini.

Ukaguzi haukuweza kuthibitisha juu ya huduma inayotolewa na Kampuni ya Knight Frank kutokana na kutokuwepo matumizi na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi hayo. Kutokuwepo kwa ufatiliaji mzuri wa huduma zinazotolewa na mtoa huduma huyo (Knight Frank), kunaweza kupelekea uwezekano mkubwa wa upotevu wa fedha kwa kujitokeza kufanya malipo bila ya kuwepo kwa huduma inayofanyika.

Kufanya hivo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 50: Malipo yaliyokosa vielelezo

Namba	Tarehe	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1	19/8/2019	10,000,000	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
2	2/9/2019	20,000,000	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
3	19/9/2019	4,013,180	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
4	20/11/2019	20,000,000	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
5	-	23,819,621	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
6	17/12/2019	50,000,000	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
7	-	50,000,000	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
8	19/6/2020	30,333,003.60	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
9	-	26,180,378.79	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
10	24/6/2020	12,285,553.67	Knight Frank	Matengenezo madogo madogo
Jumla		**246,631,737**		

Ukaguzi unashauri Shirika la Biashara la Taifa kufanya ufatiliaji wa karibu juu ya huduma (Service Charge) zinazotolewa na kampuni ya Knight Frank kila baada ya Miezi mitatu(3) ili kuweza kuthibitisha usahihi wa fedha wanayolipa na ubora wa huduma inayotolewa, vilevile kuhakikisha vielelezo vya matumizi hayo vinatunzwa na kuwekwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kuondosha dosari inayoweza kujitokeza kwa kukosekana vielelezo vya matumizi hayo.

3.6.8 Madeni ya muda mrefu shilingi 543,605,532.33

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambapo Shirika limechukua jitihada za kuhakikisha deni hilo linapungua ingawa bado shirika linasumbuliwa na uwepo wa deni hilo la muda mrefu ambalo linatokana na ukodishwaji wa Jengo la Kitega Uchumi Gulioni, jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa shirika kujiendesha kiufanisi.

Aidha, uwepo wa ulipaji usioridhisha kwa wadaiwa hao kunapelekea kujitokeza kwa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa Shirika na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali.

Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa umakini wa ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.

Ukaguzi unashauri Shirika la Biashara la Taifa kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni ikiwemo kuweka tozo kwa watakaovuka muda uliowekwa wa ulipaji wa madeni hayo.

Mchanganuo wa ulipaji wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 51: Madeni ya muda mrefu

Namba	Wapangaji	Fedha inayodaiwa (Shs)	Fedha liyolipwa (Shs)	Deni lililobakia (Shs)
1	Derm Elevetors L.T.D	3,996,640.47	-	3,996,640.47
2	Dai Global Usaid Tanzania Yotzs	23,750,567.03	19,833,752.03	3,916,815.00
3	Claritas Internation Zanzibar L.T.D	10,988,498.18	5,953,413.25	5,035,084.93
4	Amref Health African	40,733,827.03	-	40,733,827.03
5	Brain Company L.T.D	15,066,173.43	-	15,066,173.43
6	Dyness Fransis Mdoe	6,227,455.45	3,706,632.00	2,520,823.45
7	Teddy Junior Trade Bureau	4,980,859.70	-	4,980,859.70
8	Tan Trade	13,682,858.52	-	13,682,858.52
9	Suhail Tours	3,883,835.83	-	3,883,835.83
10	Jubilee Insurance Co.Tz	35,991,651.88	-	35,991,651.88
11	Health Mart	3,847,568.33	-	3,847,568.33
12	First Financial L.T.D	2,673,990.42	-	2,673,990.42
13	House Care Cleaning	1,154,162.02	-	1,154,162.02
14	Aids Business Coalition	339,197,399.34	323,237,682.24	15,959,717.10
15	Vegrab Organic Ferming L.T.D	7,631,517.56	-	7,631,517.56
16	The National Council for Technique Education	40,022,415.92	-	40,022,415.92
17	Public Service Social Security Fund (PSSSF)	74,659,961.05	24,235,021.80	50,424,939.25
18	Ministry of Finance	362,698,793.72	184,688,367	178,010,426.72
19	Zanzibar Utilities Regulatory Authority (ZURA)	59,733,705.55	37,572,629.50	22,161,076.05
20	Legal Services Fasility	19,368,924.82	10,790,113.75	8,578,811.07
21	Lam Consultant	10,247,082.60	-	10,247,082.60

22	Joint Finance Comition Tanzania	31,845,490.15	28,251,258.61	3,594,231.54
23	Jhpiego Corporation	12,404,889.56	9,475,199.57	2,929,689.99
24	Immma Advocate	78,942,819.24	12,381,485.72	66,561,333.52
Jumla		**1,203,731,087.80**	**660,125,555.47**	**543,605,532.33**

KIWANDA CHA MAFUTA YA MAKONYO NA ARKI ZA MIMEA - PEMBA

3.6.9 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda wasiokuwa na mikataba ya kazi shilingi 83,446,725

Kiwanda cha Makonyo – Pemba inao wafanyakazi wa muda (daily pay) kwa ajili ya kufanya kazi mbali mbali za Kiwanda.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 83,446,725 zimetumika kwa ajili ya kuwalipa mishahara wafanyakazi hao kwa kipindi cha mwaka fedha 2019/2020 lakini mikataba yao ya kazi imekosekana kwa ukaguzi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya mwaka 2011. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana:-

Jadweli Nambari 52: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	idadi ya walio lipwa	Malipo kwa wafanyakazi wa muda (Shs)	Eneo la kazi	Maelezo
0307/2019 07/08/2019	004582	7,497,570	22	5,401,385	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Julai 2019.
			10	2,096,185	Kiwandani	
745/2019 09/09/2019	004623	6,805,229	23	4,850,210	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Ogasti 2019.
			9	1,604,940	Kiwandani	
1080/2019 2/10/2019	004666	6,672,424	23	4,555,175	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Septemba 2019.
			9	1,759,435	Kiwandani	
1492/2019 1/11/2019	004715	6,716,564	23	4,525,785	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Oktoba 2019.
			9	1,825,230	Kiwandani	

1862/2019 3/12/2019	004761	8,555,069	23	5,115,855	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Novemba 2019.
			8	1,581,675	Kiwandani	
0025/2020 3/1/2020	004807	6,755,044	23	4,684,650	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Disemba 2019.
			8	1,572,175	Kiwandani	
0453/2020 4/2/2020	-	7,764,144	23	5,395,760	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Januari 2020.
			8	1,824,160	Kiwandani	
0981/2020 3/3/2020	004938	9,857,759	23	5,418,455	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Februari 2020.
			9	1,756,790	Kiwandani	
1554/2020 3/4/2020	004998	11,742,104	23	5,766,445	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Machi 2020.
			8	1,968,965	Kiwandani	
1876/2020 5/5/2020	005050	9,717,514	23	4,926,730	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Aprili 2020.
			9	1,693,295	Kiwandani	
2063/2020 19/5/2020	-	8,535,664	23	5,600,015	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Mei 2020.
			9	2,082,440	Kiwandani	
272/2020 21/7/2020	-	11,820,989	23	5,416,500	Shamba la Mtakata	Mishahara kwa Wafanyakazi wa muda kwa mwezi wa Juni 2020.
			9	2,024,470	Kiwandani	
Jumla				**83,446,725**		

3.6.10 Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda na vibarua kinyume na utaratibu shilingi 4,632,500

Kiwanda cha Makonyo – Pemba inao wafanyakazi wa muda (daily pay) kwa ajili ya kufanya kazi mbali mbali za Kiwanda na kulipa shilingi 8,500 kwa mfanyakazi kwa kila siku anayohudhuria kazini.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 4,632,500 zimelipwa kwa wafanyakazi wa muda na vibarua kwa siku ambazo hawakuhudhuria kazini. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo wa malipo wa Kiwanda aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar Nambari 2 ya mwaka 2011. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 53: Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda na vibarua

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha zilizolipwa (Shs)	Fedha za mshahara zilizolipwa (Shs.)	Fedha za Mshahara alizostahiki kulipwa (Shs.)	Tofauti ya mshahara (Shs)	Maelezo
0307/2019 7/8/2019	004582	7,497,570	7,497,570	7,446,570	51,000	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata kwa mwezi Julai, 2019.
0745/2019 9/9/2019	004623	6,805,229	6,715,000	6,460,000	255,000	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata pamoja na posho la Bwanashamba
1080/2019 2/10/2019	004666	6,672,424	6,314,610	5,847,110	467,500	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata kwa mwezi Septemba, 2019.
1492/2019 01/11/2019		6,716,564	6,351,015	6,053,515	297,500	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata kwa mwezi Oktoba, 2019.

1862/2019 3/12/2019	004761	8,555,069	6,138,850	5,737,350	399,500	Malipo ya mishahara kutwa kwa mwezi Novemba, 2019.
1876/2019 4/12/2019	004765	3,254,500	584,500	533,500	51,000	Malipo ya wafanyakazi wa kutwa Kiwandani
0025/2020 3/1/2020	004807	6,755,044	6,257,230	6,257,230	-	Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda kwa mwezi Disemba, 2019.
0453/2020 4/2/2020	-	7,764,144	7,219,920	7,211,420	8,500	Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda Kiwandani, Mtakata na Mamoja
0981/2020 3/3/2020	004938	9,857,759	7,175,245	6,673,745	501,500	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa kutwa na kwa mwezi wa Februari,2020
1554/2020 3/4/2020	004998	11,742,104	7,735,410	7,548,410	187,000	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda waliotumikia mwezi wa Machi, 2020.
1876/2020 5/5/2020	005050	9,717,514	6,620,025	6,093,025	527,000	Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa muda na kutwa.

2063/2020 19/5/2020	-	8,535,664	7,682,455	7,291,455	391,000	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata kwa kazi mbali mbali za Kiwandani.
2098/2020 21/5/2020	-	2,363,000	2,363,000	1,572,500	790,500	Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa kutwa wa Kiwanda kwa shughuli za uzalishaji.
0272/2020 21/7/2020	-	11,820,989	8,318,489	7,612,989	705,500	Malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa muda wa Kiwandani na Mtakata kwa kazi mbali mbali za Kiwandani.
Jumla					**4,632,500**	

3.6.11 Deni la kiwanda kwa watoa huduma shilingi 8,114,990

Ukaguzi umebaini kwamba Kiwanda cha Makonyo kinadaiwa jumla ya shilingi 8,114,990 na watoa huduma mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Kulimbikiza madeni kwa muda mrefu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) (b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo

Jadweli Nambari 54: Orodha ya watoa huduma ambao wanalidai shirika

Namba	Watoa huduma	Fedha wanazodai (Shs)
1.	Nassor Said Nassor	1,295,930
3.	Tahfif Auto Works	1,399,480
5.	Mbarouk Salim Ali	1,104,320
6.	Zanzibar Port Corporation	4,315,260
Jumla		**8,114,990**

3.6.12 Hasara iliyosababishwa na uvujaji wa mafuta wakati wa uzalishaji shilingi 101,144,000

Kiwanda cha makonyo kinafanya uzalishaji wa mafuta ya makonyo kwa kutumia vyungu vitano ambavyo vinamilikiwa na kiwanda kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa viwango vya uzalishaji kiufanisi, kilogramu 700 za makonyo zinatakiwa zizalishe kilogramu 33 za mafuta ambapo kwa sasa zinazalisha chini ya kiwango hicho. Ikiwa bei ya kilogramu moja ya mafuta kwa kipindi cha 2019/2020 ina thamani ya shilingi 80,000 hivyo ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 101,144,000 ni hasara itokanayo na uzalishaji wa mafuta ya makonyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hasara hiyo imesababishwa na uvujaji wa mafuta katika vyungu vya uzalishaji unaotokana na kutokufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Mchanganuo wa hasara hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 55: Mchanganuo wa hasara ya uvujaji wa mafuta

Mwezi	Kiwango cha Makonyo (Kg)	Mafuta yanayopaswa kuzalishwa (Kg)	Mafuta halisi yaliyozalishwa (Kg)	Tofauti (Kg)	Hasara (Shs.)
Novemba	11,260	530.8	253	277.8	22,224,000
Januari	21,298	1,004	959	45	3,600,000
Machi	70,929	3,343.8	3318	25.8	2,064,000
Aprili	21,725	1,024.2	177	847.2	67,776,000
Mei	41,057	1,935.5	1,867	68.5	5,480,000
Jumla	**166,269**	**7,838.3**	**6,574**	**1264.3**	**101,144,000**

3.6.13 Mafuta ambayo hayakuingizwa katika daftari la ghalani shilingi 2,674,800

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 2,674,800 zimelipwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta lakini mafuta hayo hayakuingizwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi yake. Kutokuingizwa mafuta katika daftari la ghalani ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonesha katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 56: Mafuta ambayo hayakuingizwa ghalani

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
75/2020, 7/1/2020	004818	1,770,800	Zanzibar Petroleum LTD	Ununuzi wa Mafuta ya gari petrol ltrs 400
1153/2020, 9/3/2020	004949	904,000	Zanzibar Petroleum LTD	Malipo ya ununuzi wa Mafuta ya diesel ltrs 400
Jumla		**2,674,804**		

Maoni ya Ukaguzi

Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Biashara la Taifa kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Biashara la Taifa limepata hati yenye shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.7 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 14,880,312,387.7 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 16,210,994,551.7 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 1,330,682,164 sawa na asilimia 8.9.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Shirika la Meli Na Uwakala Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 15,602,644,040 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 16,759,823,599 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 1,157,179,559 sawa na asilimia 7.4.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA

Mwenendo Usioridhisha wa hali ya kifedha

Kwa miaka miwili, Shirika la Meli limekuwa na mwenendo usioridhisha kwa kupata hasara mfululizo. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hasara iliyopatikana ilikuwa shilingi 548,829,047.17 na kwa hesabu za mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019, hasara ilikuwa shilingi 722,331,653.16. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya uendeshaji wa meli pamoja na ongezeko la gharama za uendeshaji wa meli.

Mfululizo wa hasara hizo una athari kubwa kwenye Mtaji wa Shirika, hivyo kulifanya kutokopesheka ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha.

Aidha, kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2020, madai yameongezeka kwa asilimia 28.75, hadi shilingi 10,613,722,819.77 kutoka shilingi 8,243,483,029.18 zilizoripotiwa kwenye hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2019. Kwa upande mwengine, thamani ya wadaiwa imeongezeka hadi shilingi 958,469,686.45 kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni 2020, kutoka shilingi 681,131,184.63 zilizoripotiwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2019.

Hali ya uwiano wa mali na madeni hairidhishi, na kuna viashiria vinavyoonesha kwamba Shirika haliwezi kugharamia mahitaji yake ya kifedha.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Meli kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa mapato na kuimarisha mahitaji yake ya kifedha.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.7.1 Kutowasilisha makato ya kisheria shilingi 203,895,169

Ukaguzi ulipitia taarifa za makato ya kisheria kwa Shirika la Meli na kubaini kwamba, jumla ya kiasi cha fedha kilichotajwa hapo juu kinachojumuisha makato ya kisheria ya kodi ya mapato kutoka katika mshahara (PAYE) ya shilingi 135,508,821 na kodi ya ujuzi na maendeleo (SDL) yenye thamani ya shilingi 68,386,347 hayakupelekwa katika Mamlaka ya mapato ya Tanzania (TRA).

Madeni hayo yameendelea kuongezeka kwa miaka kadhaa. Hali hii huweza kupelekea kulipa faini, riba, na adhabu ambazo zitaathiri hali ya kifedha ya Shirika la Meli hivyo kupelekea kushindwa kufikia malengo yaliyopangwa. Kutokulipa kwa kodi kunaweza kuaathiri kiasi cha mapato ambayo Serikali ingepata.

Uongozi wa Shirika la Meli unashauriwa kufanya jitihada za ziada ili kuhakikisha makato yote ya kisheria yanapelekwa kwenye taasisi husika kwa wakati. Hali hii itasaidia kuepuka faini, riba na adhabu zisizokuwa za lazima.

3.7.2 Kukosekana kwa ufanisi katika uendeshaji wa Meli ya MT Ukombozi II

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishi Juni 2020 ukaguzi ulipitia taarifa za mapato na matumzi ya meli mpya ya MT Ukombozi II kwa lengo la kuangalia ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa meli hiyo na kubaini kwamba jumla ya fedha kiasi cha shilingi 2,471,430,196.76 zilitumika ikiwa ni sehemu ya gharama za uendeshaji wa meli ya MT Ukombozi II ukilinganisha na mapato halisi yaliyopatikana kupitia meli hiyo ambayo ni jumla ya shilingi 287,495,145.18. Aidha ukaguzi umelifuatilia zaidi na kubaini kwamba meli mpya ya mafuta MT Ukombozi II tangu ilipowasili Zanzibar ilifanya safari moja tu baada ya Serikali kuikabidhi meli hii mpya ya Mafuta mnamo

tarehe 01 Oktoba 2019. Kukosekana kwa ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa meli hii mpya kumepelekea Shirika la Meli kukosa mapato ambayo yangeweza kusaidia kumudu gharama za uendeshaji na kulifanya shirika kujiendesha kiufanisi.

Uongozi wa Shirika la Meli unashauriwa kufanyia kazi changamoto za kiundeshaji na kiufundi zinazoikabili meli hii ili Shirika liweze kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato kupitia vyombo vyake vya usafiri ili kuweza kupatikana ufanisi na tija.

3.7.3 Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Viashiria vya Hatari kwa Taasisi

Suala la kuhakikisha viashiria vya hatari kwa taasisi vinatambulika na kutafutiwa ufumbuzi ni mbinu mojawapo ya kuhakikisha malengo ya taasisi yanafanikiwa. Hatua hii inahusisha utambuzi wa viashiria vya hatari, mapitio ya viashairi hivyo, uchambuzi wa viashiria hivyo pamoja na kutafuta ufumbuzi kwa viashiria vinavyoonekana kuathiri kufikiwa kwa malengo ya taasisi.

Hata hivyo, Shirika la Meli halijaandaa mfumo wa namna ya kufanya utambuzi wa viashiria vya hatari kwa Shirika jambo ambalo lingesaidia kuepukana na viashiria vinavyoweza kupelekaa kuathiri utendaji wa Shirika la Meli katika uendeshaji wa meli pamoja shughuli za uwakala ili kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kukosekana kwa mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari kwa Shirika kumepelekea kusita kwa utoaji wa huduma za meli kwa muda mrefu na kusababisha usumbufu kwa abiria ambao ni wananchi wanaotegea huduma za meli za Serikali kwa kiwango kikubwa kutokana na gharama nafuu za tiketi za safari kwa upande wa wasafiri wa Unguja na Pemba.

Uongozi wa Shirika la Meli unashauriwa kuanzisha mfumo wa usimamizi wa viashiria vya hatari kwa Shirika katika uendeshaji na utoaji wa huduma za meli na Uwakala jambo ambalo linaweza kusaidia kuepukana na viashiria vinavyoweza kupelekea kuathiri utendaji wa Shirika la Meli katika uendeshaji wa meli pamoja shughuli za uwakala na malengo mapana ya Shirika ya utoaji wa huduma.

3.7.4 Kukosekana kwa Ripoti ya kiufundi katika usimamizi wa matengenezo ya Meli ya MV Maendeleo uliogharimu shilingi 3,322,810,664.23

Katika kupitia taarifa za fedha za Shirika la Meli kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020 ukaguzi umebaini kwamba jumla shilingi 3,322,810,664.23 ni gharama ya fedha zilizotumika kwa ajili ya kuifanyia matengenezo makubwa meli ya MV Maendeleo iliyopo chelezoni Mombasa Kenya. Pamoja na gharama kubwa iliyotumika katika matengenezo hayo kumekosekana ripoti ya kiufundi kutoka katika idara ya ufundi ya Shirika la Meli ambayo inawajibika kutolea taarifa za matengenezo ya Meli zote za Shirika kutokana na uharibifu pamoja na pale chombo kinapohitajika kufanyiwa matengenezo mara kwa mara ili kutoa picha halisi ya vifaa pamoja matengenezo husika yaliyofanyika kabla ya malipo kufanyika.

Kukosekana kwa ripoti ya kifundi ya matengenezo ya meli ya MV Maendeleo kumepelekea kutokuwepo kwa thamani ya mchango wa kiufundi kutoka idara ya ufundi ya Shirika la Meli pamoja na kutokuwepo kwa uwazi wa gharama kubwa zinazotumika katika matengenezo ya meli hiyo ya MV Maendeleo ambayo kwa kipindi kirefu zaidi ya mwaka mmoja ipo chelezoni Mombasa Kenya.

Uongozi wa Shirika la Meli Zanzibar unatakiwa kuhakikisha kwamba idara ya ufundi ya Shirika la Meli inatekeleza majukumu yake ipasavyo ili tija ya uwepo wa idara katika kusimamia matengenezo ya meli za shirika iweze kupatikana.

Maoni ya Ukaguzi

Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonyesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar limepata Hati inayoridhisha yenye aya za msisitizo yaliyotajwa hapo juu kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.8 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Taarifa za mapato

Mapato ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar yameongezeka kutoka shilingi 110,270,566,408 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 114,372,053,812 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na ongezeko la mapato ya shilingi 4,101,487,404 sawa na asilimia 3.7.

Taarifa za matumizi

Matumizi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar yamepungua kutoka shilingi 48,658,332,212 kwa mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi 42,320,530,058 kwa mwaka 2019/2020 kukiwa na upungufu wa matumizi ya shilingi 6,337,802,154 sawa na asilimia 13.

3.8.1 Kutofanyia kazi mapendekezo ya ripoti ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji (Actuarial valuation report) kama ilivyoelekezwa na Bodi

Katika kikao chake cha tarehe 29 Septemba, 2019, Bodi ilipokea ripoti ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji (Actuarial valuation report) iliyotayarishwa na kampuni ya African Risk and Insurance Services kwa mwaka 2018. Ripoti hiyo ilibainisha kasoro ambazo zinahitaji mikakati imara ichukuliwe na Uongozi wa ZSSF ili kuongeza uendelevu na ukwasi wa Mfuko.

Ripoti hiyo ilibainisha hatari kubwa zikiwemo uwekezaji katika mali zisizolipa na zisizopangiliwa vizuri, faida ndogo kutokana na uwekezaji na wigo mdogo wa michango ya wanachama. Ripoti ilitahadharisha kuwa iwapo kama hatua za kurekebisha hali ya ukwasi ya Mfuko hazitochukuliwa, fedha zitakazokuwa zinaingia katika Mfuko wa ZSSF zitazidiwa na fedha zitakazokuwa zinatoka katika Mfuko katika kipindi cha baina ya mwaka 2039 hadi 2050. Hata hivyo, ripoti haikueleza ni lini hasa Mfuko utafilisika.

Baada ya kupokea ripoti hiyo, Bodi iliagiza Uongozi wa Mfuko kufanyia kazi mapendekezo ya ripoti hiyo ya tathmini ya makisio ya takwimu zinazohusiana na uhai wa wachangiaji ikiwemo kupitia upyamuundo wa mkusanyiko wa uwekezaji, kuwekeza katika uwekezaji wenye tija ya kutosha, uwekezaji katika miradi inayolipa haraka pamoja na kuwa na uanishaji mzuri wa mitaji.

Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 ZSSF ilikuwa na vitu vifuatavyo:-

i) ZSSF imewekeza kwa kiasi kikubwa katika majengo ikiwemo ujenzi unaoendelea shilingi bilioni 29. Aidha, tumebaini faida ndogo inapatikana katika majengo ikiwemo nyumba za Mbweni ambazo mauzo yake yamepata hasara ya asilimia 2.

ii) Uwepo wa uwekezaji usio na tija ikiwemo shilingo bilioni 3.15 zilizowekezwa ZAFICO.

iii) Uwekezaji wa baadae umepangwa uwe katika majengo. Mradi wa kukamilisha majengo matatu yaliyopo Mbweni pamoja utafutaji fedha kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya Mradi wa Mji Mpya Kwahani.

iv) Wigo wa Michango hauridhishi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba ZSSF imewafikia asilimia 17 tu ya watu walioajiriwa. Aidha hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2020, Mfuko ulikuwa unadai michango ya shilingi bilioni 1.256.

Kutokufanyia kazi ushauri wa kitaaalam wa mtathmini wa vihatarishi unaweza kupelekea Mtiririko wa fedha na uwekezaji unaweza kushindwa kulipa madeni ya Mfuko.
Uongozi wa ZSSF upitia muundo wake wa uwekezaji na ipeleke fedha nyingi katika miradi yenye tija na inayolipa haraka.

3.8.2 Mapungufu katika udhibiti wa Bajeti iliyoidhinishwa

(a) Matumizi yaliyozidi kiwango cha bajeti pasi na kupata idhini, shilingi 2,001,314,302

Kanuni nambari 6.2.2 ya Kanuni ya Fedha ya ZSSF inamruhusu Mkurugenzi Mkuu kufanya matumizi kama yalivyoidhinishwa na Bodi ya Wadhamini. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka wa fedha huu, matumizi yalizidi bajeti kwa shilingi 2,001,314,302, na bodi ya wadhamini hawakuidhinisha matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni nambari 15.5 ya Kanuni ya Fedha ya ZSSF ambayo inasema "hakuna matumizi yatakayoruhusiwa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa". Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 4**.

(b) Hakuna udhibiti wa moja kwa moja kuhakikisha kuwa matumizi yanadhibitiwa dhidi ya bajeti.

Nyaraka za matumizi ikiwemo fomu za maombi ya malipo na hati za malipo hazina maelezo ya udhibiti wa bajeti ili kuangalia kama kifungu husika cha bajeti kimeshatumia fedha zote, hitaji la kufanya uhaulishaji au kifungu kimeshazidi kiwango cha bajeti. Aidha, mfumo wa uhausibu hauna udhibiti wa kuzuia matumizi zaidi ya bajeti.

(c) Ripoti za Utekelezaji za Kila mwezi haziandaliwi ili kupima utekelezaji

Kanuni ya 7.6.7 ya kanuni inataka kutayarishwa ripoti ya utekelezaji ya mwezi ili kulinganisha na bajeti. Uchambuzi na sababu za tofauti zinahitaji kufuatiliwa kwa makini pamoja na kuchukua hatua muafaka mapema iwezekanavyo. Hata hivyo, ukaguzi haukupata ripoti za utekelezaji ili kupima utekelezaji.

3.8.3 Udhaifu katika Usimamizi na Udhibiti wa Mapato ya Kodi za Pango

Ukaguzi umebaini kasoro zifuatazo katika usimamizi wa mapato ya kodi za pango

(a) Uwepo wa deni la muda mrefu la wadaiwa shilingi milioni 826.

Uzoefu wa upangishaji unataka kodi kulipwa kwa kutangulizwa fedha kabla ya nyumba kukaliwa na mpangaji. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa ZSSF inaruhusu wapangaji kutumia ofisi na nyumba pasi na kulipa kodi. Ukaguzi ulitembelea majengo ya Mbweni, Mwanakwerekwe, Hotel ya Mapinduzi na hoteli ya Achipelago na umebaini uwepo wa kodi inayodaiwa ya shilingi milioni 826.
Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 57: Madeni yatokanayo na ukodishwaji wa majengo ya ZSSF

Namba	Jengo lililokodishwa	Fedha za kodi zinazodaiwa (Shs)
1	NIDA	54,500,000
2	Archipelago Hotel	180,220,236
3	Mnarani – PBZ	14,016,884
4	Zanzibar Cable Television	56,000,000
5	Mwanakwerekwe	80,419,611
6	Jumba la Treni	38,000,000
7	Mbweni old	169,212,078
Jumla		**592,368,809**

i) Ufuatiliaji mdogo wa kodi inayodaiwa. Hakukuwepo na ripoti za uongozi zilizotayarishwa kuhusiana na kodi zinazodaiwa na maamuzi ya uongozi.
ii) Mfumo hauwezi kutoa Ripoti ya umri au muda wa madeni yanayodaiwa.
iii) Hakuna mikataba na wapangaji

3.8.4 Kasoro zilizobainika katika mikopo ya Wafanyakazi

Ukaguzi umebaini kasoro zifuatazo katika usimamizi wa mikopo ya wafanyakazi:-

(a) Mikopo ya wafanyakazi iliyotolewa shilingi bilioni 1.154 haikuidhinishwa na Bodi ya Wadhamini

Ukaguzi umebaini kuwa bajeti ya mikopo ya wafanyakazi kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2020 ilikuwa ni shilingi milioni 500. Hata hivyo, mikopo iliyotolewa ndani ya mwaka ilikuwa ni shilingi bilioni 1.154. Kanuni za fedha za ZSSF zinamruhusu Mkurugenzi Mkuu kutumia fedha kama zilivyotajwa na kuidhinishwa katika bajeti. Kwa tofauti hiyo kubwa, kulikuwa na haja ya kupata idhini ya Bodi ya Wadhamini. Hatahivyo, ukaguzi haukupatiwa idhini ya Bodi ya Wadhamini kwa tofauti hiyo.

(b) Mikopo iliyotolewa haikukatwa kodi.

Sheria ya Kodi ya Mapato 2004 inaainisha vigezo vya mikopo kutokukatwa kodi ni lazima isiwe mara tatu ya mshahara na iwe inarejeshwa si zaidi ya miezi 12. Hata hivyo tumebaini kuwa mikopo inazidi mara 3 ya mshahara, haina riba na inarejeshwa zaidi ya miezi 12.

i) Hakuna ukomo wa jumla ya mikopo ya Wafanyakazi.
ii) Wafanyakazi wenye mikopo wanapatiwa mishahara tangulizi.

Kutoa mikopo pasi na idhini ya Bodi ya Wadhamini kunapelea kutumia vibaya fedha za Mfuko wa ZSSF aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwa mikopo isiyotozwa kodi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa ZSSF kufanya mapitio ya sera ya mikopo kwa wafanyakazi ili kuhakikisha kasoro zilizobainishwa na ukaguzi zinakwenda kufanyiwa marekebisho ili kuepusha hasara za zitokanazo na mikopo hiyo.

3.8.5 Kukosekana kwa uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa malipo ya gharama za awali za Mradi wa Mji Mpya Kwahani, shilingi bilioni 1.19.

Tarehe 4 Oktoba, 2019, ZSSF iliingia mkataba na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya ufadhili wa Mradi wa Mji Mpya Kwahani. Katika utangulizi, mkataba huo unasema kwamba Mkopaji (Wizara) amekubali kulipa gharama za awali zilizolipwa na Mkopeshaji (ZSSF) pasi na kutaja gharama halisi zilizolipwa hadi mkataba huo unawekwa saini. Gharama za awali zilikuwa ni shilingi bilioni 1.19 wakati wa kusaini Mkataba. Bakaa ni kubwa na thamani yake ilipaswa kutajwa katika Mkataba.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa barua ya tarehe 6 Oktoba, 2019 kutoka ZSSF kwenda kwa Katibu Mkuu (OR) Fedha na Mipango inayoomba uthibitisho kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Hatahivyo, ukaguzi hakupata barua kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayokubali bakaa inayodaiwa. Hali hii inaleta maswali iwapo gharama za awali za Mradi zitarejeshwa kwa ZSSF ama hazitarejeshwa.

Kukosekana kwa barua kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango inayokubali bakaa inayodaiwa. ZSSF inawezekana kuwa imepata hasara ambayo haitalipika baadae. Ukaguzi unashauri ZSSF waombe barua ya kukubali deni (commitment letter) kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa gharama za awali zilizotumika.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.9 MFUKO WA BARABARA ZANZIBAR (ZRF)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Mfuko wa Barabara yameongezeka kutoka shilingi 12,437,192,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 13,530,051,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 1,092,859,000 sawa na asilimia 8.8.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Mfuko wa Barabara yameongezeka na kufikia shilingi 15,858,422,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kutoka shilling 11,669,313,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 4,189,109,000 sawa na asilimia 35.9.

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Mfuko wa Barabara kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 58: Ufanisi wa utendaji wa Kifedha

	Mwaka wa Fedha 30/06/2020 (Shs)	Mwaka wa Fedha 30/06/2019 (Shs)
Mali za muda mfupi (Total current Assets)	13,975,203,000	10,814,829,000
Dhima za muda mfupi (Total Current Liabilities)	11,735,343,000	5,343,299,000
Mali Halisi za muda mfupi (Working Capital)	2,239,860,000	5,471,530,000
UWIANO:		
Uwiano (current ratio)	1.2:1	2:1
Kipimo cha Uwiano (Normal Current Ratio)	**2:1**	2:1

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika uwezo wa Mfuko wa barabara kumudu madeni ya muda mfupi umepungua kufikia uwiano wa 1.2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020 ukilinganisha na uwiano wa 2:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2019, kutokana na upungufu huo, ukaguzi umebaini kuna upungufwa uwezo wa shirika kumudu madeni ya muda mfupi. Hali hii kama ikiendelea Mfuko unaweza kushindwa kumudu madeni ya muda mfupi.

Kwa mujibu wa vigezo vinavyotakiwa kiuhasibu vya uwezo wa Mfuko wa Barabara kumudu madeni ya muda mfupini uwiano wa 2:1 ambapo unaonesha uwezo mzuri wa kifedha wa Mfuko kumudu madeni ya muda mfupi.

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe na Mfuko ili kuboresha uwiano wa mali za muda mfupi pamoja na madeni ya muda mfupi.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.9.1 Ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi za ukarabati wa barabara

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020, Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF) ulisaini mikataba ya utendaji wa mwaka (Annual Performance Agreements) baina yake na Wizara ya Mawasiliano pamoja na Wizara ya Tawala za Mikoa ambapo ulipanga kutumia shilingi 14,553,985,000 kwa ajili ya kazi ya matengenezo ya barabara.

Kwa upande wa Wizara ya Mawasiliano ilipangiwa kutumia shilingi 8,926,984,751, Wizara ya Mawasiliano - Pemba ilipangiwa kutumia shilingi 1,786,506,899 na Tawala za Mikoa walipangiwa kutumia shilingi 3,723,097,000.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 ni shilingi 4,632,742,734 kati ya 14,553,985,000 zimetumika na kubaki na bakaa ya shilingi 9,921,242,267 ya fedha ambazo hazikutumika sawa na asilimia 68 ya makadirio.

Hii inatokana na ucheleweshaji wa utekelezaji wa kazi za ukarabati wa barabara zilizopangwa ambapo kwa mwaka wa fedha ulioshia 30 Juni, 2020, kati ya miradi 16 iliyopangwa kutekelezwa, miradi 4 haikutekelezwa kabisa na 2 imechelewa kukamilishwa.

Kutokana na hali hiyo ya ucheleweshaji katika utekelezaji wa mradi husababisha kuongezeka kwa muda, matumizi ya fedha zaidi ya bajeti iliyopangwa, kukosekana kwa ubora wa mradi na wakati mwengine kutelekezwa kwa mradi.

Ukaguzi unashauri kwa Uongozi wa Mfuko wa Barabara kuhakikisha kuwa na upangaji na utekelezaji mzuri wa miradi, uteuzi wa wakandarasi na ufuatiliaji wa miradi kwa wakati katika kila hatua ya utekelezaji.

Mchanganuo wa utekelezaji wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo, na maelezo zaidi **Kiambatisho nambari 5** kinahusika.

Jadweli Nambari 59: Mchanganuo wa miradi iliyotekelezwa

Namba	Maelezo ya miradi	Fedha zilizopangwa Katika utekelezaji (Shs)	Fedha halisi iliyotumika katika utekelezaji (Shs)	Tofauti ya fedha (Shs)	Asilimia
1.	Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi- Unguja	8,926,984,751	1,981,644,020	6,945,340,731	**78**
2.	Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi- Pemba	1,786,506,899	1,674,394,820	112,112,079	**6**
3.	Emergency both MOICT Unguja and Pemba	117,396,350	117,396,350	-	**0**
4.	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	3,723,097,000	859,307,544	2,863,789,456	**77**
Jumla		**14,553,985,000**	**4,632,742,734**	**9,921,242,267**	**68**

3.9.2 Kukosekana kwa ushahidi wa mapokezi ya vifaa shilingi 134,321,000

Ukaguzi umebaini kuwa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) iliwalipa wauzaji wa kokoto, mchanga na vifaa vyengine vya ujenzi vyenye jumla ya shilingi 134,321,000. Hata hivyo ukaguzi haukupata ushahidi wa daftari la kumbukumbu la mapokezi ya vifaa hivyo ili kuthibitisha kupokelewa kwa vifaa hivyo. Badala yake Idara ya UUB ilipokea hati ya mapokezi ya vifaa ambayo pia haionyeshi idadi ya magari yaliyoleta vifaa hivyo. Hii inatokana na kukosekana kwa usimamizi wa mkataba ili kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa vifaa vilivyopokelewa tu.

Kukosekana kwa ushahidi wa mapokezi ya mchanga na kokoto kunaweza kupelekea malipo kufanyika kwa vitu ambavyo havikupokelewa jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya 2016.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Idara kuhakikisha kuwa wanaweka na kusimamia udhibiti mzuri katika manunuzi ili kuhakikisha kuwa malipo yanafanyika kwa bidhaa zilizopokelewa. Mchanganuo wa vifaa vilivyolipwa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 60: Wasambazaji wa vifaa na fedha zilizotumika

Tarehe	Namba ya Hati ya Malipo	Wasambazaji	Mradi	Kiasi Kilicholipwa (Shs)
28/01/2020	18/01	Zinamola General Traders	Provision PM Institute of Technology	48,321,000
23/01/2020	14/01	Salum Ali Mussa	RM Patchwoks	34,000,000
31/07/2019	02/07	Salum Ali Mussa	Kiembe samaki Mnazimmoja	26,000,000
20/12/2019	15/12	Salum Ali Mussa	RM Patchwoks	26,000,000
Jumla				**134,321,000**

3.9.3 Mikataba iliyosainiwa kwa wakandarasi walio na leseni zilizomalizika muda na wasio na leseni

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Ujenzi Mawisiliano na Usafirishaji (MOICT) ilisaini mikataba ya ujenzi kwa wakandarasi yenye jumla ya shilingi 282,549,640 ambao leseni zao za biashara zilikwisha muda na wengine hawakuwa na leseni.

Kutoa zabuni kwa wakandarasi ambao leseni zao za biashara zilikwisha muda na wengine kutokuwa nazo kabisa kunapelekea kutoa zabuni kwawakandarasi wasio na sifa na ambao hawajasajiliwa.

Ukaguzi unaishauri Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji kuimarisha udhibiti wa ndani juu ya mchakato wa zabuni, tathmini na utoaji wa mikataba.

Aidha ukaguzi unapendekeza kwa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji inatakiwa ihakikishe nyaraka zote zinazoambatanishwa katika mikataba ni halali na za kuaminika.

Uchambuzi wa mikaba hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

Jadweli Nambari 61: Orodha ya Wakandarasi ambao leseni zao zimemaliza muda

Jina la Mradi	Jina la Mkandarasi	Nambari ya Mkataba	Utekelezaji wa Mawakala	Jumla ya Fedha (Shs)	Tarehe ilipoisha leseni
Road Marking of Mazizini-fumba 18km)	M/S EdgePoint Company Limited	SMZ/PO1/W/ RB/2019-20-5	MOICT	218,651,640	Leseni iliisha tarehe 05 Julai 2020
Routine Miantanance for Paved Roads for (Machomane-Vitongaji, Chake-chake -Wesha na chanjaani-U/ ndege)	Chake chake Youth Co. Ltd	WUMUP/ UUB/RM/ LOT.03/2019	MOICT PEMBA	10,075,000	Leseni iliisha tarehe 31 December 2019
Routine Miantanance for Paved Roads for (Wete Konde)	Hifadhi Ya Mungu Co Ltd	WUMUP/ UUB/RM/ LOT.06/2019	MOICT PEMBA	10,892,000	Hakuna ushahidi wa leseni ya biashara
Routine Miantanance for Paved Roads for (Ole Konde na Madenjani-Mtakao)	Cleaning services co limited	WUMUP/ UUB/RM/ LOT.01/2019	MOICT PEMBA	24,016,000	Hakuna ushahidi wa leseni ya biashara
Routine Miantanance for Paved Roads for (Chanjaani mbugani mtuhaliwa-chokocho)	Bright security Co. Ltd	WUMUP/ UUB/RM/ LOT.02/2019	MOICT PEMBA	18,915,000	Hakuna ushahidi wa leseni ya biashara
Total				**282,549,640**	

3.9.4 Utekelezaji wa kiwango cha chini wa kazi zilizopangwa za matengenezo ya barabara

Makubaliano ya utendaji kazi yaliyoidhinishwa ya 23 Aprili 2020 kwa Wizara ya nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2020 ilikuwa shilingi 3,723,097,000. Ripoti ya kila mwaka kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum ilibainisha kuwa jumla ya shilingi 859,015,544 zilitumika katika kazi za matengenezo ya barabara ambayo ni sawa na asilimia 23 ya shughuli zilizopangwa.

Aidha gharama za usimamizi zilitumika kwa kiwango cha asilimia 54 na gharama za uendeshaji zilitumika kwa asilimia 100.

Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa ushahidi wa wahandisi kutembelea maeneo ya miradi, ukaguzi haukupatiwa ushahidi unaothibitisha wahandisi kutembelea maeneo ya miradi.

Kwa mujibu wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara maalum ,utekelezaji halisi ulikuwa kwa asilimia 83 lakini hakukupatikana vyeti vya kazi zilizokamilishwa alizopelekewa mkandarasi.

Kuchelewa kutoa vyeti na ushahidi wa kazi iliyofanywa kwa malipo husababisha fedha kutokulipwa kwa mwaka wa fedha husika na kupelekea matumizi hayo kuonekana katika kipindi tofauti cha mwaka wa fedha. Aidha kunapelekea wananchi kukosa huduma za maendeleo kwa wakati.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mfuko wa Barabara kuhakikisha unakamilisha shughuli zilizopangwa kwa wakati. Kwa kuongezea, malipo ya kazi zilizokamilishwa yanapaswa kudaiwa na kulipwa kwa wakati kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za hesabu.

3.9.5 Kukosekana kwa ushahidi wa ukaguzi uliofanywa kwa bidhaa zilizonunuliwa shilingi 86,890,900

Kwa mwaka 2019 UUB Pemba ilinunua bidhaazenye jumla ya shilingi 86,890,900 kutoka kwa wauzaji tofauti, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupewa ushahidi kwamba bidhaa zilizonunuliwa zilikaguliwa mara tu baada ya kupelekwa UUB.

Ukaguzi umetia shaka kwamba, bidhaa zinazowasilishwa bila kukaguliwa zinaweza kuwa sio kulingana na mahitaji ya mtumiaji kwa idadi na ubora.

Kutokufanya ukaguzi wa bidhaa mara zinapowasilishwa kwa ajili ya kuhifadhiwa ghalani ni kwenda kinyume na sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma namba 11,2016.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa UUB kuhakikisha bidhaa zote zilizonunuliwa zinakaguliwa mara tu zinalipofikishwa kabla ya kuingizwa ghalani.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mfuko wa Barabara imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.10 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,500,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kutoka vyanzo vyake mbalimbali vya ndani, na shilingi 4,120,900,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini .

Hadi kufikia 30 Juni 2020 jumla ya shilingi 793,735,630.94 zilipatikana kutoka vianzio mbali mbali vya ndani ikiwa sawa na asilimia 52.91 ya makadirio na shilingi 3,441,852,125 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini sawa na asilimia 83.5 ya makadirio.

Taarifa ya matumizi

Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 5,620,900,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 4,181,912,094.49 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 74.4 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.10.1 Kukosekana kwa kamati ya Ukaguzi wa ndani

Kwa mujibu wa kifungu cha 118(1) cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, inataka kila Taasisi inayohusika na bajeti ya Serikali kuwa na kamati ya Ukaguzi wa ndani itakayoteuliwa na Afisa Mhasibu kwa kushauriana na mlipaji mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba shirika la utangazaji Zanzibar haina kamati ya Ukaguzi wa ndani.

Kukosekana kwa kamati ya Ukaguzi wa ndani kunapelekea kutokuwepo kwa chombo kitakacho simamia na kuleta mawasiliano ya vihatarishi na kutoa taarifa kwenye maeneo husika kwa Shirika pamoja na kutoa ushauri kwa Afisa Mhasibu juu ya hatua za kuchukuliwa kutokana na mambo yaliyojitokeza kwenye ripoti ya ukaguzi wa ndani au kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuanzisha kamati ya ukaguzi wa ndani kwa mujibu wa sheria ili kuimarisha usimamizi wa ndani.

3.10.11 Mapungufu katika matumizi ya mafuta shilingi 151,517,080

Ukaguzi ulipitia taarifa za usimamizi wa mafuta na kufanya ulinganisho wa rekodi zilizo kwenye madaftari la kuhifadhia kumbukumbu za mafuta.

Jumla ya shilingi 151,517,080 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta, malipo ambayo yalilipwa kwa wasambazaji wa kampuni ya United Group Limited shilling 133,517,080 na shillingi 18,000,000 kutoka Zanzibar Petroleum kwa ajili ya matumizi ya Shirika. Aidha ukaguzi umebaini kujitokeza kwa mapungufu mbalimbali ya kiutendaji katika uwekaji wa kumbukumbu za mafuta hayo, kasoro zenyewe ni kama hizi zifuatazo:

- Kutokuwepo kwa Daftari la kuonyesha mapokezi na matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa na Shirika.
- Kutokuwepo na taarifa za ulinganishaji wa kumbukumbu za matumizi ya mafuta katika daftari la kurikodiwa mafuta ya Shirika na Kampuni ya Mafuta ili kuweza kuangalia taarifa za usuluhishi wa mafuta.
- Kukosekana kwa mkataba wa manunuzi baina ya Shirika na Kampuni ya Mafuta.

Matumizi ya mafuta kwa Shirika yanagharimu fedha nyingi sana; hivyo basi, kutokuwa na uwekaji na utunzaji mzuri wa kumbukumbu za mafuta huweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha kutokuwapo kwa taarifa za usuluhishi wa mafuta yaliyonunuliwa na kutumika kulipelekea kushindwa kutambua matumizi ya mafuta yaliyonunuliwa. Kwa hiyo, kuna uwezekano wa matumizi yasiyofaa ya mafuta.

Ukaguzi unapendekeza kwa Shirika la Utangazaji kuimarisha udhibiti uliowekwa wa kurekodi matumizi ya mafuta ikiwa ni pamoja na kuweka taarifa sahihi katika daftari la kutunzia mafuta.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura halisi na sahihi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Utangazaji Zanzibar limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.11 SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC)

Taarifa ya Mapato

Shirika la Nyumba Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,035,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya makusanyo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Shirika la Nyumba Zanzibar limekusanya jumla ya shilingi 2,091,811,601.41 ambazo ni sawa na asilimia 68.92 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Shirika la Nyumba Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,011,062,790 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Shirika limetumia jumla ya shilingi 1,980,203,734 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.11.1 Kuripotiwa kwa mapato pungufu ya shilingi 586,000,000

Katika kupitia taarifa za hesabu za mapato ya Shirika la Nyumba ukaguzi umebaini kutokujumuishwa kwa sehemu ya mapato yatokanayo na kodi ambazo huduma ilisha tolewa lakini fedha hazikuweza kukusanywa mpaka kufikia mwisho wa mwaka. Jumla ya mapato yaliyopaswa kuonekana katika hesabu za Shirika ni shilingi 2,617,841,101.4 tofauti na kiwango cha mapato kilichobainishwa katika hesabu za mapato ya Shirika.

Kwa mujibu wa mfumo wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka unaotumiwa na Shirika la Nyumba, mapato na matumizi hutambuliwa pale huduma inapotolewa au kupokelewa na sio wakati wa malipo yanapo pokelewa au yanapofanyika (Cash basis).

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 2,031,841,101.4 zilioneshwa katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ambazo zimekusanywa kwa fedha taslimu na kuwepo tofauti ya shilingi 586,000,000 ambazo hazikurikodiwa katika taarifaa za hesabuna kuwasilishwa.kwa mujibu wa mfumo wa ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka unaotumiwa na Shirika la Nyumba, na kupelekea kubainika kwa dosari ya uwasilishaji wa taarifa za fedha. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kwenda kinyume na Sheria za kimataifa za uandaaji na ufungaji wa hesabu kwa taasisi za Umma (IPSAS).

3.11.2 Ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Nyumba Zanzibar

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Shirika la Nyumba na kubaini kuwa, makusanyo yanatokana na kodi za nyumba na vyanzo vingine yameshuka kutoka shilingi 2,878,682,812.3 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 na kufikia shilingi 2,091,811,601.4 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kwa tofauti ya shilingi 786,871,210.90 sawa na asilimia 10.8.

Aidha Shirika la Nyumba limeendelea kujiendesha kwa hasara katika kipindi cha miaka miwili mfululizo pamoja na kuwa hasara imepungua kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020 ukilinganisha na mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019.

SHIRIKA LA NYUMBA – PEMBA

3.11.3 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 2,243,400

Jumla ya shilingi 2,243,400 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya Shirika. Ukaguzi umebaini kwamba vifaa hivyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016.Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama vifuatavyo:-

Jadweli Nambari 62: Vifaa ambayo havikurikodiwa ghalani

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha Zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1/11 5/11/2019	T.T	1,425,900	Capital Technology Centre.	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa APC Back Up
9/7 23/7/'19	T.T	666,500	Kassim Massoud Nassor	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa Tangi la maji, Zulia, Busati, Feni na ndoo za maji.
10/7 23/7/'19	T.T	151,000	Nassor Said Nassor	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa Vifaa vya usafi.
Jumla			**2,243,400**	

3.11.4 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim shilingi 1,430,000

Jumla ya shilingi 1,430,000zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Nyumba Pemba. Ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo. Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 63: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslimu

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelip-wa	Maelezo
3/10 7/10/2019	000019	550,000	Shirika la Nyumba - Pemba	Malipo ya fedha za mwanzo kwa ajili ya matengenezo ya nyumba No. 31 A & B na 17 zilizopo Wete anayolipwa Nd. Khatib Juma Hamad wa Furaha Chake Chake Pemba.
5/10 11/10/2019	000020	480,000	Shirika la Nyumba – Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya ghrarama za matengenezo ya nyumba iliyopo Madungu Block No. 4.
7/10 21/10/2019	000021	400,000	Shirika la Nyumba – Pemba	Malipo ya fedha za mwisho kwa ajili ya matengenezo ya nyumba No. 31 A & B na 17 zilizopo Wete.
Jumla		**1,430,000**		

3.11.5 Malimbikizo ya madeni ya wapangaji wa nyumba za Shirika shilingi 235,867,500

Ukaguzi umebaini uwepo wa madeni nyenye jumla ya shilingi 235,867,500 ambazo zinadaiwa na Shirika la Nyumba – Pemba kutokana na ukodishaji wa nyumba zake za maendeleo na milango ya biashara.

Aidha ukaguzi umebani kwamba uongozi wa Shirika la Nyumba - Pemba umeshindwa kuchukua hatua zinazostahiki kwa wadaiwa hao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 7(i) cha Mkataba wa ukodishaji wa nyumba za maendeleo na milango ya biashara. Aidha ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangaliweza kutumika kwa shughuli mbali mbali za kimaendeleo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama ufuatavyo:-

Jadweli Nambari 64: Malimbikizo ya madeni

Wilaya	Aina ya nyumba	Aina ya wapangaji	Idadi ya wapangaji	Jumla ya deni
CHAKE CHAKE	Nyumba za Maendeleo – Madungu	Watu Binafsi	25	9,150,000
	Nyumna za Maendeleo - Machomane	Watu Binafsi	15	6,950,000
	Nyumba za Vijiji – Machomane, Wawi, Vitongoji na Chanjaani	Watu Binafsi	7	8,700,000
Nyumba za SMZ – Madungu		Wizara ya Afya	2	11,802,000
	Nyumba za SMZ – Madungu	Mtu Binafsi	1	180,000
	Nyumba za SMZ – Tibirinzi	Watu Binafsi	3	1,440,000
	Nyumba Kutaifishwa – Kichungwani	Watu Binafsi	9	5,400,000
	Nyumba Kutaifishwa – Skioni, Njia kuu, Kilima tinde, Machomane na Tibirinzi.	Watu Binafsi	11	8,925,000
	Milango ya Biashara – Wilaya ya Chake.	Wafanyabiashara	56	22,972,000
JUMLA YA DENI WILAYA YA CHAKE CHAKE				**75,519,000**
MKOANI	Nyumba za Maendeleo – Mapinduzi	Katibu wa CCM W/MKOANI	1	1,400,000
	Nyumba za Maendeleo – Mapinduzi	Katibu wa UV/ CCM W/MKOANI	1	1,800,000
	Nyumba za Maendeleo – Mapinduzi	Watu Binafsi	18	3,900,000
	Nyumba za Maendeleo – Ngo'mbeni	Mtu Binafsi	1	150,000
	Nyumba za SMZ – Kikwajuni	Watu Binafsi	4	1,850,000
	Nyumba za SMZ – Ngo'mbeni	Mtu Binafsi	1	600,000
	Nyumba za Vijiji – Kengeja	Mtu Binafsi	1	135,000
	Nyumba za Vijiji – Muambe	Mtu Binafsi	1	240,000
	Milango ya Biashara – Ng'ombeni	Mfanyabiashara	1	163,500
JUMLA YA DENI WILAYA YA MKOANI				**10,238,500**

WETE	Nyumba za Maendeleo – Mtemani	Watu Binafsi	76	31,050,000
	Nyumba za Maendeleo - Mtemani	K.M.K.M	2	1,900,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Mbuyuni	K.M.K.M	1	950,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Mbuyuni	Watu Binafsi	13	10,550,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Mbuyuni	ZAFAH WILAYA YA WETE	1	2,025,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Kipangani	K.M.K.M	2	1,900,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Kipangani	Watu Binafsi	10	4,350,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Kitutia	Watu Binafsi	5	2,775,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Utaani	Watu Binafsi	1	500,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Selemu	Watu Binafsi	5	3,550,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Selemu	K.M.K.M	1	950,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Bomani	Watu Binafsi	3	2,000,000
	Nyumba za Kutaifishwa – Mitiulaya	Watu Binafsi	2	1,800,000
	Nyumba za SMZ – Police Line Wete	Mrajis	1	5,250,000
	Nyumba za SMZ – Police Line Wete	Watu Binafsi	12	9,700,000
	Nyumba za Vijiji – Limbani	Mtu Binafsi	1	150,000
	Nyumba za Vijiji – Kojani	Watu Binafsi	6	7,155,000
	Milango ya Biashara – Wilaya ya Wete	Wafanyabiashara	59	29,985,000
JUMALA YA DENI WILAYA YA WETE				**116,540,000**
MICHEWENI	Nyumba za Maendeo - Micheweni	ZIPA	1	150,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	Katibu wa CCM Micheweni	1	735,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	UHAMIAJI	2	360,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	Katibu wa CCM	1	735,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	C.C.M	1	735,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	Usalama wa Taifa	2	825,000
	Nyumba za Maendeleo – Micheweni	Watu Binafsi	22	7,980,000
	Nyumba za Vijiji – Maziwa Ng'ombe	Watu Binafsi	12	17,445,000
	Nyumba za Vijiji – Kiuyu Mbuyuni	Watu Binafsi	4	4,605,000
JUMLA YA DENI LA WILAYA YA MICHEWENI				**33,570,000**
JUMLA KUU YA MADENI KWA WILAYA ZOTE				**235,867,500**

Maoni ya ukaguzi

Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Nyumba Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Nyumba Zanzibar limepata hati yenye shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.12 KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 800,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi36,654,150 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 35,854,150 sawa na asilimia 448.17.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 581,923,842 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 853,135,499.42 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 271,211,657.42 sawa na asilimia 46.6.

Ufanisi katika Uendeshaji wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (Operating Performance)

Katika ukaguzi uliofanyika umeweza kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar kwa kufanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020 na kubaini mapato ya Kampuni ya ZAFICO yameongezeka na kufikia shilingi 36,654,150 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 800,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 35,854,150 sawa na asilimia 448.17 ya ongezeko.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 853,135,499.42 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 581,923,842 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 581,923,842 sawa na asilimia 46.6.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kampuni ya Uvuvi ya Zanzibar haikufanya mauzo ya samaki, ukilinganisha na mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na mauzo ya shilingi 87,039,266.

Katika tathmini iliyofanyika kwa vipindi vya miaka miwili Kampuni ya Uvuvi Zanzibar imeendelea kujiendesha kwa hasara, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020 hasara imeonekana kuongezekana kufikia shilingi 816,481,349.42.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato sambamba na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kufikia dhana na malengo ya uanzishwaji wa Kampuni hiyo.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.12.1 Hasara iliyopatikana kutokana na mauzo ya samaki shilingi 50,385,116

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kampuni ya Uvuvi Zanzibar imetumia gharama kubwa ya uzalishaji unaotokana na uendeshaji wa shughuli za uvuvi ukilinganisha na mapato yatokanayo na uuzwaji wa samaki jambo ambalo limepelekea gharama hizo kuongezeka mara mbili zaidi ya pato linalopatikana kutokana na uuzwaji wa samaki, hivyo kukosekana tija na ufanisi wa shughuli zinazoendeshwa na kampuni.

Maelezo ya uzalishaji na uuzaji wa samaki ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Gharama za Uzalishaji (Shs)	Mauzo ya Samaki (Shs)	Hasara ya Uzalishaji (Shs)
87,039,266.00	36,654,150.00	(50,385,116.00)

Ukaguzi umebaini hasara hiyo husababishwa na uzoefu mdogo juu ya shughuli za uvuvi, ukosefu wa vitendea kazi vya kisasa vya uvuvi, na kukosekana kwa uwezo wa kufanya shughuli za uvuvi katika kina kikubwa cha bahari.

Ukaguzi unashauri Serikali kuiwezesha na kuipatia Kampuni ya uvuvi vifaa vya kisasa ambavyo vitawezesha kuweza kufanya shughuli za uvuvi katika kina kikubwa cha bahari kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato yanayotokana na mauzo ya samaki na kupelekea dhamira ya uanzishwaji wa kampuni hiyo kuweza kufikiwa.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Kampuni ya Uvuvi Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Kampuni ya Uvuvi Zanzibar imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.13 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA ZANZIBAR

Taarifa ya mapato

Shirika la Huduma za Maktaba ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 10,300,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Shirika la Huduma za Maktaba limekusanya jumla ya shilingi 2,574,000 ambazo sawa na asilimia 25 ya makadirio.

Taarifa ya matumizi

Shirika la Huduma za Maktaba lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 886,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Shirika la Huduma za Maktaba limetumia jumla ya shilingi 682,580,357.4 ambazo sawa na asilimia 77 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.13.1 Dosari katika utayarishaji wa malipo shilingi 16,885,000

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Huduma za Maktaba limefanya malipo ya shilingi 16,885,000 kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Shirika, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanyika kwa malipo ya fedha kwa njia ya fedha taslimu badala ya kufanya malipo kwa kutumia hundi za benki, jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa vihatarishi katika utunzaji wa fedha za Umma. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo yanaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 65: Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim

Namba	Hati namba	Hundi namba	Aliyelipwa	Jumla ya fedha (Shs)	Maelezo
1	52/6/2020	1923	Shirika la huduma za maktaba	8,900,000	Fedha za malipo kwa hatua ya mwanzo ujenzi wa maktaba Dunga
2	4/7/2019	1658	Shirika la huduma za maktaba	1,000,000	Matengenezo ya chumba cha mkutano cha maktaba unguja
3	9/9/2019	1700	Shirika la huduma za maktaba	3,985,000	Malipo kwa ajili ya maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kujua kusoma
4	24/5/2020	1889	Shirika la huduma za maktaba	3,000,000	Matumizi ya ununuzi vitu mbalimbali
Jumla				**16,885,000**	

3.13.2 Dosari katika taratibu za manunuzi shilingi 57,316,000

Ukaguzi umebaini Shirika la Maktaba limefanya makubaliano ya ujenzi na Kampuni ya Skifaru Investment & Engineering Ltd wenye gharama ya shilingi 57,316,000 kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa Jengo la Maktaba (Dunga), dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa ushindani wa kumpata mkandarasi pamoja na kukosekana kwa mkataba wa ujenzi wa maktaba hio. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi wa Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016, kwa mujibu wa Jadweli la 5 la Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji linaloelekeza taratibu na ukomo wa viwango vya manunuzi.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Huduma za Maktaba Zanzibar limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.14 SHIRIKA LA MAGAZETI

Taarifa ya Mapato

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 838,900,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato na shilingi 845,192,395 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 935,260,525 zilikusanywa ambapo ni sawa na asilimia 111.5 ya makadirio na shilingi 632,994,425 ya ruzuku ilipokelewa kutoka wizarani sawa na asilimia 75 ya makadirio.

Taarifa ya matumizi

Shirika la Magazeti lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,559,592,395 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2019/2020, hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 1,297,644,216.6 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 83 ya makadirio.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WASHIRIKA LA MAGAZETI

Katika utendaji wa kifedha wa Shirika (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinachoonesha namna Shirika linavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa biashara na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Magazeti limebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa "Accrual basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash basis" jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za shirika kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shirika kifaida au hasara.

Ukaguzi unashauri Shirika la Magazeti kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.14.1 Kutokufanya kazi kwa Kamati ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa sheria ya fedha na usimamizi wa mali za umma namba 12 ya mwaka 2016 inaeleza majukumu ya Kamati ya ukaguzi wa hesabu (Audit Committee) ni kama ifuatavyo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Shirika la Magazeti bado halijaanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu (Audit Committee) na hivyo kutumia kamati ya ukaguzi iliyoanzishwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo jambo ambalo ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari ya kutokufanya kazi kwa kamati hiyo na kupelekea kubainika mapungufu mbali mbali katika usimamizi wa ndani wa Shirika la Magazeti ya Serikali kama ifuatavyo:-

- Kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani
- Kutokupitia taarifa za hesabu za Shirika la Magazeti ya Serikali.
- Kutobainisha mapungufu ya ripoti ya ukaguzi wa hesabu yaliyobainishwa na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani na Mkaguzi wa Hesabu wa Nje kwa lengo la kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainika na kulishauri Shirika ili liweze kujiendesha kwa tija.

3.14.2 Manunuzi ambayo yamekiuka utaratibu shilingi 102,364,625

Kifungu namba 42(2)(c) cha sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za umma namba 11 ya mwaka 2016 kinazungumzia katazo la kugawa ununuzi na uondoshaji kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Magazeti ya Serikali limekuwa likigawa manunuzi ya bidha za vifaa vya teknologia ya habari na mawasilano kwa ajili ya kuzuia kutumia njia sahihi za ununuzi kama zilivyoelekezwa katika Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Hii imejitokeza wakati Shirika likifanya manunuzi ya vifaa vya teknologia ya habari na Mawasilano vilivyogharimu shilingi 102,364,625.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 66: Manunuzi yaliyokiuka utaratibu

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Aliyelipwa	Fedha zilizolipwa (Shs)	Maelezo
1	13/12, 18/12/2019	TLM Computer services	11,970,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kompyuta.
2	14/12, 18/12/2019	TLM Computer services	27,930,000	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta.

3	15/12, 18/12/2019	TLM Computer services	29,925,000	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Kamera.
4	16/12, 18/12/2019	TLM Computer services	13,965,000	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi HP
5	44/12, 18/12/2019	FNT Computer Services	10,124,625.00	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Kompyutasaba.
6	1/11, 18/12/2019	FNT Computer Services	8,450,000	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa HP laptop i5 3 GH1 TB 8 GB
Jumla			**102,364,625**	

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Shirika la Magazeti kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Shirika la Magazeti limepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.15 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 7,200,000,000 kupitia vyanzo vyake vya ndani katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Maji Zanzibar imekusanya jumla ya shilingi 3,396,047,461.10 ambazo ni sawa na asilimia 47 ya makadirio.

Mamlaka ya Maji Zanzibar imeshindwa kufikia malengo ya bajeti ya makusanyo kupitia vyanzo vyake vya ndani kwa asilimia 53.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,069,040,459 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 117,286,286,991,843 kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020Mamlaka ya Maji Zanzibar imetumia jumla ya shilingi 6,673,150,626.60 kwa kazi za kawaida ikiwa sawa na asilimia 44 ya makadirio na shilingi 17,026,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 15 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.15.1 Manunuzi ya Mashine na Pampu za maji yaliyokiuka utaratibu wa manunuzi shilingi 126,766,686

Kifungu namba 42(2)(b)(c) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba " Taasisi ya Ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa Ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na zaidi utazingatia kutumia mikataba maalum kwa namna inavyohitajika, kutoa huduma bora zenye gharama nafuu kwa njia inayoweza kubadilika kupata kazi, huduma au usambazaji wa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda.

Aidha, kifungu namba 42(2)(c) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 kinazungumzia katazo la kutokugawa ununuzi na uondoshaji kwa lengo la kutokutumia utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar imekiuka taratibu za manunuzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa fedha zilizotumika katika manunnuzi hayo unaonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 67: Malipo kwa ajili ya manunuzi ya pampu

Namba	Tarehe	Hati za Malipo	Jumla ya fedha (Shs)	Alielipwa	Maelezo
1	23/07/2019	PV 5/7	4,567,797	Equiplus Company ltd	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Grundfos Motor 6'3PH5.5 ya Buyu
2	16/08/2019	PV. 63/8	22,611,839	DJN Kirenga General Supply	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
3	16/08/2019	PV. 64/8	18,913,585	DJN Kirenga General Supply	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
4	6/11/2019	PV 23/11	9,144,000	DJN Kirenga General Supply	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Franklin Motor ya Zawa Chwaka
5	19/11/2019	PV01/11	5,684,000	DJN Kirenga General Supply	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Franklin Motor ya Zawa Basra
6	10/12/2019	PV29/12	3,517,220	Bab Plumbing and water works	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps ya Jambiani Mfumbwi

7	14/12/2019	PV/01/12	11,977,560	H.A Store	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
8	14/12/2019	PV/2/12	6,986,910	H.A Store	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
9	24/12/2020	PV 126/1	2,989,000	Equiplus Company ltd	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
10	24/01/2020	PV 127/1	1,568,000	Quesy Hardware	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
11	22/02/2020	PV 53/2	32,240,775	Reni International	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Pumps
12	10/03/2020	PV-6/3	3,283,000	Trade links and services	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Franklin Motor ya Zawa Chwaka
13	21/04/2020	PV17	3,283,000	Trade links and services	Malipo kwa ajili ya manunuzi ya Franklin Motor ya Zawa Chwaka
Jumla			**126,766,686**		

3.15.2 Ongezeko la gharama za matumizi ya mafuta shilingi 260,597,019

Ukaguzi ulipitia taarifa za usimamizi wa mafuta kwa kuangalia gharama za matumizi ya mafuta kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na matumizi hayo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kubaini uwepo wa tofauti kubwa ya gharama za matumizi ya mafuta isiyo ya kawaida ya shilingi 260,597,019.00 ikiwa ni ongezeko. Mchanganuo wa gharama za mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Nambari 68: Gharama za matumizi ya mafuta

Aina ya Mafuta	Gharama za matumizi ya mafuta kwa 2019/2020 (Shs)	Gharama za matumizi ya mafuta kwa 2018/2019 (Shs)	Tofauti (Shs)
Petroli	97,162,590	27,943,102	69,219,488
Dizeli	254,890,130	63,512,599	191,377,531
Jumla	**352,052,720**	**91,455,701**	**260,597,019**

Ukaguzi ulifuatilia kwa kina ili kutaka kujirisha kutokana na sababu zilizopekea matumizi ya mafuta kuengezeka na kubainika kuwa matumizi hayo yameongezeka kutokana na uwepo wa usimamizi wa mafuta usioridhisha, jambo ambalo limepelekea kupanda kwa gharama za mafuta ukilinganisha na mwaka uliopita.

Matumizi ya mafuta katika Mamlaka ya Maji Zanzibar yanagharimu fedha nyingi sana; hivyo basi, kutokuwa na uwekaji na utunzaji mzuri wa madaftari ya kuratibu safari za magari kunaweza kupelekea mianya ya matumizi mabaya ya fedha za umma.

Ukaguzi unapendekeza Mamlaka ya Maji Zanzibar kuimarisha udhibiti uliowekwa wa kurekodi matumizi ya mafuta ikiwa ni pamoja na kuweka taarifa sahihi katika leja za mafuta, na daftari za kuratibu safari za magari. Kwa kuongeza, lazima kuwe na ufuatiliaji na usimamizi wa kutosha wa mafuta yanayotumiwa na vyombo visivyokuwa vya Mamlaka kwa kazi za ZAWA na uwepo wa kumbukumbu nzuri za mafuta kama taratibu na miongozo inavyoagiza.

3.15.3 Malipo kwa wafanyabiashara wasiosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi shilingi 34,237,762.6

Kifungu cha 23(1) cha sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinazungumzia usajili wa watoa huduma kama inavyoeleza "kwa mujibu wa masharti ya sheria hii mtu, kampuni au Taasisi haitowasilisha ombi au haitoshiri katika zabuni mpaka mtu, kampuni au taasisi hiyo iwe imesajiliwa kama mtoa huduma chini ya sheria hii".

Ukaguzi umebaina kwamba jumla ya shilingi 34,237,762.6 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Maji Pemba kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Kufanya miamala na wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 69: Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	3/7 16/7/2019	002031	846,034	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali
2.	12/7 26/7/2019	002036	912,576	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa cable wire 4
3.	12/8 9/9/2019	T.0	3,528,000	Masim Building Contractor.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa changarawe
4.	13/8 9/8/2019	002053	1,176,000	Soud Talib Juma.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa changarawe
5.	14/8 13/8/2019	002054	1,368,864	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme
6.	17/8 15/8/2019	002057	8,579,165	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ufungaji mita za maji

7.	20/9 16/9/2019	002084	5,637,058	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
8.	43/9 27/9/2019	002096	598,878	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji
9.	44/9 27/9/2019	0002097	224,341.60	Khamis Yussuf Hamad.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viti vya plastiki
10.	7/11 7/11/2019	002128	5,880,000	Soud Talib Juma.	Malipo ya frdha za awamu ya pili na ya mwisho kwa ajili ya ununuzi wa vifaa
11.	9/11 15/11/2019	002129	1,725,339	Khamis Sultan Said.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa
12.	16/11 15/11/2019	T.O	2,352,000	Midodoni Hardware.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
13.	17/3 26/03/2020	2244	304,192	Samail College Of Science And Technology	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya chakula na vinywaji
15.	7/4 14/4/2020	002262	368,600	Khamis Hassan Mgau.	Malipo ya fedha kwa ajili ya uekezaji.
16.	10/4 15/4/2020	002265	736,715	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kamba pamoja na dawa
Jumla			**34,237,762.6**		

3.15.4 Ufanisi katika uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar

Ukaguzi baada kupitia taarifa za fedha za Mamlaka ya Maji Zanzibar ulibaini kuwa, makusanyo yanatokana na mauzo ya maji yameshuka kutoka shilingi 3,137,452,685 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2019 na kufikia shilingi 2,799,196,832 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2020 kwa tofauti ya shilingi 338,255,853sawa na asilimia 10.8.

Aidha Mamlaka ya maji Zanzibar imeimarika kwa kupata faida ya shilingi 182,000,293 ukilinganisha na hasara iliyopatikana katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019.

MAMLAKA YA MAJI – PEMBA

3.15.5 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 6,899,290

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,899,290 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Maji (ZAWA) - Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayoo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 70: Malipo yaliyokosa vielelezo

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	15/8 15/8/2019	002055	1,455,700	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha za marejesho kwa matumizi mbali mbali ya dharura.
2.	42/9 27/9/2019	002077	2,281,000	Sharif Petrol Station	Malipo ya fedha za sehemu ya mwanzo ya ununuzi wa mafuta
3.	2/10 3/10/2019	002101	200,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi ya madogo madogo ya dharura
4.	35/11 27/11/'19	002141	320,000	Mamlaka ya Maji- Pemba	Malipo ya fedha za marejesho kwa ajili ya ununuzi wa chakula
5.	15/3 17/3/2020	2242	2,100,000	Mamlaka ya Maji - Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya walinzi ambao si waajiriwa
6.	2/4 9/4/2020	002258	142,590	Samail Collage of Science and Technology	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya chakula kwa washiriki wa kikao
7.	34/6 25/6/2020	002321	400,000	Mamlaka ya Maji Pemba	Malipo ya fedha ya awamu ya mwisho kwa ajili ya gharama za masomo
JUMLA			**6,899,290**		

3.15.6 Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawajasajiliwa shilingi 34,237,762.6

Jumla ya shilingi 34,237,762.6 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Maji Pemba kwa wafanya biashara tofauti. Ukaguzi umebaina kwamba wafanya biashara hao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Kutokusajiliwa kwa wafanyabiashara na Mamlaka ya Ununuzi ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 71: Malipo kwa wafanyabiashara waliokuwa hawakusajiliwa

Namba	Nambari ya Hati za malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizotumika (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	3/7 16/7/2019	002031	846,034	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali
2.	12/7 26/7/2019	002036	912,576	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa cable wire 4
3.	12/8 9/9/2019	T.0	3,528,000	Masim Building Contractor.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa changarawe
4.	13/8 9/8/2019	002053	1,176,000	Soud Talib Juma.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa changarawe
5.	14/8 13/8/2019	002054	1,368,864	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme
6.	17/8 15/8/2019	002057	8,579,165	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ufungaji mita za maji
7.	20/9 16/9/2019	002084	5,637,058	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
8.	43/9 27/9/2019	002096	598,878	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji
9.	44/9 27/9/2019	0002097	224,341.60	Khamis Yussuf Hamad.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viti vya plastiki
10.	7/11 7/11/2019	002128	5,880,000	Soud Talib Juma.	Malipo ya frdha za awamu ya pili na ya mwisho kwa ajili ya ununuzi wa vifaa
11.	9/11 15/11/2019	002129	1,725,339	Khamis Sultan Said.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa
12.	16/11 15/11/2019	T.O	2,352,000	Midodoni Hardware.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji safi
13.	17/3 26/03/2020	2244	304,192	Samail College Of Science And Technology	Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya chakula na vinywaji
14.	7/4 14/4/2020	002262	368,600	Khamis Hassan Mgau.	Malipo ya fedha kwa ajili ya uekezaji.
15.	10/4 15/4/2020	002265	736,715	Nassor Ali Abdalla.	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kamba pamoja na dawa
Jumla			**34,237,762.6**		

3.15.7 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 276,118,668

Mamlaka ya Maji – Pemba huingia katika makubaliano ya ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbali kutoka kwa wafanyabiashara pamoja na Taasisi za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji – Pemba inadaiwa na wafanyabiashara hao, wafanyakazi pamoja na Taasisi za Serikali jumla ya shilingi 276,118,668 kutokana na kupatiwa bidhaa na huduma mbali mbali. Aidha madeni haya ni ya muda mrefu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) (b) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 72: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu

Mwaka wa fedha	Watoa huduma	Hati za madai	Fedha zinazodaiwa (Shs)
2011/2012	Sapphier Engineering (T) Limited	476, 0486.	16,350,000
	Wizara ya Fedha na Mipango – Pemba	1705, 1711, 1715.	1,140,000
Jumla ndogo			**17,490,000**
2012/2013	Sapphier Engineering (T) Limited	0489, 0497, 0498, 0499.	22,361,000
2012/2013	Wizara ya Fedha na Mipango – Pemba	1721, 1732, 1866.	1,150,000
Jumla ndogo			**23,511,000**
2013/2014	Sapphier Engineering (T) Limited	0351, 0352 na 0193	7,900,000
	Wizara ya Fedha na Mipango – Pemba	1958	150,000
Jumla ndogo			**8,050,000**
2014/2015	Sapphier Engineering (T) Limited	0362	6,500,000
	Sapphier Engineering (T) Limited	0196	3,000,000
Jumla ndogo			**9,500,000**
2015/2016	Zanzibar Petroleum Ltd	027	2,529,250
	Commissioner of Income Tax	PAY ROLL	12,715,527
Jumla ndogo			**15,244,777**
2016/2017	Commissioner of Income Tax	PAY ROLL	24,544,167
	Misufini Stationery Centre	2442	2,625,000
	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 17	Hati ya madai	8,500,000
	Deni la Posho (Oct,2016 – June,2017)	Hati za madai	6,210,000
Jumla ndogo			**41,879,167**

2017/2018	Broad Mind Company Ltd	02033, 02036.	20,650,000
	Misufini Stationery Centre	3158, 3369, 4331	1,794,000
	Nassor Said Nassor	432, 0092, 0261, 0373, na 0397	7,145,780
	Khamis Sultan Said	26, 29, 30,	1,510,400
	Salim Hamdan Maalim	0807, 0316, 0525	2,932,000
	Nassor Ali Abdalla	A.0130, A.0119, A.0141, A.0140, A.0129	3,040,500
	Suleiman Seif Rashid	0036	2,800,000
	Khamis Ali Makame	028, 029	2,550,000
	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 7 (Juni,2018)	Hati ya madai	3,500,000
	Malipo ya Wafanyakazi bora 5 (Juni, 2019)		2,750,000
	Malipo ya Posho uchimbaji – Ngomeni	Hati ya madai	1,500,000
Jumla ndogo			**50,172,680**
2018/2019	Suleiman Seif Rashid	0418, 0443, 0181, 0187, 0362	8,815,000
	Rashid Mohd Soud	119, 134	920,000
	Salim Hamdan Maalim	0666, 0675, 0682, 0825	3,775,500
	Misufini Stationery Centre	4671, 4533, 4852.	2,430,000
	Nourbhai Auto Services	2166, 2167, 2168, 2165	6,555,000
	Nassor Ali Abdalla	A.0157, A.0158, A.0160, A.0166, A.0171, A.0177, A.0176	5,466,000
	Kikwajuni Zanzibar Solar	0055	2,100,000
	Khamis Ali Makame	051, 049.	2,098,000
	Issa Sarhan Said	063, 064, 065	3,080,000
	Nassor Said Nassor	0041	1,044,300
	Rahisi Auto Spares	0048, 0051, 0089, 0117	3,009,000
	Ali Mohd Mvinja	0020, 0021.	1,410,000
	Efficient Plumbers	0750, 0806, 0305	7,794,300
	Suleiman Nassor Suleiman	0027	1,500,000
	Ali Sarahani Said	0010	746,000
	Juma Faki Salim	0033	487,104
	Malipo ya kuwaaga Wastaafu 12 (Juni, 2019)	Hati za madai	6,000,000
	Deni posho la likizo (Julai, 2018 – Juni, 2019)	Hati za madai	12,940,000
	Deni la Walimu wa chuo (Julai, 2018 – Juni, 2019)	Hati za madai	2,656,000
	Malipo ya wafanyakazi bora 5 (Juni, 2019)	Hati za madai	2,750,000
Jumla ndogo			**75,576,202**

2019/2020	Nassor Ali Abdulla	A.0181	2,376,000
	Omar Hamad Kombo	0130	1,242,000
	MUUMU PEMBA	P.AB.93/484/01/23	360,000
	Ali Mohd Mvinja	0041, 0043, 0044, 0053	4,445,000
	Suleiman Nassor Suleiman	30	8,500,000
	Ali Sarhan Said	0015	649,000
	Khamis Sultan Said	0054, 0053.	1,610,000
	Rahisi Auto Spares	338, 405.	1,899,210
	Nassor Said Nassor	302	141,600
	Malipo ya kuwaaga wastaafu 5 (Juni, 2020)	Hati za madai	2,500,000
	Deni posho la likizo (Julai, 2019 – Juni, 2020)	Hati za madai	5,520,000
	Deni posho (Aprili, 2020 – Juni, 2020)	Hati za madai	2,340,000
	Deni la Walimu wa Chuo (Julai, 2019 – Juni, 2020)	Hati za madai	3,112,000
Jumla ndogo			**34,694,810**
Jumla			**276,118,668**

3.15.8 Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa shilingi 37,163,447.44

Jumla ya shilingi 37,163,447.44 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Maji – Pemba kwa wafanyabiashara tofauti. Ukaguzi umebaini kwamba wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ili kuweza kufanya biashara na taasisi za serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli nambari 73: Malipo kwa wafanya biashara ambao hawakusajiliwa

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	11/12 17/12/19	000852	4,146,750	Suleiman Nassor Suleiman	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo ya kazi ya uchimbaji kisima cha maji safi na salama eneo la Pagali Chake Chake – Pemba.
2.	1/1 7/1/20	T.O	7,075,600	Midodoni Hardware	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya maji safi

3.	1/3 26/3/19	000858	120,861.44	Juma Faki Salim	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mbao kwa ajili ya ukarabati kibanda cha Amani road.
4.	1/6 5/6/20	000862	11,979,500	Suleiman Nassor Suleiman	Malipo ya fedha kwa ajili ya uchimbaji wa kisima eneo la Chamanangwe
5.	2/6 5/6/20	000863	13,840,736	Suleiman Nassor Suleiman	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa pipe za UPVC na changarawe kwa ajili ya uchimbaji wa kisima cha Chamanangwe.
Jumla			**37,163,447.44**		

3.15.9 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato shilingi 6,866,873,986.55

Mamlaka ya Maji – Pemba (ZAWA) ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 6,866,873,986.55 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imeweza kukusanya jumla ya shilingi 991,096,969.88 sawa na asilimia 14.43 ya makadirio ambapo hali hii inaonyesha Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la makusanyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 32(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

3.15.10 Madeni ya huduma ya maji ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu shilingi 16,007,884,152.98

Katika ukaguzi ulifanyika imebaika uwepo wa madeni ya maji yenye jumla ya shilingi 16,007,884,152.98 ambayo yanadaiwa na Mamlaka ya Maji – Pemba kwa Taasisi za Serikali, Wafanya biashara na watu binafsi ambapo madeni hayo ni muda mrefu. Aidha uongozi wa Mamlaka ya Maji - Pemba umeshindwa kuchukua hatua zinazostahiki kwa wadai husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar namba 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 73: Madeni maji ambayo hayajalipwa kwa muda mrefu

Namba	Wilaya	Aina ya mteja	Idadi ya wanaodaiwa	Fedha zinazodaiwa (Shs)
1	CHAKE CHAKE	DOMESTIC	17,920	5,390,385,282.78
		INSTITUTION	393	564,224,667.15
		COMMERCIAL	144	135,498,213.58
		AGRICULTURE	42	37,505,502.76
	Jumla ndogo		**18,499**	**6,127,613,666.27**
2	WETE	DOMESTIC	15,377	4,140,032,322.05
		INSTITUTION	230	283,330,179.58
		COMMERCIAL	85	112,570,286.97
		AGRICULTURE	25	6,948,914.48
	Jumla ndogo		**15,717**	**4,542,881,703.08**
3	MKOANI	DOMESTIC	10,297	3,138,630,255.16
		INSTITUTION	234	259,365,569.62
		COMMERCIAL	48	88,753,470.00
		AGRICULTURE	13	3,023,188,90
	Jumla ndogo		**10,592**	**3,489,772,483**
4	MICHEWENI	DOMESTIC	5,892	1,491,077,570.81
		INSTITUTION	194	253,044,047.28
		COMMERCIAL	46	99,683,693.95
		AGRICULTURE	4	3,810,987.91
	Jumla ndogo		**6,136**	**1,847,616,299.95**
	Jumla Kuu		**50,944**	**16,007,884,152.98**

Maoni ya Ukaguzi

Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Maji Zanzbar imepata hati yenye shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.16 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Taarifa ya Mapato

Mapato ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 16,424,630,000 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 16,734,169,912 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni ongezeko la shilingi 309,539,912 sawa na asilimia 1.8.

Taarifa ya Matumizi

Matumizi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar yameonekana kuongezeka kutoka shilingi 13,554,813,036 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 14,008,586,980 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na ongezeko la shilingi 453,773,944 sawa na asilimia 3.35.

Hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha 2019/2020

Taarifa ya Utendaji wa Kifedha

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini kwamba utendaji wa kifedha wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar umeimarika kwa kutoa huduma na kuongezeka kwa ufanisi katika utendaji wa shughuli zake. Kutokana na taarifa za kihesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi imebainika kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar inaendelea kupata faida.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ilipata faida ya shilingi 2,725,582,932. Hata hivyo faida ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imeonekana kupungua kutoka shilingi 2,869,816,964 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi 2,725,582,932 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kukiwa na upungufu wa shilingi 144,234,032 sawa na asilimia 5.

Upungufu huo wa faida unatokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji. Ukaguzi unashauri kwamba jitihada za ukusanyaji wa mapato ziendelee kuchukuliwa pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA) - PEMBA

3.16.1 Vifaa ambayo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 615,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 615,000 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunza vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 74: Vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
12/1 31/12/'19	183	490,000	ZURA	Air cleaner 4pcs, Bearing 2 pcs, Battery 1pc, Plug 1pc, Coil ya nje 1pc, Coil ya ndani 1pc, Locks 1 pc, Seat cover 1 set
6/3 2/3/'20	183	125,000	ZURA	Air cleaner, Oil, hydrolic shokup, fore disk, roller, bolt and service charge
Jumla		**615,000**		

3.16.2 Malipo yaliyofanywa kwa fedha taslim shilingi 1,205,000

Jumla ya shilingi 1,205,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati. Ukaguzi umebaini kuwa malipo hayo yamefanywa kwa njia ya fedha taslim ambapo ni kinyume na taratibu za malipo.

Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 75: Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslim

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
07/08 05/08/2019	152	715,000	ZURA	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya moto
12/1 31/12/2019	183	490,000	ZURA	Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vyombo vya moto
Jumla		**1,205,000**		

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.17 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

Taarifa ya Mapato

Ukaguzi umefanya uchambuzi wa ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na kubaini mapato hayo yameongezeka hadi kufikia 17,372,432,528.56 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 14,542,276,472.72 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,830,156,055.84 sawa na asilimia 16.29.

Taarifa ya Matumizi

Ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji ziliongezeka hadi kufikia shilingi 17,947,277,332 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 17,539,920,118.14 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni ongezeko la shilingi 407,357,213.86 sawa na asilimia 2.3.

Ufanisi katika Uendeshaji wa ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (Operating Performance)

Ukaguzi ulifanya tathmini ya utendaji wa Shirika kwa kupima ufanisi katika shughuli za uendeshaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kuangalia taarifa za fedha kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2019/2020

katika taarifa za mapato za Mamlaka ya Viwanja vya ndege imebainika mapato hayo yameongezeka hadi kufikia 17,372,432,528.56 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ukilinganisha na shilingi 14,542,276,472.72 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kukiwa na ongezeko la shilingi 2,830,156,055.84 sawa na asilimia 16.29 ya ongezeko.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama za uendeshaji zimepungua hadi kufikia shilingi 11,464,827,380.50 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pasi na kujuimuisha hasara iliyopatikana kutokana na tathmini ya mali za kudumu za Mamlaka ukilinganisha na shilingi 17,539,920,118.14 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ni pungufu ya shilingi 6,075,092,736.79.

Aidha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imeendelea kujiendesha kwa hasara na kufikia kiasi cha shilingi 46,620,728,123 ukilinganisha na hasara ya shilingi 2,997,643,645.4 ya mwaka wa fedha ulioishia Juni 2019.

Ukaguzi umebaini kuwa hasara ya shilingi 46,620,728,123 imeripotiwa kimakosa katika hesabu za fedha zinazoishia Juni 2020 kutokana na makosa katika utiaji thamani wa majengo ya Mamlaka.

Kutokana na tathmini iliyobainika hapo juu, ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato sambamba na kuibua

vyanzo vipya vya mapato ili kufikia dhana na malengo ya uanzishwaji wa Mamlaka hiyo.

Ufanisi katika Utendaji wa Kifedha (Financial Performance)

Katika kupima ufanisi wa utendaji katika masuala ya kifedha, ukaguzi umeangalia mlinganisho wa msimamo wa mtaji (Position of Working Capital) wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa muda wa miaka miwili kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Maelezo	30/06/2020	30/06/2019
Mali za muda mfupi	2,832,408,503.13	3,618,474,916.73
Madeni ya muda mfupi	4,050,897,418.64	2,541,226,367.65
Mali Halisi za muda mfupi	(1,218,488,915.51)	1,077,248,549.08
Uwiano		
Mali za muda mfupi/ Madeni ya muda mfupi	2,832,408,503.13 4,050,897,418.64	3,618,474,916.73 2,541,226,367.65
Uwiano	0.69:1	1.4:1
Uwiano	2:1	2:1

Kutokana na jadweli linaloonekana hapo juu imebainika uwiano kati ya mali za muda mfupi na madeni ya muda mfupi (jumla ya mali za muda mfupi/jumla ya madeni ya muda mfupi) umepungua na kufikia 0.69:1 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020 kutoka 1.4:1 kwa mwaka ulioshia juni 2019 kama inavyoainishwa kwenye Jedwali hapo juu. Uwiano huu unaonesha kwamba Mamlaka inaweza kushindwa kulipa madeni yake ya muda mfupi katika kipindi cha miezi 12 ijayo.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.17.1 Kukosekana kwa mikataba ya ukusanyaji wa mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Viwanja vya ndege imeingia mikataba na watoaji huduma mbali mbali kwa lengo la kutoa huduma hizo na Mamlaka kupata mapato kupitia huduma hizo. Kutokana na mikataba ya makubaliano yao imebainika kukosekana kwa mapato yatokanayo na kodi pamoja na ada mbali mbali za viwanja vya ndege.

Ukaguzi haukuweza kupatiwa mikataba hiyo pamoja na jitihada mbali mbali zilizochukuliwa za kuitaka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuwasilisha mikataba hiyo kwa ajili ya ukaguzi.

Kushindwa kuwasilisha makubaliano ya mikataba iliyofungwa baina ya Mamlaka na watoa huduma hao, kumepelekea kutokujiridhisha juu ya usahihi wa mikataba hiyo, kima kinachopaswa kutozwa na kukusanywa, muda wa kuanza na kumalizika kwa makubaliano hayo na thamani halisi ya fedha inayopaswa kukusanywa kupitia mikataba hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji Sheria namba 11 ya mwaka 2016.

Jadweli Nambari 76 : Watoa huduma wanaolipwa bila ya mikataba

Nambari	Watoa huduma waliopatiwa mikataba	Maelezo
1	Arkia Israel – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
2	Neos Spa – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
3	Isra Air – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
4	Kenya Air Ways – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
5	Precision Air – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
6	Blue Panorama – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
7	Enter – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
8	Tui Fly- Belgium - Rent	Kukosekana kwa Mkataba
9	Tui Fly- Netherland – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
10	Travel Service-Tvs 3z – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
11	Travel Service-Tvs Qs – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
12	Polish Air – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
13	Air Itally/Meridiana Fly – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
14	Rossiya Air – Rent	Kukosekana kwa Mkataba
15	Smart Wings – Rent	Kukosekana kwa Mkataba

3.17.2 Kutowasilishwa mikato ya kodi na michango ya ZSSF ya wafanyakazi kwa wakati shilingi 639,932,727

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetayarisha malipo ya mishahara ya wafanyakazi wake kwa mwezi unaoishia tarehe 30 Juni, 2020. Mamlaka ilifanya zuio la makato ya wafanyakazi wake yanayokatwa kutoka katika mishahara yao kwa lengo la kulipiwa kodi pamoja na michango ya mfuko wa hifadhi ya Jamii.

Ukaguzi umebaini dosari ya malipo hayo kutokulipwa kwa wakati, jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 7 na kifungu nambari 81 cha Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 pamoja na kifungu nambari 9(1)(a-c) cha sheria nambari 2 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF).

Hadi ukaguzi unakamilika makato hayo ya kodi pamoja na michango ya wafanyakazi kwa mfuko wa Hifadhi ya Jamii hayakuwasilishwa kwa taasisi husika. Kushindwa kulipa michango hiyo kwa wakati kutapelekea Mamlaka ya Viwanja vya ndege kulazimika kulipa malipo ya adhabu ya kutowasilisha kodi pamoja na michango ya wafanyakazi kwa Mfuko wa ZSSF. Mchanganuo wa mikato hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 77: Fedha za mikato ya kodi kwa wafanyakazi

Namba	Mwezi	Kodi iliyo paswa kulipwa PAYE (Shs)	Tarehe ya mwishoya kuwasilisha kisheria
1.	Julai 2019	32,240,656	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
2.	Agosti 2019	32,240,656	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
3.	Septemba 2019	32,100,890	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
4.	Oktoba 2019	32,244,228	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
5.	Novemba 2019	39,007,542	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
6.	Disemba 2019	38,837,065	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
7.	Januari 2020	38,495,290	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
8.	Febuari 2020	Haikupatikana	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
9.	Machi 2020	38,478,840	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
10.	Aprili 2020	38,488,740	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
11.	Mei 2020	38,456,169	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
12.	Juni 2020	38,394,951	Ndani ya siku saba za mwezi unaofuata
Jumla		**398,985,027**	

Jadweli Nambari 78: Mikato ya fedha za ZSSF kwa wafanyakazi

Namba	Mwezi	Mchango uliopaswa kuwasilishwa (Shs)	Tarehe ya kuwasilisha
1.	Julai 2019	20,152,300	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
2.	Agosti 2019	20,152,300	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
3.	Septemba 2019	20,761,580	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
4.	Oktoba 2019	20,832,490	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
5.	Novemba 2019	22,854,125	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
6.	Disemba 2019	22,810,445	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
7.	Januari 2020	22,735,930	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
8.	Febuari 2020	Haikupatikana	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
9.	Machi 2020	22,706,635	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
10.	Aprili 2020	22,632,855	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
11.	Mei 2020	22,676,185	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
12.	Juni 2020	22,632,855	Ndani ya siku 15 za mwezi unaofuata
Jumla		**240,947,700**	

3.17.3 Kukosekana kwa nyaraka za uthibitisho wa mapokezi ya bidhaa zenye thamani ya shilingi 251,935,641.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetumia jumla ya shilingi 251,935,641 kuwalipa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa zinazotumiwa na Mamlaka. Dosari iliyobainika na wakaguzi ni kutokupatika kwa uthibitisho wa nyaraka (GRN) za upokeaji wa bidhaa hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Kutokuwepo kwa nyaraka za uthibitisho wa mapokezi ya vifaa kumetokana na uwepo wa mazingira dhaifu ya udhibiti yaliyotajwa hapo juu yanaweza kutoa fursa ya udanganyifu.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka kuchukuwa hatua zinazofaa ili kuboresha mazingira yake ya udhibiti wa ndani wa mali za taasisi.Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 79: Malipo kwa ajili ya ununzi wa bidhaa mbali mbali

Namba	Tarehe	Nambari ya hati ya Malipo	Jina la Msambazi	Jumla ya fedha (Shs)	Maelezo
1	15/02/2020	73/2	Chituli Electrical Material	19,250,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme wa jua
2	2/3/2020	20/3	Chituli Electrical Material	11,550,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme wa jua
3	16/03/2020	101/04	Said Abdalla Ali	12,651,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme katika vituo vilivyotengwa kwa ajili ya wagonjwa wa korona
4	19/03/2020	116/03	Chituli Electrical Material	15,400,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa umeme wa jua katika eneo la kuwekea magari
5	9/7/2019	54/8	Davot Company Ltd	16,887,641	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa UPS na Stabalizer
6	6/11/2019	42/11	Mohasha General Supply	10,700,000	Ikiwa ni malipo ya awali kwa ununuzi wa mashine ya kupigia matofali
7	5/1/2020	36/1	Cm Electrical Power	25,628,000	Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa taa kwa ajili ya MDBS

8	30/06/2020	Jun-20	Seven Star Enterprises	16,500,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ID's kwa wafanyakazi
9	7/8/2019	43/8	Almas Faiz Abeid	14,000,000	Ikiwa ni malipo ya awali kwa ununuzi wa mkasi wa kukatia majani
10	30/06/2020	Jun-20	Almas Faiz Abeid	11,200,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa maringi ya gari la Zimamoto
11	26/04/2020	107/4	Bin Nyange Shop	9,280,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi za ZAAT na kituo cha Polisi kilichopo Uwanja wa Ndege
12	26/04/2020	123/4	Bin Nyange Shop	8,725,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kukarabati Jiko la Mamlaka ya Viwanja vya Ndege
13	9/7/2019	54/7	Bin Nyange Shop	11,930,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya utengenezaji wa Paa la sehemu ya Mizigo
14	12/7/2019	65/7	Wazalendo Company Ltd	8,205,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matengenezo ya choo
15	2/2/2020	2/12	Mohasha General Supply	28,700,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa T-shirt, Kofia, Peni na Toys za Ndege
16	28/02/2020	198/2	Mohasha General Supply	31,329,000	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya manunuzi ya T-shirt kwa ajili ya ufunguzi wa Uwanja wa Ndege Kigunda
Jumla				**251,935,641**	

3.17.4 Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka Shilingi 46,620,728,123

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Mamlaka na kubaini kufanyika kwa makosa katika tathmini ya majengo ya Mamlaka ambapo thamani yake iliporomoka kutoka shilingi 52,633,008,901 mpaka kufikia shilingi 7,347,669,639 kwa mujibu wa ripoti ya mtathmini wa mali.

Aidha ukaguzi ulifuatilia kwa kina mabadiko hayo ya utiaji thamani na kubaini kwamba thamani ya jengo ya awali ilikuwa ni shilingi 52,633,008,901 baada ya kutoa gharama za uchakavu ambayo pia ilikuwa na makosa kwa kujumuisha mali za kudumu nyengine zisizohusiana na jengo na kupelekea makosa katika kufananisha vitu viwili visivyo fanana.

Makosa hayo kwa kiwango kikubwa yamepelekea uwepo wa hasara inayotoka na kushuka kwa thamani kwa jengo na kuzifanya hesabu za Mamlaka kutokuonesha sura halisi na sahihi.

Ukaguzi unapendekeza kwa Uongozi wa Mamlaka ya Uwanja wa ndege kuweka vizuri taarifa za mali za kudumu za Mamlaka kwa kuzingatia thamani halisi ya mali za kudumu za Mamlaka.

3.17.5 Kukosekana kwa mikataba ya ujenzi na utoaji huduma yenye thamani ya shilingi 382,649,624

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanya malipo ya jumla ya shilingi 125,531,200 kwa ajili ya kumlipa mkandarasi Ockra Construction Company Ltd kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kushukia na kurukia ndege (Airstrip) ya Uwanja mdogo wa ndege uliopo Nungwi (Kigunda).

Hadi ukaguzi unakamilika imebainika malipo ya fedha kufanyika bila ya kuwepo kwa mkataba uliosainiwa kwa ajili ya ujenzi huo.

Aidha, ukaguzi umebaini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanya malipo ya jumla ya shilingi 257,118,424 kwa ajili ya kumlipa "Mohasha General Supplier" mtoa huduma za usambazaji wa vifaa na vitu mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka bila ya kuwepo kwa mkataba uliosainiwa kwa ajili ya usambazaji wa vifaa hivyo.

Kufanyika kwa matumizi ya fedha bila ya kuwepo kwa makubaliano ya mikataba kunapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo ya fedha hizo ikiwa yamezingatia makubaliano ya pande mbili za mkataba. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE - PEMBA

3.17.6 Kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato shilingi 618,378,900

Jumla ya shilingi 618,378,900 zilikadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ukaguzi umebaini kwamba makadirio haya ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2020, jumla ya shilingi 324,089,485 zilikusanywa sawa na asilimia 52.4 ya makadirio ambapo hali hii inaonyesha Mamlaka imeshindwa kufikia lengo la makusanyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016

3.17.7 Kukosekana kwa uthibitisho wa uletwaji wa vitabu vya kukusanyia mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba inapaswa kukushanya mapato katika maeneo ya Mamlaka kwa mujibu wa sheria. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka inapokea vitabu vya mapato kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Zanzibar bila ya kuwepo kwa uthibitisho wa uletwaji na mapokezi wa vitabu hivyo, aidha ukaguzi umeshindwa kujuwa jumla ya vitabu halisi vya mapato vilivyopokelewa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

3.17.8 Mamlaka kushindwa kukusanya mapato ya shilingi 65,609,020

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba hutoa huduma kwa kampuni mbali mbali za ndege ambapo hulazimika kukusanya mapato kutoka kwa kampuni hizo. Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka imeshindwa kukusanya jumla ya shilingi 65,609,020 kutoka kwa kampuni za ndege mbali mbali ambazo zilipatiwa huduma katika uwanja wa ndege wa Pemba.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 80: Fedha za mapato ambazo hazikupatikana

Namba	Mtoa huduma	Jumla ya fedha (Shs)
1.	Assa laam Air	47,804,380
2.	Zan Air	10,785,440
3.	Coastal Travel	7,019,200
Jumla		**65,609,020**

3.17.9 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 130,542,607

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba huingia katika makubaliano ya ununuzi wa bidhaa na huduma mbali mbali kutoka kwa wafanyabiashara tofauti na Taasisi za Serikali kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba inadaiwa na wafanyabiashara na Taasisi za Serikali jumla ya shilingi 130,542,607 kutokana na kupatiwa bidhaa na huduma mbali mbali. Aidha madeni haya ni ya muda mrefu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 81: Madeni ya muda mrefu

Namba	Jina la mdai	Fedha anazodai (Shs)
1.	AKB Cleaning Enterprises	15,200,000
2.	RK General Supplier	25,000,000
3.	Nassor Said Nassor	15,481,000
4.	Fatah Moh'd Ali	5,000,000
5.	Rashid M. Soud	22,573,000
6.	Mbarouk Salim Ali	5,263,980
7.	Adem Store	3,268,000
8.	Asaa Kheri Asaa	1,495,070
9.	Misufini Stationary	4,562,000
10.	Juma Enterprises	907,500
11.	Ali Sarhan	362,500
12.	Rahisi Auto Spares	826,000
13.	ZECO	7,752,775
14.	ZAWA	22,850,782
Jumla		**130,542,607**

3.17.10 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 95,636,945

Jumla ya shilingi 95,636,945 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba kutokuambatanishwa kwa baadhi ya vielelezo vya matumizi katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 82: Malipo yaliyokosa vielelezo

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	03/7 08/7/2019	001555	590,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya fedha za nauli na posho la kujikimu kwa ajili ya safari kikazi Unguja.
2.	8/7 08/7/2019	001555	560,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya marejesho ya nauli pamoja na posho la kujikimu anazolipwa Muhasibu kwa ajili ya safari kikazi Unguja
3.	13/7 08/7/2019	001560	887,000	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji vinavyotumika katika miundombinu ya maji katika uwanja wa ndege.

4.	16/7 10/7/2019	001563	600,000	Sheby Enterprises	Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo na ufungaj wa vifaa vya taa za sola maeneo ya uwanja wa ndege.
5.	35/7 19/7/2019	001573	4,000,000	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya awamu mwanzo kwa ajili ya matengenezo ya nyumba ya wafanyakazi (ZAA Hospitality Inn) flat 3.
6.	38/7 25/7/2019	001577	6,000,000	RK General Traders Co. Ltd	Malipo ya awamu ya mwanzo ya ukarabati wa ukumbi wa mkutano, jiko pamoja na vyoo.
7.	43/7 25/7/2019	001578	475,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya nauli pamoja na posho la kujikimu analolipwa meneja kwa ajili ya safari kikazi Unguja.
8.	01/8 05/7/2019	001578	1,794,500	Kikosi Cha Zimamoto na Uokozi	Malipo ya fedha ya harama za ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto maeneo ya uwanja wa ndege Pemba.
9.	02/8 05/8/2019	001580	10,000,000	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya awamu ya pili na ya mwisho kwa ajili ya matengenezo ya nyumba ya wafanyakazi
10.	03/8 05/8/2019	001581	1,000,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya awamu ya tatu na ya mwisho anazolipwa Mwenyekiti wa kikundi kwa ajili ya uchimbaji na ufukiaji wa msingi uliotumika kwa uwekaji wa miundombinu ya taa za barabarani.
11.	05/8 07/8/2019	001582	1,500,000	ZMOTION STUDIO	Malipo ya gharama za utayarishaji wa igizo fupi na matangazo ya barabarani kwa ajili ya sherehe za maadhimisho ya miaka nane ya mamlaka ya viwanja vya ndege.
12.	07/8 06/08/2019	001584	1,885,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya shughuli za usafishaji katika maeneo mbali mbali ya kiwanja cha ndege uliofanywa na kikundi cha mashujaa cha Mgogoni Chake Chake
13.	08/8 09/8/2019	001585	2,500,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo kwa ajili ya shughuli za usafishaji katika maeneo mbali mbali ya kiwanja cha ndege uliofanywa na kikundi cha Nguvu kazi cha Mfikiwa Chake Chake Pemba.
14.	10/8 06/8/2019	001587	420,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya posho la kujikimu analolipwa Captain Said I. Ndumbogani (Mkurugenzi Mkuu) kwa ajili ya safari kikazi Uwanja wa ndege Pemba.

15.	18/8 09/8/2019	001592	800,000	Salim Abdalla Seif	Malipo ya fedha kwa kikundi cha sanaa ya maigizo kilichotumbwiza katika sherehe za kilele cha maadhimisho ya Mamlaka day.
16.	16/8 09/8/2019	001590	1,020,000	Awali Mussa Msafir	Malipo ya fedha kwa ajili ya upambaji wa mashamiana na maeneo ya sherehe katika kilele cha maadhimisho ya Mamlaka day.
17.	19/8 07/8/2019	001593	400,000	BAI SIGN WRITER	Malipo ya fedha kwa ajili ya utengenezaji wa mabango ya matangazo ya kilele cha maadhimisho ya miaka 8 ya mamlaka ya viwanja vya ndege.
18.	23/8 13/8/2019	001597	2,167,965	ZECO	Malipo ya fedha za gharama za ubadilishaji wa line ya umeme kutoka single phase kwenda three phase katika nyumba ya ZAA Hospitality Inn.
19.	41/8 20/8/2019	001603	620,000	M/V/Ndege Pemba	Malipo ya fedha za gharama za vyakula na viburudishaji vilivyotumika kwa wafanyakazi wa kitengo cha AVSEC.
Jumla			**37,219,465**		

3.17.10 Vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani shilingi 16,524,383

Jumla ya shilingi 16,524,383 zimelipwa kwa ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege – Pemba

Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari la kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 83: Vifaa ambavyo havikurikodiwa ghalani

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Fedha zilizolipwa (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	34/7 18/7/2019	001572	936,000	Asaa Kheri Asaa	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi
2.	15/8 09/8/2019	001589	436,500	Rahisi Auto Spares	Ununuzi wa vifaa vya trekta SMZ 129 D
3.	04/10 2/10/2019	001638	1,552,000	Suleiman Seif Rashid	Ununuzi wa vifaa vya usafi

4.	7/11 8/11/2019	001681	2,091,320	MARO MASTER ALLUMINIUM	Matengenezo ya partition ya Alminium inayotumika katika ukumbi wa VIP No 2.
5.	2/12 02/12/2019	001694	1,114,000	Zanzibar Petroleum ltd	Ununuzi wa mafuta
6.	42/1 24/1/2020	001753	308,945	Quick-win computer repair	Matengenezo ya mashine
7.	33/1 23/1/2020	001748	1,450,400	Rahisi Auto spares	Ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya trekta SMZ 129B
8.	41/1 24/1/2020	001752	266,168	Electrotherminal supplies and services	Ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya vipoza joto
9.	24/2 12/2/2020	001769	1,427,185	Adem store	Ununuzi wa kioo cha bus SMZ 127 A
10.	16/2 11/2/2020	001761	1,284,466	Misufini Statinaries	Ununuzi wa vifaa vya kuandikia
11.	18/2 11/2/2020	001763	2,000,000	Rahisi Auto spares	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi (capstones)
12.	4/5 07/05/2020	001819	2,012,330	Misufini stastionary	Ununuzi wa vifaa vya stationary.
13.	32/5 20/05/2020	01838	570,874	Adult Training center	Malipo ya fedha za ununuzi wa HDD – 4TB kwa matumizi ya CCTV
14.	33/5 22/05/2020	001839	551,845	Salim Hamdan Maalim	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi
15.	13/6 15/6/2020	001847	522,350	Rashid M. Soud	Ununuzi wa vifaa vya magari
Jumla			**16,524,383**		

3.17.12 Malipo ya fedha kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa shilingi 74,525,422

Jumla ya shilingi 74,525,422 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba kwa wafanyabiashara tofauti. Ukaguzi umebaini kwamba wafanyabiashara hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar ili kuweza kufanya biashara na taasisi za Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 6.**

Maoni ya Ukaguzi

Hati Isiyoridhisha

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Viwanja vya NdegeZanzibarkwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonyesha sura sahihi na halisi isipokua kwa mambo yaliyoainishwa hapo juu kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imepata hati isiyoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.18 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 4,345,593,300 katika kipindi cha fedha 2019/2020 ikijumuisha vyanzo vya ndani vya mapato, ruzuku pamoja na fedha kutoka kwa washirika wa Maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ilikusanya jumla ya shilingi 2,461,169,334 sawa na asilimia 56.66 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,104,865,652 kwa kazi za kawaida na jumla ya shilingi 8,347,500 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imetumia jumla ya shilingi 2,417,720,871 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 77.86 ya makadirio, na shilingi 47,416,120 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 568 ya makadirio.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WAMAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR

Katika utendaji wa kifedha wa Mamlaka (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinachoonesha namna Mamlaka inavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa biashara na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji imebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa "Accrual basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash basis" jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa Mamlaka kifaida au hasara.

Ukaguzi unashauri Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.18.1 Kamati ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016 inamtaka Afisa Mhasibu kuanzisha Kamati ya ukaguzi kwa ajili ya kutathmini udhibiti wa ndani wa Mamlaka husika. Ukaguzi umebaini Mamlaka haijaanzisha Kamati hiyo jambo ambalo linapelekea kukosa maoni na ushauri juu ya taarifa zinazotolewa na mkaguzi wa hesabu za ndani na mkaguzi wa hesabu za nje.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

3.18.2 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu shilingi 46,938,994

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza "Kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi chini ya sheria hii".

Ukaguzi umebaini Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi, kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo. Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuikosesha serikali mapato yanayotokana na kodi ya thamani na ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama unavyoonekana hapo chini:-

Jadweli Nambari 84: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa

Namba	Tarehe	Aliyelipwa	Thamani (Shs)	Maelezo
1	20-Sep-19	ZANLINK	2,018,898	Ikiwa ni malipo ya huduma za internet kwa matumizi ya ofisini
2	12-May-20	ZANLINK	1,087,275	Ikiwa ni malipo ya usajili wa mtandao kampuni ya ZANLINK LTD
3	3-Jun-20	ZANLINK	1,957,095	Ikiwa ni malipo ya huduma za internet kwa matumizi ya ofisini kwa mwezi ya Juni 2020
4	2-Sep-19	EL NABHANY MOBILE	1,070,359	Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa vya gari No SMZ 331A

5	12-May-20	Zanzibar Trade & Investment Co Ltd	6,073,738	Ikiwa ni ununuzi na ufanyaji wa service kwa A/C za ofisi na za Fridge za ofisi za Mamlaka
6	29-Apr-20	MK Alliminium Company Limited	1,244,600	Ikiwa ni malipo ya utengenezaji wa milango minne ya vyoo ya ofisi ndogo ya Mamlaka iliopo Amani
7	30-Jun-20	MK Alliminium Company Limited	2,414,720	Ikiwa ni utengenezaji wa file shelf kwa ajili ya ofisi ya maktaba
8	10-Jun-20	MK Alliminium Company Limited	3,192,136	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uwekaji wa makabati katika baadhi ya ofisi za Maruhubi
9	30-Jun-20	Classic Computer Technology	327,957	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya utiaji wa Ant Virus kwa computer za ZIPA
10	25-Jun-20	Classic Computer Technology	5,725,340	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuzifanyia services Computa za Ofisi
11	10-Jun-20	New Zanzibar Motors	8,087,378	Ikiwa ni ununuzi wa bajaj kwa ajili ya matumizi ya ofisi
12	10-Jun-20	Bab Plumbing & Water works	4,494,175	Ikiwa ni malipo ya uchimbaji kisima kwa ajili ya ofisi ya Maruhubi
13	10-Jun-20	Masomo Bookshop Ltd	652,823	Ikiwa ni unuzi wa magazeti kuazia mwezi wa January-June 2020
14	1-Mar-20	Majid Store	2,842,000	Ikiwa ni malipo kwa ununuzi wa vifaa kwa ajili ya walinzi wa mamlaka
15	29-Apr-20	Saleh Decoration	5,750,500	Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa zulia na gharama na utiaji kwa ofisi ya Maruhubi
Jumla			**46,938,994**	

3.18.3 Madeni ya muda mrefu USD 1,053,995

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Mamlaka kujiendesha kiufanisi. Aidha kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa Mamlaka na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali.

Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.

Ukaguzi unashauri Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji, kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana kwenye majadweli yafuatayo:-

a) Miradi iliyokuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu lakini ina madeni makubwa yenye thamani ya dola za kimarekani 418,390 sawa na shilingi 969,982,405.9 kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo.

Jadweli Nambari 85: Miradi iliyokuwa haifanyi kazi kwa muda mrefu

Namba	Jina la Mdaiwa	Fedha zinazodaiwa (USD)
1	Almahra Processing	48,375
2	Asaalam	42,000
3	Autozone (LTD)	10,570
4	Blue Horizon	172,577
5	Breik Motor	10,720
6	City Motor	2,880
7	Flemingo International Ltd	7,695
8	Hakuna Matata Used Car	5,460
9	HLS Management	25,000
10	ISSZAI Motor	11,200
11	Marcopolo	2,690
12	MD Motor	3,280
13	SM Motor	2,522
14	Success Motors	13,890
15	Supershine	3,300
16	SWABI Motor	8,260
17	Visiwani Motors	18,300
18	ZAREC	29,671
Jumla		**418,390**

b) Miradi ambayo imedhaminiwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ambapo tangu kuanzishwa kwake hakukuwa na malipo yoyote yaliyofanywa na hadi kufikia tarehe 30 Juni,2020 madeni hayo yamefikia jumla ya dola za kimarekani 462,207 ambazo sawa na shilingi 1,071,566,380.38 kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 86: Miradi ambayo imedhaminiwa na Serikali

Namba	Jina la Mdaiwa	Fedha zinazodaiwa (USD)
1	Fumba Beach Lodge	84,070
2	Malik Food	86,779
3	OZTI	51,000
4	SHAMON	71,626

5	Zan Bottling	60,740
6	Zanzibar Quality	107,992
Jumla		**462,207**

c) Madeni ya miradi ambayo inaendelea na shughuli za uzalishaji lakini kutokana na mwenendo wa biashara ukaguzi umebaini malipo yanayolipwa hayaridhishi na kupelekea kulimbikizika kwa madeni hayo na kufikia jumla ya dola za kimarekani 173,398 sawa na shilingi 402,000,547.86 kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli nambari 87: Madeni ya miradi inayoendelea na shughuli za uzalishaji

Namba	Jina la Mdaiwa	Fedha zinazodaiwa (USD)
1.	Mtoni Motor	12,890
2.	Relaxo Footwear (HAWAII)	7,800
3.	Royal Motors	17,291
4.	Safari Co Ltd	22,395
5.	TANTEX	13,965
6.	ZANTEL	32,018
7.	Zanzibar Fashion	27,600
8.	Zanzibar Fibre Glass	6,220
9.	Zanzibar spare parts	12,241
10.	ZANOP	3,420
11.	Zenj Motor	17,558
Jumla		**173,398**

3.18.3 Kutokutekelezwa kwa miradi ya maendeleo kwa muda mrefu

Miongoni mwa majukumu makubwa ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji (ZIPA) ni kuandaa mazingira mazuri na yaliyo salama kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuisaidia Serikali kuu kupata Mapato yanayotokana na uwekezaji huo. Ukaguzi ulitembelea baadhi ya maeneo huru ya uwekezaji kama vile "Amani Industrial Park" ili kujionea namna shughuli hizo zinazo simamiwa na Mamlaka zinavyoendelea.

Ukaguzi umebaini kuwa maeneo huru ya uwekezaji zoni ya Amani, (Amani Industrial Park) kuna miradi ya maendeleo ambayo bado hairidhishi ufanyaji wake wa kazi na mengineyo kuwa bado haijaanza kufanya kazi jambo ambalo inashindwa kusaidia maendeleo ya nchi kwa mujibu wa malengo ya Serikali. Mchanganuo wa utekelezaji wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 7.**

Kutokana na mchanganuo wa taarifa hiyo kama inavyoonekana, ukaguzi unapendekeza uwepo wa miradi kidogo ambayo itaweza kutekelezeka na kutoka tija kwa jamii kuliko kuweko kwa miradi ambayo haitekelezeki, haina ufanisi, haina tija na kukosekana kwa dhana ya uwepo wa Uwekezaji katika jamii.

Maoni ya ukaguzi

Hati Inayoridhisha Yenye Aya za Msisitizo

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonyesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi limepata Hati inayoridhisha yenye aya za msisitizo kutokana na mambo yaliyotajwa hapo juukwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.19 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA (ZPPDA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 300,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya makusanyo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imekusanya jumla ya shilingi 194,190,497.28 ambazo ni sawa na asilimia 64.73 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,857,400,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imetumia jumla ya shilingi 1,601,175,791.47 ambazo ni sawa na asilimia 86.21 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.19.1 Kutokufanya kazi kwa Kamati ya Ukaguzi

Kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016 inamtaka Afisa Mhasibu kuanzisha Kamati ya ukaguzi kwa ajili ya kutathmini udhibiti wa ndani wa Mamlaka husika.

Mamlaka imeanzisha kamati hiyo ikiwa na wajumbe wa tatu. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 ukaguzi umeshindwa kupatiwa ripoti zinazothibitisha kuwa kamati hiyo ilikaa kikao na kufanya kazi ka mujibu wa taratibu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

3.19.1 Mapato ambayo hayakuwasilishwa benki shilingi 4,900,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebaini kujitokeza kwa miamala 25 iliyorekodiwa katika daftari la fedha yenye jumla ya shilingi 4,900,000 lakini haikuonekana katika taarifa za benki (uncredited deposit) iliyokaa kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita bila ya kufutwa au kufanyiwa mabadiliko. Kutokuwasilisha mapato kwa wakati ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mapato ambayo hayakupelekwa benki ni kama inavyooneka katika jadweli lifuatalo :-

Jadweli Nambari 88: Fedha za mapato ambazo hazikuwasilishwa benki

Namba	Orodha ya Watoa Huduma	Fedha ambazo hazikupelekwa benki (Shs)
1	Tahfif Auto Works	170,000
2	Ngoto Auto Accessories	120,000
3	Adult Training Center	170,000
4	Fair Hardware	170,000
5	Seif Ali Hamad	20,000
6	Suleiman Ali Said	120,000
7	Vista Auto Parts	170,000
8	Rahisi Auto Parts	170,000
9	Azmi Transport Limited	170,000
10	Asaa Kheir Asaa	170,000
11	Chuma Constraction	370,000
12	Mums Dood and Refreshment	170,000
13	Quick Wine	170,000
14	Iddi Mohammed Salim	120,000
15	Issa Mohammed Said	120,000
16	Rashid Abraham Jabir	170,000
17	Mwitani Stationary	170,000
18	Rashid Mohd Soud	170,000
19	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	300,000
20	Mohd Ussi Makame	170,000
21	Kana Cattering Group	120,000
22	Sule and Said Building Contractors	320,000
23	Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili	360,000
24	Shirika la Bandari	360,000
25	Wizara ya Vijana	360,000
Jumla		**4,900,000**

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma (ZPPDA) imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.20 MAMLAKA YA UDHIBITI, UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI ASILI ZANZIBAR (ZPRA)

Taarifa ya Mapato

Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,325,254,000 kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya mapato.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji Mafuta na Gesi Asilia imekusanya jumla ya shilingi 2,087,901,622 ambazo nisawa na asilimia 90 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Udhibiti utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,325,254,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Udhibiti utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia imetumia jumla ya shilingi 2,727,830,618 ambazo ni sawa na asilimia 117.31 ya makadirio.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA MAMLAKA YA UDHIBITI, UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI MAFUTA NA GESI ASILI ZANZIBAR

Katika utendaji wa kifedha wa Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinacho onesha namna Mamlaka inavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa utoaji huduma na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia inatumia mfumo wa "Cash basis" mfumo ambao hauoneshi uhalisia wa taarifa za mali za kudumu pamoja na taarifa za madeni ya Taasisi katika hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka.

Ukaguzi unashauri Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.20.1 Kutokuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia bado halijaanzisha Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu (Audit Committee), ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari mbali mbali katika udhibiti wa ndani wa Mamlaka kama zifuatavyo:-

- Kutokujadili na kuidhinisha mpango mkakati wa mwaka wa ukaguzi wa ndani
- Kutokupitia taarifa za hesabu za Mamlaka.
- Kutobainisha mapungufu ya ripoti ya ukaguzi wa hesabu yaliyobainishwa na Mkaguzi wa Hesabu za Ndani na Mkaguzi wa Hesabu wa Nje kwa lengo la kuyafanyia kazi mapungufu yaliyobainika na kuishauri Mamlaka ili liweze kujiendesha kwa tija.

3.20.2 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu shilingi 78,791,332

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza "Kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi chini ya sheria hii".

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kupitia hesabu nambari 0400519000 ya matumizi ya kawaida (Reccurent Account), Mamlaka ya Udhibiti, Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asiliaimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi, kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo. Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuikosesha serikali mapato yanayotokana na kodi ya thamani na ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama unavyoonekana hapo chini:-

Jadweli Nambari 89: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa

Namba	Aliyelipwa	Nambari ya usajili (ZPPDA)	Thamani (Shs)
1	Jae Enterprises Co. Ltd, Zanzibar	Haikusajiliwa	3,439,800
2	Smart Security Zanzibar	Haikusajiliwa	16,170,000
3	Fahud Africa (T) Ltd	Haikusajiliwa	6,388,032
4	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Haikusajiliwa	52,793,500
Jumla			**78,791,332**

3.20.3 Ukiukwaji wa taratibu za Malipo shilingi 50,793,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 50,793,500 zimetumika kwa kumlipa mshauri elekezi lakini taratibu za malipo hayo hazikufuatwa na hatimae Mamlaka kuamua kufanya manunuzi kwa njia ya ukwepaji wa utangazaji wa zabuni na kumlipa mshauri mmoja mmoja (Split of tender). Aidha ukaguzi umebaini watoa huduma hao hawakukatwa kodi ya zuio ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 83(a) cha sheria ya kodi ya mwaka 2004.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi namba 11 ya mwaka 2016

Malipo yenyewe ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 90: Malipo yaliyokiukwa utaratibu wa manunuzi

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1	1/7, 7/1/2019	2,000,000	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Malipo kwa ajili uwasilishaji wa rasimu BLM
2	7/3, 15/07/2019	2,750,000	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Ikiwa ni Malipo ya fedha kwa ajili ya kuandaa proposal ya 2D Sesmic Survey
3	9/3, 5/9/2019	5,000,000	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuandaa draft announcement
4	10/9, 16/10/19	15,000,000	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Ikiwa ni Malipo kwa ajili ya uandaaji SP
5	12/7, 10/12/2019	18,000,000	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Malipo kwa ajili ya uandaaji wa SP
6	42/06, 30/06/2020	8,043,500	Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson	Malipo kwa ajili ya mafunzo ya Program ya Tender Evaluation for 2D.
Jumla		**50,793,500**		

Aidha, kutokana na mapungufu yaliyobainika Mamlaka imekuwa ikifanya malipo kwa ajili ya ushauri kutoka kwa Yona Killagane, Kelvin Komba & Hudson, ambapo ukaguzi umeshindwa kupatiwa uthibitisho wa ulipaji wa kodi kwa kukosekana nambari ya utambulisho inayotumiwa na watoa huduma hao kama ni uthibitisho wa mlipa kodi (TIN number).

Vilevile imebainika Mamlaka imekuwa ikifanya malipo kwa mshauri elekezi kupitia hesabu binafsi, hii ilidhihirisha kwamba Mshauri Elekezi huyo hakusajiliwa kama ni Taasisi inayofanya kazi ya kutoa huduma za ushauri elekezi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 133(2) cha sheria ya kodi ya mwaka 2004. Malipo hayo yalikuwa yakifanyika kupitia hesabu zifuatazo:-

Jadweli Nambari 91: Hesabu zilizotumika katika kufanya malipo

Namba	Jina la Hesabu	Nambari ya Hesabu	Jina la Benki
1	Yona Killagane	22301604511	NMB Bank, Azikiwe Street, Dar es Salaam
2	Yona Killagane	0112024994600	CRDB Bank, Azikiwe Street, Dar es Salaam
3	Willington Eniyoye Hudson	01J2025023300	CRDB Bank, Azikiwe Street, Dar es Salaam

3.20.4 Watumishi wanaokaimu nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita

Kanuni ya 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inasema kuwa, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 20(1), hakuna nafasi ya kukaimu kwa muda wa miezi kumi na mbili mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa mhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea.

Ukaguzi umebaini kwamba kuna watumishi wanakaimu nafasi mbalimbali za ukuu wa Idara kwa zaidi ya miezi 12 bila kuthibitishwa au nafasi hizo kujazwa kinyume na kanuni za Utumishi wa Umma. Watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lililopo hapo chini:-

Jadweli Nambari 92: Watumishi wanaokaimu nafasi mbali mbali

Namba	Idara	Nafasi inayokaimiwa	Muda wa kukaimu
1	Mipango Fedha na Uendeshaji	Kaimu Mkurugenzi Fedha na Uendeshaji	Zaidi ya miezi 12
2	Idara ya Afya, Usalama na Mazingira	Kaimu mkurugenzi wa Afya na Mazingira	Zaidi ya miezi 12
3	Idara ya Usimamizi na taarifa za mafuta na Gesi	Kaimu Mkurugenzi wa taarifa za mafuta na Gesi asilia.	Zaidi ya miezi 12
4	Idara ya Sheria	Kaimu Mkurugenzi Sheria	Zaidi ya miezi 12

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Udhibiti ,Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Udhibiti Utafuataji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.21 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Taarifa ya mapato

Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 4,491,804,899 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Usafiri Baharini imekusanya jumla ya shilingi 2,286,469,743 ambazo sawa na asilimia 51 ya makadirio.

Taarifa ya matumizi

Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,577,364,860 kwa matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Usafiri Baharini imetumia jumla ya shilingi 2,312,192,538 ambazo sawa na asilimia 51 ya makadirio.

UFANISI KATIKA UTENDAJI WA MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI

Katika utendaji wa kifedha wa Mamlaka ya Usafiri Baharini (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinacho onesha namna Mamlaka inavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa biashara na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Usafiri Baharini imebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa "Accrual basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash basis" jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za mamlaka kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za Mamlaka.

Ukaguzi unashauri Mamlaka ya Usafiri Baharini kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.21.1 Vitabu vya mapato ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Usafiri Baharini inakusanya mapato lakini ukaguzi umeshindwa kuthibitisha mapato yanayopatikana kutokana na huduma mbali mbali za Mamlaka.

Kukosekana kwa vitabu vya ukusanyaji wa mapato kumepelekea kushindwa kufahamu idadi ya fedha iliyokusanywa na taratibu za fedha hizo zilivyotumika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016, uchambuzi wa vitabu hivyo ni kama vinavyonekana katika jadweli lifuatalo:

Jadweli Nambari 93: Vitabu ambavyo havikupatikana kwa ukaguzi

Namba	Mtiririko wa nambari za stakabadhi	Aliyepewa	Maelezo
1	14751 – 14800	Pandu (Mkokotoni)	Vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato havikupatikana kwa ukaguzi
2	15151 – 15200	Pandu (Mkokotoni)	Vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato havikupatikana kwa ukaguzi
3	205401 – 20590	Abubakar Ali Haji	Vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato havikupatikana kwa ukaguzi
4	205851 –205900	Abubakar Ali Haji	Vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato havikupatikana kwa ukaguzi
5	291901 – 291950	Abubakar Ali Haji	Vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato havikupatikana kwa ukaguzi

3.21.2 Kukosekana kwa Mapato yatokanayo na usajili wa vyombo vya uvuvi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 4(1), (b) cha Sheria nambari 3 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar ya mwaka 2009, kinaipa uwezo wa Mamlaka juu ya usajili wa vyombo mbali mbali vikiwemo vya uvuvi baharini. Aidha Kifungu nambari 5(1), (e) kinaeleza uwezo na udhibiti wa Mamlaka juu ya utoaji wa leseni kwa vyombo vidogo vidogo, vyombo vya asili pamoja na kuhakikisha usalama wa vyombo vya uvuvi.

Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali zinazopelekea kuikosesha Serikali mapato kwa kutokuvifanyia kazi kwa vifungu vya sheria tulivyovinakili hapo juu, dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokuvifanyia usajili vyombo vya uvuvi katika maeneo tofauti ya bahari ikiwemo Mkokotoni, Kisakasaka nk.
- Kutokukusanya mapato yanayotokana na vyombo vinavyofanya shughuli mbali mbali baharini zinazofanyika kupitia bandari ndogo ndogo kwa mfano Donge Muanda, Kisakasaka nk.

Kutokuvifanyia kazi vifungu hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 3 ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar ya mwaka 2009.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kwa mwaka wa fedhaunaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.22 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI ZANZIBAR (VTA)

Taarifa ya Mapato.

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 407,430,000. katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020. Hadi kufikia 30, Juni 2020 Mapato halisi yaliyokusanywa na Mamlaka yalikuwa jumla ya shilingi 1,253,763,608. ambayo sawa na asilimia 307.72ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi.

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,168,630,000. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 6,174,273,998 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,994,356,002.00 ikiwa ni matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia 30 Juni 2020, kiasi cha shilingi 5,945,954,275.00 zimeingizwa na kutumika kwa matumizi ya kawaida ni sawa na asilimia 96.30 ya makadirio na shilingi 1,082,127,320. zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa sawa na asilimia 54.25 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.22.1 Tofauti iliyojitokeza baina ya makusanyo halisi na kilichoripotiwa katika taarifa za fedha shilingi 283,171,319.44

Katika kupitia stakabadhi za makusanyo ya mapato, taarifa za kibenki na dafatari la fedha, ukaguzi umebaini kwamba, kuna tofauti pungufu ya shilingi 283,171,319.44 zilizoanishwa katika taarifa ya fedha ikilinganishwa na iliyoripotiwa katika taarifa za makusanyo halisi yaliyopatikana vituoni na Afisi kuu ya mamlaka ya mafunzo amali, kama jadweli linavyoonesha hapo chini:-

Bajeti	Taarifa za kifedha	Makusanyo halisi	Tofauti
214,800,000	1,245,036,512.56	1,528,207,832.00	283,171,319.44

Kuwepo kwa tofauti baina ya taarifa za makusanyo halisi kutoka vituoni na afisi kuu kunapelekea Taarifa ya fedha kutotoa sura nzuri na sahihi.

Ukaguzi unashauri ni vyema uongozi wa Mamlaka kuchukua juhudi za kuhakikisha taarifa zote za kifedha zilizoainishwa ni sahihi kabla ya kuwasilishwa.

3.22.2 Kukosekana kwa uhalisia wa makisio ya makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi

Ukaguzi ulipitia taarifa ya makisio ya makusanyo yasiyo ya kodi pamoja na uhalisia wa makusanyo katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2020 za Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na kubaini uwepo wa tofauti ya shilingi 1,313,407,832 iliyotokana na makusanyo halisi kuwa makubwa zaidi ya makisio na kupelekea uwepo wa tofauti isiyo ya kawaida. Tofauti iliyobainishwa hapo juu inaonyesha udhaifu katika utayarishaji wa makisio. Ufafanuzi wa makusanyo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Bajeti ya Mapato yasiyo ya kodi (Shs)	Makusanyo halisi ya mapato yasiyo ya kodi (Shs)	Tofauti (Shs)
214,800,000	1,528,207,832.00	1,313,407,832.00

Kukosekana kwa uhalisia wa makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi kunaonesha uwezekano wa uwepo wa vyanzo vya mapato ambavyo havijaainishwa katika taarifa za hesabu za Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuandaa makisio yanayoendana na uhalisia wa makusanyo ili kudhibiti uvujaji wa mapato yanayopatikana katika vyanzo ambavyo havikuainishwa katika taarifa za fedha za Mamlaka.

3.22.3 Vifaa vilivyohifadhiwa muda mrefu bila matumizi vyenye thamani ya shilingi 118,901,079

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imenunua vifaa mbalimbali kutoka kwa Mzabuni furniture centre Ltd kwa ajili ya matumizi ya office ya Mamlaka inayotarajiwa kujengwa. Vifaa hivyo vimenunuliwa 3/4/2014 (Ankara namba 573 ya 3/4/2014) kupitia Mradi wa ALSDL II ambao ndio mradi uliojenga kituo cha mafunzo ya Amali Mkokotoni. Lakini ukaguzi umebaini kwamba vifaa hivyo vimehifadhiwa katika vyumba viwili vya dahalia ya wanawake kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita bila ya matumizi.

Aidha ukaguzi umebaini kwamba vifaa hivyo vimekosa ushadi wa nyaraka za kupokelea mali ghalani.

Kufanya manunuzi bila ya kuwa na mahitaji kwa kipindi husika kunapelekea kufanya matumizi mabaya ya fedha za Uma kwa mujibu wa sheria ya fedha na kunapelea uharibifu wa vifaa hivyo pamoja na hasara kwa Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kufanya manunuzi kwa mujibu uhitaji wa matuzi ili kuokoa kufanya manunuzi yasiyo na tija. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 94: Vifaa vilivyo nunuliwa muda mrefu bila ya matumizi

Namba	Idadi	Maelezo	Thamani (Shs)	Jumla ya fedha (Shs)
1.	8	Book shelf hard wood	1,848,825	14,790,600
2.	3	Boston sofa seat 3+3+1	1,856,250	5,568,750
3.	10	Bs 0029-1- black ex high back chair	405,507	4,055,078
4.	2	Bs 590 H Black PU EX HIGHBACK chair	221,941	443,883
5.	5	CMG T-A022 seater chair	433,545	2,167,728
6.	9	FRC 4 4 DRW FIRE Resistance S C	3,410,932	30,698,388
7.	8	GLOB 4 FE ROBIN 4 Drawer filing cabinet	354,236	2,833,895
8.	4	GLOB GD 18SC MAS Office Cupboard -4 Shelves	326,252	1,305,011
9.	50	MODEL 500-310-BLACK Executive chair	221,073	11,053,696
10.	5	MRS YC830-1.6 Executive Table	2,054,830	10,324,150
11.	50	SL 470\3D Hanging Pedestal	183,898	9,194,915
12.	18	SL CT 1400 Computer Table	275,000	4,950,000
13.	50	SL WT 1500 Writing Table	330,507	16,525,381
14.	12	Writing Table Hard WOOD	415,800	4,989,600
Jumla				**118,901,078**

3.22.4 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wanafunzi katika Dakhalia kulinganisha na uwezo wa Dakhalia (Hostel)

Ukaguzi umebaini kwamba Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni kina upungufu wa dakhalia usiokidhi mahitaji ya wanafunzi, hivyo kusababisha mrundikano wa wanafunzi katika vyumba vya dahalia hizo.

Mapitio ya ukaguzi yamebaini kwamba chumba kimoja chenye uwezo wa kulaza wanafunzi 4 kinalaza wanafunzi kumi (10) hali inayohatarisha afya na usalama wa wanafunzi. Aidha dahalia hizo hazina viingiza hewa vya kutosha ikiwemo madirisha na mafeni.

Mrundikano wa wanafunzi katika vyumba vya Dakhalia unaweza kupelekea uwezekano mkubwa wa kupata maradhi ya kuambukiza.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuweka usimamizi mzuri wa wanafunzi wa dahalia kwa kuhakikisha kwamba kiwango cha wanfunzi kila chumba hakizi uwezo wa chumba kwa sababu za kiusalama.

3.22.5 Dosari iliyobainika katika malipo ya mikataba ya zabuni yenye jumla ya shilingi 332,376,974

Katika kupitia hati mbali mbali za malipo pamoja na viambatanisho vyake ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari inayotokana na malipo ya mikataba ya zabuni ya wanaotoa huduma, kwa mujibu wa makubaliano ya pande zote mbili, malipo ya mikataba yote yatafanyika kwa awamu mbili ambayo ni asilimia 90na asilimia 10 baada ya kumalizika kwa kazi. Mamlaka ya mafunzo ya amali imekiuka masharti hayo kwa kulipa asilimia 100 ya kila mkataba wa zabuni uliofungwa.

kufanya hivo ni kwenda kinyume na kifungucha 31(f) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, nambari 11 ya 2016.

Dosari katika malipo ya mikataba hiyo inaweza kuwa na athari ya kifedha, hasa kwa kuwa inaweza kusababisha malipo yasiyo na tija. Ukaguzi unapendekeza kwa uongozi wa Mamlaka kufanya malipo kwa kuzingatia matakwa ya sheria na masharti ya malipo kwa mujibu wa mkataba.Uchambuzi wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Jadweli Nambari 95: Malipo ya mikataba ya zabuni

Namba	Tarehe	Hati ya malipo	Aliyelipwa	Jumla ya fedha (Shs)	Maelezo
1.	29/8/2019	61/9	Diamond Motor Ltd	72,444,719	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa gari aina ya MITSUBISHI PICK UP ENGINE NO 4D56UAV3734
2.	29/8/2019	107/10	Cfao Motors	107,024,820	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa gari aina ya MERCEDES BENZ 65195033932240
3.	10/12/2019	36/12	Greenland General Supply Company Ltd	95,725,087	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyaa practical kwa ajili ya mitihani ya taifa ya Mamlaka ya mafunzo ya Amali
4.	12/12/2019	37/12	Visiwani General Supplies	57,182,348	Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vyaa practical kwa ajili ya mitihani ya taifa (MWANAKWEREKWE, MKOKOTONI,VITONJI)

Ukaguzi unashauri kwamba Uongozi Mamlaka ya Mafunzo ya Amali uchukue juhudi kuhakikisha kwamba manunuzi yanayofanyika katika taasisi hiyo yanafuata Sheria ya Ununuzi kikamilifu, ili kuepuka kufanya matumizi kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

MAMALAKA YA MAFUNZO YA AMALI (MMA)- PEMBA

3.22.6 Mamlaka kushindwa kufikia malengo ya kukusanya mapato shilingi 51,620,000

Jumla ya shilingi 51,620,000 zilikadiriwa kukusanywa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali – Pemba kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio haya ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2020, jumla ya shilingi 42,699,398 zilikusanywa sawa na asilimia 82.7 ya makadirio ambapo hali hii inaonyesha Mamlaka imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

3.22.7 Kukosekana kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali–Pemba haina kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kuweza kusimamia shughuli za ukaguzi wa ndani na utoaji wa taarifa juu ya makusanyo na matumizi ya fedha za Serikali.

Kutokuwepo kwa kitengo cha mkaguzi wa ndani inaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha na mali za umma aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

3.22.8 Kukosekana kwa mpango wa manunuzi wa mwaka wa Mamlaka

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali – Pemba haina mpango wa manunuzi wa mwaka ili kuweza kuthibitisha mpango wa manunuzi mzima wa Mamlaka na utekelezaji wake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016 pamoja na kifungu nambari 46(1)(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

3.22.9 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 13,296,979

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 13,296,979 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Jadweli Nambari 96: Malipo yasiyokuwa na vielelezo

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	1/7 04/7/2019	000662	1,600,000	VTA	Malipo ya fedha za posho na chakula kwa usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali
2.	1/1 3/01/020	000781	252,000	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa ofisi
3.	19/1 31/01/020	000797	310,600	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa ofisi kwa mwezi wa January, 2020
4.	2/2 25/01/020	000800	2,376,500	Suleiman Said Mo-hammed	Malipo ya fedha kwa ajili ya usanifu wa mchoro na utayar-ishaji wa makadirio ya ujenzi wa nyumba ya wageni
5.	4/2 04/02/020	000802	1,308,200	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa kituo kwa mwezi wa January, 2020
6.	22/2 27/2/2020	000817	1,310,000	VTA	Malipo ya fedha za posho la usimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali
7.	23/2 27/2/2020	000817	500,000	VTA	Marejesho ya fedha zilizotumika kwa chai na chakula kwa wasimamizi wa mitihani ya marudio katika chuo cha Mafunzo ya Amali
8.	1/3 04/03/020	000819	1,447,600	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa kituo kwa mwezi wa February, 2020
9.	3/3 05/03/020	000820	150,000	VTA	Malipo ya fedha za imprest kwa matumizi madogo madogo ya kituo
10.	4/3 04/03/020	000823	252,800	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa ofisi kwa mwezi wa February, 2020
11.	22/3 31/03/020	000835	1,901,200	VTA	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa kituo kwa mwezi wa March, 2020

12.	2/5 07/2/2020	000803	1,888,079	TRA	Malipo ya fedha za kodi ya TRA inayokatwa kwa wafanya biashara kwa mwezi wa January 2020
Jumla			**13,296,979**		

3.22.10 Kukosekana kwa zabuni ya mkandarasi wa ujenzi wa jengo la maabara katika chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali – Pemba.

Jumla ya shilingi 107,147,338.78 zimelipwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali –Pemba kwa Mkandarasi wa ujenzi wa jengo la maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya mkandarasi wa ujenzi wa maabara hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha alicholipwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 97: Malipo ya zabuni ya mkandarasi ya ujenzi wa maabara

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	69/6 28/6/2019	000647	23,498,250	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa kazi ya ujenzi wa msingi.
2.	76/6 28/6/2019	000654	11,749,125	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya pili kwa kazi ya ujenzi wa msingi.
3.	78/6 28/6/2019	000656	3,916,375	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwisho kwa kazi ya ujenzi wa msingi.
4.	10/9 10/9/2019	000676	9,952,200	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa kazi ya ujenzi wa kuta jengo la maabara.
5.	1/10 01/10/2019	000706	4,976,100	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa kazi ya ujenzi.
6.	36/11 25/11/2019	000750	1,658,700	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya pili kwa kazi ya ujenzi.

7.	15/12 18/12/2019	000766	5,529,000	Iddi Mohammed Salim	Malipo ya fedha kwa kazi ya ujenzi wa paa pamoja na dari la jengo.
8.	22/12 04/12/2020	000771	4,423,200	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa kazi ya upingaji wa plasta.
9.	11/1 22/1/2020	000789	5,529,000	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya pili kwa kazi ya upingaji wa plasta jengo la maabara katika chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji
10.	15/1 30/1/2020	000793	1,105,800	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya tatu kwa kazi ya upingaji wa plasta.
11.	1/2 03/2/2020	000799	5,529,000	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya kwanza kwa kazi ya maliziaji wa ujenzi.
12.	17/2 25/2/2020	000812	13,195,327.1	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya kwanza kwa kazi ya umaliziaji ujenzi.
13.	12/4 19/4/2020	000845	10,556,261.68	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya pili kwa kazi ya kumalizia ujenzi.
14.	16/4 19/4/2020	000849	5,529,000	Salim Hamad Simba	Malipo ya fedha za awamu ya mwisho kwa kazi za kumalizia ujenzi
Jumla			**107,147,338.78**		

3.22.11 Kukosekana kwa zabuni ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi Shilingi 236,269,842.1

Jumla ya shilingi 236,269,842.1 zimelipwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali – Pemba kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ujenzi wa jengo la maabara katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji.

Ukaguzi umebaini kwamba malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara hiyo hayakuzingatia uwepo wa zabuni kulingana na kiwango cha fedha kilichotumika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 68(1)(2)(3)(4) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 98: Malipo ya manunuzi ya vifaa vya ujenzi

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
55/6 25/6/2019	000633	13,783,700	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa nondo kwa kazi ya ujenzi wa maabara
56/6 25/6/2019	000634	13,973,820	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara
57/6 25/6/2019	000634	13,973,820	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara
58/6 25/6/2019	000635	7,830,092	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara
61/6 27/6/2019	000638	13,736,170	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara
78/6 28/6/2019	000649	10,000,000	Vitongoji Development Fund	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa matufali kwa ajili ya ujenzi wa maabara
80/6 29/6/2019	000658	13,589,777	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa maabara
26/9 22/9/2019	000686	370,440	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji kwa ajili ya ujenzi wa maabara
7/11 16/10/2019	000726	5,061,945	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa maabara
20/11 16/11/2019	000737	12,719,028	Abdalla Massoud Said	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mbao kwa ajili ya kuezeka jengo la maabara
22/11 17/11/2019	000738	416,000	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa misumari kwa ajili ya kuezeka jengo la maabara
29/11 22/11/2019	000744	11,355,260	Hamad Said Bakar	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuezekea jengo la maabara
5/12 5/12/2019	000756	12,365,150	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya milango na madirisha kwa ajili ya ujenzi wa maabara
6/12 5/12/2019	000757	5,038,180	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa saruji na mchanga kwa ajili ya upigaji plaster katika ujenzi wa maabara

16/12 18/12/2019	000767	12,690,510	Maro master Alluminium	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utiaji dari katika ujenzi wa maabara
17/12 20/10/2019	000723	11,116,316.4	Maro master Alluminium	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya alluminium kwa ajili ya utengenezaji wa milango na masirisha katika ujenzi wa maabara
18/12 18/12/2019	000768	11,123,000	Asaa Kheri Asaa	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utengenezaji wa milango na madirisha kwa ujenzi wa maabara
27/12 27/12/2019	000776	13,878,760	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya rangi kwa ajili ya ujenzi wa maabara
28/12 27/12/2019	000777	7,859,600	Khamis Yousuf Hamad	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa floor tiles kwa ajili ya ujenzi wa maabara
30/12 27/12/2019	000779	10,584,000	Khamis Yousuf Hamad	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa wa tiles kwa ajili ya ujenzi wa maabara
10/1 21/1/2020	000788	2,773,400	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa maabara
81/1 30/1/2020	000796	13,000,405.6	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ujenzi wa maabara
9/2 07/2/2020	000807	6,443,166.8	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi jengo la maabara
10/2 12/2/2020	000808	4,942,169.4	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ajili ya fitting katika jengo la maabara
15/3 19/3/2020	000828	613,970	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya ujenziwa jengo la maabara
18/3 30/3/2020	000831	1,958,236	Omar Hamad Kombo	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mchanga na saruji kwa ajili ya uendelezaji wa ujenzi wa jengo la maabara
19/3 30/3/2020	00032	2,110,920	Nassor Said Nassor	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya welding kwa ujenzi wa maabara

20/4 23/5/2020	000853	2,770,460	Khamis Yousuf Hamad	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ujenzi wa maabara
17/6 14/6/2020	000897	191,545.9	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ujenzi wa maabara
Jumla		**236,269,842.1**		

3.22.12 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 21,225,000

Jumla ya shilingi 21,225,000 zimehaulishwa kutoka hesabu ya Vitongoji Development kwenda hesabu nyengine tofauti na baadhi fedha hizo kulipwa kwa watoa huduma mbali mbali kwa matumizi ya Chuo cha Mafunzo ya Amali –Pemba. Ukaguzi umebaini kwamba vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 99: Malipo yasiyokuwa na vielelezo

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	3/7 25/7/2019	T.O	11,130,000	VTA	Uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404447000 ya mamlaka ya Mafunzo ya Amali –Pemba.
2.	1/8 26/8/2019	T.T	3,600,000	PBZ	Uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0511030000 ya mamlaka ya Mafunzo ya Amali –Zanzibar.
3.	1/3 31/3/2020	T.O	6,155,000	VTA	Uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu namba 0404157000 ya Vitongoji Development Fund kwenda hesabu namba 0404163000 ya mamlaka ya Mafunzo ya Amali –Pemba loan.
4.	1/5 27/4/2020	000156	140,000	Saleh Juma Mussa	Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kuhamisha matufali

5.	1/6 30/6/2020	000159	200,000	VDF	Malipo ya fedha kwa ajili ya ushonaji wa barakoa kwa ajili ya matumizi ya kituo.
Jumla			**21,225,000**		

3.22.13 Vifaa ambavyo taratibu za mapokezi hazikuthibitishwa shilingi 16,323,817.20

Jumla ya shilingi 16,323,817.20 zimelipwa kwa ajili ya usambazaji chakula na vifaa mbali mbali katika kambi ya usahihishaji wa mitihani ya STD IV katika skuli ya Fidel castro – Pemba. Malipo hayo yalifanywa kwa kutumia hati namba 4/1 ya tarehe 23/1/2020 kwa kutumia hundi namba 000404 ambayo alilipwa ndugu Farouk Salim Said kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hio.

Ukaguzi umebaini kwamba vifaa vilivyonunuliwa havikuingizwa katika daftari la kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

3.22.14 Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa posho na gawio la faida shilingi 23,962,398

Jumla ya shilingi 23,962,398 zimelipwa na Chuo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali – Pemba kwa ajili ya posho pamoja na gawio la faida kwa watendaji walioshiriki katika kazi ya kutoa huduma kwa wasahihishaji wa mitihani ya darasa la nne.

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa muongozo wa malipo ya posho na gawio la faida kwa watendaji hao ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016.

Jadweli Nambari 100: Malipo ya posho na gawio yaliyofanyika bila ya miongozo

Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
3/1 21/1/2020	000403	14,675,000	Vitongoji skills development center	Malipo ya fedha za posho la watendaji walioshiriki katika kazi ya kutoa huduma kwa wasahihishaji wa mitihani ya darasa la nne Fidel Castro.
3/2 10/2/2020	000413	9,287,398	Vitongoji Skills Development Centre	Malipo ya gawio la faida kwa watendaji walioshiriki katika kazi ya kutoa huduma kwa wasahihishaji wa mitihani ya STD IV Fidel Castro
Jumla		**23,962,398**		

3.22.15 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 29,196,971

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 29,196,971 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Chuo ca Mafunzo ya Amali lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 101: Malipo yaliofanywa bila ya vielelezo

Hati Namba	Hundi Namba	Jumla ya fedha (SHS)	Aliyelipwa	Maelezo
1/8 9/8/2019	000393	1,291,700	Vitongoji skill development centre	Malipo ya fedha za nauli kwa wafanyakazi wa kituo cha Mamlaka ya Mafunzo ya Amali vitongoji kwa mwezi wa Juni, 2019
7/1 20/1/2020	000407	3,591,271	Hasina catering and take aware service	Malipo ya fedha kwa ajili ya usambazaji wa vyakula mbali mbali kwa ajili ya kambi ya usahihishaji wa mitihani
4/2 18/2/2020	000414	1,725,000	Vitongoji Skills Development Centre	Malipo ya fedha za nauli na posho la kukaimu kwa safari kikazi Unguja kwa mkuu wa kituo na wasaidizi wake
9/3 31/3/2020	T.O	4,589,000	Vitongoji Skills Development Centre	Uhalishaji wa fedha zilizotumika kwa un-ununzi wa chakula cha mradi wa vijana na Ajira –Kengeja kutoka A/C 0404068000 kwenda 044447000

7/4 27/4/2020	000430	18,000,000	Vitongoji Skills Development Centre	Malipo ya fedha za posho ya chakula kwa wanafunzi 240 wa mradi wa vijana na ajira katika kazi za vitendo wilayani ya Mkoani, Chake, Wete na micheweni
Jumla		**29,196,971**		

Maoni ya Ukaguzi

Hati Yenye Shaka

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi isipokuwa kwa mambo niliyoainisha hapo juu, kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imepata hati yenye shaka kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.23 MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE ZANZIBAR

Taarifa ya mapato

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 205,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imekusanya jumla ya shilingi 29,085,000 ambazo ni sawa na asilimia 14.2 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 804,200,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka imetumia jumla ya shilingi 673,737,600 ambazo ni sawa na asilimia 83.8 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.23.1 Kutokuwepo kwa kitengo cha ukaguzi wa ndani

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar haina kitengo cha ukaguzi wa ndani hali inayopelekea kuwepo kwa mapungufu katika mfumo wa usimamizi wa ndani. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 117(1) cha Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016.

3.23.2 Kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za mishahara ya wafanyakazi (Salary Register)

Kwa mujibu wa utaratibu wa kiutumishi Serikalini inazitaka idara na taasisi zote kuweka kumbukumbu sahihi za wafanyakazi wake ili kuweza kuepusha usumbufu utakaoweza kujitokeza kwa wafanyakazi hao mara baada ya kufikia muda wa kustaafu, ikiwemo kumcheleweshea au kumkosesha haki zake za kimsingi kwa mujibu wa taratibu.

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha rasilimali watu hakiwajibiki ipasavyo katika utunzaji wa kumbukumbu sahihi za wafanyakazi wake, kwani imebainika taarifa za mafao ya wafanyakazi ambazo zitakuja kufanyiwa hesabu ili kuweza kuwatengenezea na kuwalipa wafanyakazi hao mafao yao ya uzeeni hazijazwi na hatimae kukosekana kumbukumbu za "salary register" Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 13 cha Sheria nambari 3 ya Uanzishwaji wa Taasisi ya kumbukumbu na Nyaraka ya mwaka 2008.

3.23.3 Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar imefunga hesabu zake na kuziwasilisha katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa kazi. Katika ukaguzi huo imebainika baadhi ya mali za kudumu hazikuoneshwa katika taarifa ya hesabu ya Mamlaka jambo ambalo limepelekea taarifa za hesabu kukosa uhalisia. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Fedha na Usimamizi wa Mali za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mali hizo ni kama ifuatavyo:-

Jadweli Nambari 102: Mali za kudumu

Namba	Aina ya chombo	Nambari ya Usajili wa Chombo	Nambari ya Ingini
1	Vespa module star	SMZ -727c.	Chasis-md711eaebe3150169- regz046270059
2	Honda Click	SMZ-1697c.	chas-mlhijf 350445434852-Reg-z-0483887710
3	Honda click	SMZ 1916c.	chasmlhjf 3525c5053456-Reg-z-048895462
4	Honda Pasola	SMZ -1639c.	Chasis AF61-1203229. Reg z-048341139.
5	Vespa Star	SMZ -342c.	–chas md 711eabc3143323.

3.23.4 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na utaratibu shilingi 62,827,506

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza "Kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya umma isipokuwa mtu huyo, kampuni au chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi chini ya sheria hii".

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi, kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo. Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuikosesha serikali mapato yanayotokana na kodi ya thamani na ni kwenda kinyume na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

Jadweli nambari 103: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa

Namba	Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Aliyelipwa	Jumla ya fedha (Shs)	Maelezo
1	4/1	T.T	Said Abdalla Ali	12,903,000	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi
2	3/1	T.T	Vuaa Khamis Mtumwa	13,800,000	Ukarabati wa jengo la skuli ya Hurumzi.
3	1/1	T.T	Ali Said Ali	6,400,000	Ukarabati wa jingo la Mahkama
4	2/5	T.T	Said Abdalla Ali	3,019,866	Ununuzi wa vifaa vya ujenzi (chokaa)
5	1/6	T.T	Saidel Gheithy	3,450,000	Utengenezaji wa filam
6	2/6	98	Munira Humoud Said	2,500,000	Kutoa elimu ya urithi wa mji mkongwe
7	6/2	T.T	Hamadi Abdalla Omar	4,750,000	Ujenzi wa jengo la kondominio
8	11/5	T.T	Mohamed Abeid Juma	6,300,000	Utengenezaji wa madirisha ya chuma ktk jengo la kondominio
9	9/7	54	H.S.E& Security Tasks (T) Ltd	1,354,640	Malipo ya walinzi wa jengo la Beit el ajaib
10	1/10	62	Mamlaka Mji Mkongwe	2,250,000	Gharama za Mafundi
11	1/11	65	Mamlaka Ya Mji Mkongwe	2,300,000	Gharama za uhamasishaji wa mafundi
12	8/1	T.T	Black Roots Investiment	2,000,000	Uandaaji tangazo kwa njia ya video
13	10/5	T.T	Masoud Rashid Abdalla	1,800,000	Usimamizi wa Ujenzi jengo la Mahakama Kuu.
Jumla				**62,827,506**	

3.23.5 Ukiukwaji wa taratibu za kumtafuta mkadiriaji wa majengo (Quantity Surveyor) shilingi 293,500,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kufanyika kwa matengenezo ya ukarabati wa jengo la Beit El Ajaib katika ukarabati huo kasoro mbali mbali ziliweza kubainika kama ifuatavyo:-

- Kutotangazwa kwa Zabuni ya kumtafuta mkadiriaji wa majengo (Consultant)
- Kutokufanyia kazi kwa ushauri elekezi kutoka kwa Mwanasheia Mkuu wa serikali juu ya Mkataba uliofungwa jambo ambalo limepelekea kwenda kinyume na kifungu cha 27(3) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.
- Kukosekana kwa muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni ya Mamlaka ya Mji Mkongwe.
- Kutokubainishwa kwa namna ya ulipwaji wa Mshauri elekezi (Mode of Payment)

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe Zanzibar imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.24 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI ZANZIBAR

Taarifa ya Matumizi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,061,400,000 kati ya fedha hizo shilingi 1,095,900,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 965,500,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imepokea na kutumia jumla ya shilingi 1,741,092,718 sawa na asilimia 84 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 1,097,611,696 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 100 ya makadirio na shilingi 643,481,022 kwa matumizi mengineo sawa na asilimia 67 ya makadirio.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.25 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

TAARIFA ZA UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA

Katika uwasilishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2018/2019 na 2019/2020 za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kubaini kuwa taarifa za fedha hazikuonyesha uhalisia kulingana na vigezo vya utayarishaji wa hesabu hizo. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iliutaka uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kufanya mapitio na masahihisho ya hesabu zilizowasilishwa kwa ajili kukaguliwa na baadae ziwasilishwe si zaidi ya tarehe 25/3/2021 kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu Namba NAM.AUD/W/EMA/CKTZ/10/8/VOL.1/1 ya tarehe 18/3/2021 ili kuweza kuzipitia na kuzitolea maoni kwa mujibu wa vigezo vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa. Hata hivyo Chuo Kikuu cha Taifa kilishindwa kuzirekebisha hesabu hizo na kuziwasilisha kwa ajili ya ukaguzi.

Aidha, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mara nyengine ilitoa barua yenye kumbukumbu Namba NAM.AUD/W/EMA/CKTZ/10/8/VOL.1/2 ya tarehe 16/4/2021 iliyotowa taarifa kwa Uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwamba kazi za ukaguzi na uwandishi wa ripoti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 umekamilika na matokeo ya ukaguzi wa taasisi yako yatachukuliwa na kubainishwa katika ripoti kuu kwa mujibu wa maelezo ya barua ya awali.

Maoni ya Ukaguzi

Hati Mbaya

Ukaguzi umeshindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha zilizoandaliwa na Chuo Kikuu Taifa cha Zanzibar kwa ajili ya ukaguzi, hali hii imeathiri taarifa za fedha kiasi cha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusiana na taarifa hizo.

3.26 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Taarifa ya Mapato.

Chuo cha Utawala wa Umma kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,152,154,000 kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya hizo jumla ya shilingi 1,118,564,000 ni ruzuku na shilingi 2,033,590,000 ni makusanyo ya ndani.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Chuo cha Utawala wa Umma kilipokea jumla ya shilingi 1,108,323,675 kama ni ruzuku sawa na asilimia 99 ya makadirio na jumla ya shilingi 1,153,093,920 sawa na asilimia 57 ya makadirio.

Taarifa ya Matumizi

Chuo cha Utawala wa Umma kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,101,147,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Hadi kufikia 30 Juni 2020 kiasi cha shilingi 2,255,555,478 zilitumika sawa na asilimia 73 ya makadirio.

Ufanisi katika utendaji wa Chuo Cha Utawala wa Umma

Katika utendaji wa kifedha wa Chuo cha Utawala wa Umma (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinachoonesha namna Chuo kinavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa biashara na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Chuo cha Utawala wa Umma kimebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa "Accrual basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash basis" jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Chuo kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za chuo.

Ukaguzi unashauri Chuo cha Utawala wa Umma kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.26.1 Madeni yanayodaiwa na Chuo cha Utawala wa Umma kwa muda mrefu shilingi 57,150,000

Katika ukaguzi uliofanyika, kumebainika uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo hakuna jitihada zozote zilizofanywa katika ufuatiliaji wa kuhakikisha madeni hayo yanalipwa jambo ambalo linapelekea kuathiri uwezo wa Chuo kujiendesha kiufanisi. Aidha kutokuwepo kwa ufuatiliaji mzuri wa madeni kunapelekea uwepo wa madeni sugu ambayo hayataweza kulipika na kusababisha hasara kubwa kwa Chuo na kuibebesha mzigo mkubwa Serikali. Kuongezeka kwa wadaiwa kunachangiwa na kutokuwepo kwa jitihada za ukusanyaji wa madeni pamoja na kukosekana kwa sera nzuri ya ukusanyaji wa madeni hayo.
Ukaguzi unashauri Chuo cha Utawala wa Umma, kuandaa mikakati na mbinu zitakazowezesha kukusanya madeni hayo kwa wakati pamoja na kuandaa sera ya ufuatiliaji wa madeni.

Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:-

Jadweli Nambari 104: Madeni yanayodaiwa na Chuo cha Utawala wa Umma

Namba	Jina la Mdaiwa	Nambari ya Ankara	Fedha zinazodaiwa (Shs)
1	Wizara ya Fedha	1838	450,000
2	Mkuu Wa Mkoa Kusini	1843	2,100,000
3	Kamisheni ya Utalii	1847	150,000
4	Wizara ya Vijana	1849	1,200,000
5	Chuo Cha Uandishi Wa Habari	1853	1,500,000
6	Mkurugenzi Wa Mashtaka	1857	450,000
7	(OR) Tawala Za Mikoa	1886	2,100,000
8	W/Ardhi Nyumba Maji	1897	1,200,000
9	Wizara ya Habari	1898	450,000
10	Mamlaka Viwanja Vya Ndege	1931	1,050,000
11	Wizara ya Ardhi Pemba	1932	900,000
12	Ofisi ya Mdhamini	1946	7,500,000
13	Wizara ya Fedha Pemba	1953	1,050,000
14	Ofisi ya Mkuu Wa Mkoa Kusini	1956	1,200,000
15	Ofisi ya Mkuu Wa Wilaya Kati	1957	600,000
16	Idara ya Nishati	1962	1,050,000
17	Mamlaka ya Hifadhi Mji Mkongwe	1964	150,000
18	Baraza la Mji Chake	1868	2,850,000
19	Ofisi Wa Makamo wa Pili	1975	3,750,000
20	Wizara ya Biashara	1976	1,650,000
21	Baraza la Mji Mkoani Pemba	1977	8,100,000
22	Wizara ya Biashara Na Viwanda	1980	1,650,000
23	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	1982	150,000
24	OMPR Idara ya Mipango	1985	300,000
25	OMPR Watu Wenye Ulemavu	1986	150,000
26	OMPR Madawa ya Kulevya	1988	150,000
27	OMPR Uendeshaji na Utumishi	1987	1,200,000
28	OMPR Tume Ya Ukimwi	1989	900,000
29	OMPR Mamlaka ya Mazingira	1990	150,000
30	OMPR Idara ya Sherehe	1991	150,000
31	OMPR Ofisi ya Uratibu SMZ	1992	300,000
32	OMPR Ofisi Kuu Pemba	1993	150,000
33	Wizara ya Kazi Wanawake na Watoto	1996	2,250,000

34	Wizara ya Kazi Wanawake na Watoto	1997	2,250,000
35	Wizara ya Kazi Wanawake na Watoto	1998	1,500,000
36	Wakala wa Uchapaji	2014	1,650,000
37	Mamlaka Mji Mkongwe	2017	3,000,000
38	Wizara ya Fedha	2021	1,350,000
39	Utumishi wa Umma Pemba	2023	450,000
Jumla			**57,150,000**

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Chuo Cha Utawala wa Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura halisi na sahihi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Chuo Cha Utawala wa Umma kimepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.27 CHUO CHA UANDISHI WA HABARI.

Taarifa ya mapato

Chuo cha Uandishi wa Habari kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 142,000,000 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufikia 30 Juni, 2020 Chuo kilikusanya jumla ya shilingi 77,625,135 sawa na asilimia 54.6 ya makadirio.

Taarifa ya matumizi

Chuo cha Uandishi wa Habari kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 833,400,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia 30 Juni, 2020 jumla ya shilingi 845,058,603 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 101.4 ya makadirio.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.27.1 Kushuka kwa kiwango cha udahili wa wanafunzi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Chuo cha Uandishi wa Habari kimekabiliwa na changamoto kubwa ya udahili wa wanafunzi jambo ambalo hupelekea kuporomoka kwa mapato ya chuo mwaka hadi mwaka.

Aidha ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Chuo cha Uandishi wa Habari kimekuwa na upungufu mkubwa wa wanafunzi ambapo hadi sasa chuo kimedahili wanafunzi 67 tu sawa na 42 ya makadirio, ambapo lengo kuu la chuo ni kudahili wanafunzi 160 kwa mwaka sawa na 100, jambo ambalo limeathiri kwa kiasi kikubwa taswira ya uzalishaji wa fani ya uandishi wa habari, mapato ya chuo na harakati za uendeshaji na ukuzaji wa chuo.

Ufanisi katika utendaji wa Chuo cha Uandishi wa Habari

Katika utendaji wa kifedha wa Chuo cha Uandishi wa Habari (financial performance) na kiutendaji (Operating performance) ni kipimo kinachoonesha namna Chuo kinavyoweza kutumia mali zake kutokana na msingi wa utoaji wa huduma na namna ya ukusanyaji wa mapato katokana na vyanzo vyake mbali mbali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Chuo cha Uandishi wa Habari kimebadilisha namna ya ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kutoka katika mfumo wa "Accrual basis" na kuingia katika mfumo wa "Cash basis" jambo ambalo ni dosari kwa mfumo wa uendeshaji wa shughuli za chuo kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vilivyopo kitaifa na kimataifa na kupelekea kutokuonekana kwa taarifa muhimu ambazo zinawezesha kupima ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za chuo.

Ukaguzi unashauri Chuo cha Uandishi wa Habari kuandaa hesabu zake kwa kufuata miongozo ya uandaaji na utayarishaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa viwango vya uandaaji wa hesabu kitaifa na kimataifa.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Chuo Cha Uandishi wa Habari kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2020 zinaonesha sura sahihi na halisi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Chuo cha Uandishi wa Habari kimepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.28 TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Taarifa ya mapato

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 1,349,147,000 kutoka vyanzo vyake mbali mbali vya mapato na shilingi 1,626,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikali kuu.

Hadi kufikia Juni 2020 Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia ilikusanya jumla ya shilingi 604,834,725 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 44.8 ya makadirio na shilingi 1,677,098,660 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini sawa na asilimia 103.Taasisi ya sayansi ya Karume imeshindwa kufikia malengo ya makusanyo yake ya ndani kwa asilimia 55.2.

Taarifa ya matumizi

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,631,500,000 kati ya hizo shilingi 1,216,500,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 415,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia 30 Juni, 2019 jumla ya Shillingi 1,538,352,710 ziliingizwa na kutumika ikiwa sawa na asilimia 94 ya makadirio, kati fedha hizo shilingi 1,206,347,910 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 99 na shilingi 331,996,800 kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 80, ya fedha zilizoidhishwa na kutumika.

MATOKEO YA UKAGUZI

3.28.1 Kukosekana kwa mpango wa manunuzi wa mwaka

Kifungu cha 42(1) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11, 2016 kinaeleza kwamba Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, kwa kila mwaka wa fedha katika tarehe itakayoelezwa na Mlipaji mkuu wa Serikali, itaandaa na kuwasilisha kwa Mlipaji mkuu wa Serikali na Mamlaka mpango wake wa mwaka wa ununuzi na uondoshaji kwa mwaka unaofuata, sheria.

Aidha Kifungu cha 29(e) cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba moja ya kazi ya kitengo cha manunuzi na uondoshaji wa mali za umma ni kupanga na kuandaa mipango ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma za taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma. Ukaguzi umebaini kuwa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia haikutayarisha mpango wake wa manunuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa mwaka 2019/2020, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 42 cha Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma nambari 11 ya mwaka 2016.

Maoni ya Ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura halisi na sahihi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

3.29 TUME YA KITAIFA YA KURATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Taarifa ya matumizi

Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,653,200,000 kwa kazi za kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 973,200,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na shilingi 680,000,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia 30 Juni,2020 jumla ya shilingi 1,550,814,388 zimeingiziwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 94 ya makadirio kati ya hizo 870,814,388 zilitumika kwa matumizi ya kawaida, na shilingi 680,000,000 zilitumika kwa matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

Maoni ya ukaguzi

Kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi, hesabu za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020 zinaonesha sura halisi na sahihi kufuatana na vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kwa hali hiyo Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imepata hati inayoridhisha kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2020.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO NAMBARI 1:

Orodha ya madeni ya kodi ya muda mrefu ambayo hayajasuluhishwa shilingi 20,515,860,319 na USD. 4,110,033

Mwaka wa Fedha 2014							
Namba	**Jina la Mlipa Kodi**	**Fedha za madeni ya Kodi Halisi**		**Fedha za Kodi zilizolip-wa**		**Bakaa ya fedha za kodi zilizosalia**	
		TZS	**USD**	**TZS**	**USD**	**TZS**	**USD**
1	Step Two Co.Ltd (Paje By Night Hotel)	42,044,527	-	8,149,999	-	33,894,527	-
2	Salim Rashid Nassor	63,893,008	-	-	-	63,893,008	-
3	Samos (Karafuu Hotel)		1,230,446.00	-	-	-	1,230,446
	Jumla	105,937,535	1,230,446	8,149,999	-	97,787,535	1,230,446
Mwaka wa Fedha 2015							
4	Zanzibar Tea Packers Co.Ltd	55,509,499	-	-	-	55,509,499	-
5	Zatepa Food Co.Ltd	18,652,378	-	-	-	18,652,378	-
6	SalumNassor Ali	65,583,061	-	-	-	65,583,061	-
7	Al-batina Building Co.	834,169,112	-	-	-	834,169,112	
8	Sogea Satom	1,882,725,398	-	-	-	1,882,725,398	-
9	Cristal Resort Ltd	15,669,585	98,515			15,669,585	98,515
10	Al-mubeen G. Group	45,951,129	-	-	-	45,951,129	--
	Jumla	2,918,260,162	98,515			2,918,260,162	98,515
Mwaka wa Fedha 2016							
11	Imara Consultants	56,174,069		18,700,000		37,474,069	-

12	Gallery Tours and Safari Ltd		148,596				148,596
13	Dhow inn Hotel/ GUMASA	53,502,519	223,117		25,000	53,502,519	196,117
	Jumla	109,676,588	447,581	18,700,000	25,000	90,976,588	422,581
Mwaka wa Fedha 2017							
14	Dezo Civil ConstructionCo.Ltd	1,026,310,636	-	-	-	1,026,310,636	-
15	Zan Air Ltd	191,086,826	-	-	-	191,086,826	-
16	Zan Tours Ltd	2,044,161,197	-	-	-	2,044,161,197	-
17	My Blue Boutique Hotel (SAGI-OMA)	-	2,358,491	-	-	-	2,358,491
	Jumla	3,261,558,659	2,358,491	-	-	3,261,558,659	2,358,491
Mwaka wa Fedha 2018							
18	MIC Tanzania Ltd Tigo	14,531,671,445	-	384,394,070	-	14,147,277,375	-
	Jumla	14,531,671,445	-	384,394,070	-	14,147,277,375	-
	Jumla Kuu	**20,927,104,389**	**4,135,033**	**411,244,070**	**25,000**	**20,515,860,319**	**4,110,033**

KIAMBATANISHO NAMBARI 2: Malipo ya Bima yaliyochelewa kupelekwa Benki

Namba	Tarehe ya makusanyo	Jina la Waka-la	Stakabadhi za makusanyo	Fedha iliyokusanywa	Tarehe iliyopelekwa benki	Maelezo
1	25/09/2019	SMS	296829-156850	8,456,770	02/01-28/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitatu (3)
2	19/09/2019	ARON	156829-156850	28,852,720	6/01/ to 31/01/ 2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitatu (3)
3	18/10/2019	ARON	158851-158900			
4	22/11/2019	ARON	161551-161597			
5	2/12/2019	ARON	161757-161785			
6	12/8/2019	SAFESIDE	151539-151550	2,688,100	27/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitatu (3)
7	2/12/2019	SAFESIDE	160262-160264	446,100	2/1/2020	Delayed for a month
8	20/08/2019	TH	151969-154551	19,983,300	3/1/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
9	2/12/2019	TH	162008-162035	4,029,000	27/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
10	1/8/2019	EAGLE	152181-151250	13,449,640	17/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne (4)
11	25/10/2019		157751-157800	11,281,005	29/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitatu (3)
12	2/12/2019		159987-16000	2,647,316	13/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
13	3/10/2019	AIKA	158351-158400		18/01/2020	
14	2/12/2019		161805	141,600	8/1/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
15	3/10/2019		158451-158400	9,371,500	18-31/01/20	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne (4)

16	28/11/2019	RESPONSIVE	157535-157550	3,392,500	4/7/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi saba (7)
17	3/12/2019		162801-162812	2,094,500	2/1/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
18	3/12/2019		162813-162823	1,298,000	4/1/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
19	3/12/2019		162824-162833	1,121,000	13/01/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
20	15/08/2019	BAHASANY	152219-152250	5,701,450	03-22/01/20	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitano (5)
21	1/12/2019		159663-159667	1,097,400	3&6/01/20	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
22	20/09/2019	MADSON	158478	1,079,700	2/1/2020	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne (4)
23	6/12/2019	WASTARA	162301-152750	66,214,445	02-07/01/20	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
Jumla				**183,346,046**		

Tawi la Mwanza

Namba	Tarehe ya makusanyo	Jina la Wakala	Stakabadhi ya Makusanyo	Fedha iliyokusanywa	Tarehe iliyopelekwa benki	Maelezo
1	10.01.2019	ROMAKA INSURANCE AGENT	132336	59,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi 12
2	10.01.2019	ROMAKA INSURANCE AGENT	132337	59,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi 12
3	10.01.2019	ROMAKA INSURANCE AGENT	132341	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi 12
4		GIBELTIAN	130886	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi 12
5	01.08.2019		130888	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitano
6	01.08.2019		130890	230,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitano
7		ARARATI	131871	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
8	05.09.2019		131872	141,600	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
9	05.09.2019		131873	141,600	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne

10	05.09.2019		131874	141,600	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupele-kwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
11	05.09.2019		131875	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
12	05.09.2019		131876	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
13	05.09.2019		131877	141,600	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
14	05.09.2019	FRESH FAMILY FOODS BROKER	100932	354,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi minne
15	22.7.2019	BAWAZIR CARGO LTD.	100933	118,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitano
16	22.7.2019	ENDLESS SAFARIS LTD.	100943	177,000	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya miezi mitano
17	9.9.2019	MARY PAUL MUSHI (DIRECT DEBTOR)		1,020,110	Kukosekana kwa uthibitisho wa fedha hizo kupelekwa Benki	Fedha zimechelewa kupelekwa Benki kwa zaidi ya mwezi mmoja
Jumla				**3,291,510**		

KIAMBATISHO NAMBARI 3: Mikopo ya muda mrefu na mapato ya Bima ambayo hayajakusanywa.

Namba	Jina la Wakala	Fedha inayodaiwa kuanzia 1/1/2019 (Shs)	Fedha alizopatiwa kwa mwaka (Shs)	Fedha alizolipa kwa mwaka (Shs)	Fedha inayodaiwa hadi kufika 31/12/2019 (Shs)	Maelezo	Tawi la Bima
1	ATLAS INSURANCE BROKER	25,087,973	0	-	25,087,973	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 5	MWANZA
2	COLOBUS INSURANCE AGENCY	10,016,040	0	-	10,016,040	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 4	DODOMA
3	MJAY INSURANCE AGENCY	0	19,481,650	-	19,481,650	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya mwaka mmoja	DODOMA
4	NIA NJEMA INSURANCE AGENCY	6,031,200	0	-	6,031,200	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 5	DSM
5	NIA NJEMA INSURANCE AGENCY	9,712,000	0	-	9,712,000	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 4	DSM
6	OPTION INSURANCE AGENCY	5,926,190	0	-	5,926,190	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 5	DSM
7	EPIQ INSURANCE AGENCY	5,031,694	0	-	5,031,694	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 5	DSM
8	ASOA INSURANCE BROKER	73,287,482	0	-	73,287,482	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 5	DSM
9	MACREE INSURANCE BROKER	25,550,000	0	-	25,550,000	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	DSM
10	MACREE INSURANCE BROKER	413,000	0	-	413,000	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	DSM
11	GIRBERTIAN	3,037,800	0	-	3,037,800	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	DSM
12	MSAE INVESTMENT	605,340	0	-	605,340	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	DSM

13	SMART B	42,026,632	0	-	42,026,632	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
14	MAKAMBAKO	8,856,787	0	-	8,856,787	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
15	FATA -MBINGA			(236,000)	12,398,059	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
16	GWANKAJA - KYELA	9,024,576		(2,006,000)	7,018,576	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
17	EAGLE INSURANCE	130,929,892		(12,725,690)	118,204,201	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
18	TINA INSURANCE AGENCY	8,140,090		(3,321,030)	4,819,059	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
19	ZOMBA INSURANCE AGENCY	5,994,182		-	5,994,182	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
20	MNGETA GENERAL DEALER	128,374,545		-	128,374,545	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	MBEYA
21	KILIMANJARO	6,938,428	0	-	6,938,428	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 6	ARUSHA
22	YANGSUN	7,290,550	0	-	7,290,550	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	ARUSHA
23	NAISUAKI	1,156,625	0	-	1,156,625	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	ARUSHA
24	KETRIX	1,567,700	0	-	1,567,700	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 3	ARUSHA
25	CHILAMU	2,700,650	0	-	2,700,650	Wakala amesita kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 2	ARUSHA
Jumla					**531,526,363**		

Mikopo ya Mawakala

Namba	Jina la Wakala	Fedha inayodaiwa kuanzia. 01/01/2019 (Shs)	Fedha alizopatiwa kwa mwaka (Shs)	Fedha alizolipa kwa mwaka (Shs)	Fedha inayodaiwa hadi kufika 31/12/2019 (Shs)	Tawi la Bima
1	GIRAFFE INSURANCE AGENCY	2,434,580			2,434,580	DSM
2	MNGETA A&B	5,339,335		0	5,339,335	DSM
3	NIA NJEMA	4,725,000		0	4,725,000	DSM
4	NYAMTEKI INSURANCE AGENCY	258,900		0	258,900	DSM
5	ZOMBA INSURANCE AGENCY	2,510,824		0	2,510,824	DSM
6	FREEDOM INSURANCE AGENCY 76	-	25,000,000	0	25,000,000	DSM
7	NASDEEM INSURANCE AGENCY	-	25,000,000	0	25,000,000	DSM
8	FAM INSURANCE AGENCY	-	25,000,000	0	25,000,000	DSM
9	SMS	3,150,000	0	0	3,150,000	Makao Makuu, Zanzibar
10	BAHASSANY INSURANCE AGENCY	1,800,000	5,000,000	0	6,800,000	Makao Makuu, Zanzibar
11	EAGLE INSURANCE AGENCY	17,146,613	0	0	17,146,613	Mbeya

KIAMBATISHO NAMBARI 4: Matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bodi ya Wadhamini ya ZSSF

Kifungu	Maelezo	Makadirio 2019/2020 (Shs)	Matumizi Halisi 2019/2020 (Shs)	Tofauti (Shs)
	MSHAHARA			
21160	POSHO LA KUKAIMU	8,882,230.50	10,579,839.00	1,697,609
21220	MAPOSHO MENGINEYO	435,700,000.00	476,871,600.67	41,171,601
21170	POSHO LA DHAMANA	-		
	JUMLA NDOGO	**4,289,316,303.32**	**487,451,439.67**	**42,869,209.17**
4300	**MATUMIZI YA OFISI**			
23120	MATENGENEZO	12,000,000.00	15,079,424.00	3,079,424
23240	MATENGENEZO YA UMEME	-	22,859,340.00	22,859,340
22130	USAFI	42,000,000.00	73,650,158.33	31,650,158
23230	MATENGENEZO YA OFISI	60,000,000.00	110,276,910.00	50,276,910
22290	MATUMIZI YA KOMPYUTA	207,240,000.00	451,117,993.97	243,877,994
22160	BIMA YA VYOMBO	15,000,000.00	71,174,904.04	56,174,904
23250	MATENGENEZO YA JENERETA	5,000,000.00	5,944,400.00	944,400
	JUMLA NDOGO	**707,640,000.00**	**1,018,046,956.01**	**408,863,130.34**
	USAFIRI NA USAFIRISHAJI			
22250	MAFUTA	320,770,000.00	368,158,150.00	47,388,150
	CORPORATE EXPENSES	-		
22180	UCHAPAJI NA VIFAA VYA KUANDIKIA	155,162,000.00	251,018,533.91	95,856,534
22280	UTANGAZAJI	467,295,000.00	802,121,261.01	334,826,261
22310	UNUNUZI WA MAGAZETI	3,000,000.00	6,807,160.00	3,807,160
22200	SEMINA NA MIKUTANO	65,000,000.00	118,503,633.50	53,503,634
22210	ADA YA UWANACHAMA (ISSA+ECASSA+TSSA)	79,000,000.00	81,401,976.35	2,401,976
22370	MICHANGO	106,000,000.00	150,160,200.00	44,160,200
JUMLA NDOGO		**1,659,896,059.87**		**534,555,764.77**

4700	**BOARD OF TRUSTEES**			
25110	VIKAO VYA BODI	206,350,000.00	319,275,000.00	112,925,000
25140	MAPOSHO MENGINEYO YA VIKAO VYA BODI	80,300,000.00	158,140,000.00	77,840,000
	SUBTOTAL	**452,010,000.00**	**556,815,000.00**	**190,765,000**
	JUMLA KUU YA GHARAMA ZA UENDESHAJI			**1,177,053,104**
	UEKEZAJI			
24120	GHARAMA ZA UEKEZAJI	1,034,880,000.00	1,406,811,414.11	371,931,414
	MAJENGO	-	452,329,783.16	452,329,783
	JUMLA YA MATUMIZI		1,859,141,197.27	824,261,197.27
JUMLA KUU				**2,001,314,302**

KIAMBATISHO NAMBARI 5:Hali ya utekelezaji wa miradi ya barabara

Jina la Mradi:	Kiasi cha Mkataba	Mkandarasi	Tarehe ya Kuanza Mkataba	Tarehe ilopas-wa Kukamilisha Mradi	Hali ya Mradi hadi Juni 2020
WIZARA YA UJENZI-UNGUJA					
Matengenezo ya Mara kwa Mara ya Baraba-ra ambazo Hazijatengenezwa					
Sharifumsa Mwanyanya -Bububu School road and Kinduni-Kichungwani-Kitope road to bitumen Standard and construction of box culvert -Phase 1	8,146,017,005	M/S Coastal Dredging Company Limited			Haujatekelezwa
Ujenzi wa Mitaro					
Construction of three cells box culverts at Nguli along Upenja iwengwa Roads (Lot 1)	2,636,096,705	M/S China Engineering Construction Corporation	23-June-2006	Miezi 6 baada ya kuanza Mkataba	Haujatekelezwa
Construction of storm water drainage along Nyerere road (Kiembe samaki -Airport section) (Lot 2)					
Usalama Barabarani					
Installation zebra crossings and signs on schools, markets, dispensaries, mosque on village -along Kinazini nungwi	19,399,981 (budgeted amount as per PA)				Haujatekelezwa
TAMISEMI					
Periodic Maintanance of Fuoni Mombasa to Mwera Road (3.40 KM) to bitumen Standards	3,597,816,873	M/S Mwananchi Engineering & Contracting Company Limited (Mecco)	23-Sep-19	Miezi 5 baada ya kusaini mkataba. (March 2020)	Umetekelezwa kwa 60%
Mikataba – PEMBA					

Routine and Maintanance for paved roads (Wete-mtemani)-gando Gando Raha ukungwi (208.45 km)	20,111,636					Haujatekelezwa
Periodic Maintanance of Gombani to Pagali Roads (1.8Km) To Bitumen standard	2,171,874,075		M/S Mwananchi Engineering & Contracting company limited (MECCO)	21-Jun-09	Miezi 3 (30 Sept-2020)	Umetekelezwa kwa 55%

KIAMBATISHO NAMBARI 6: Malipo kwa wafanyabiashara ambao hawakusajiliwa shilingi 74,525,422

Namba	Nambari ya Hati ya malipo	Nambari ya Hundi	Jumla ya fedha (Shs)	Aliyelipwa	Maelezo
1.	16/7 10/7/2019	001563	600,000	Sheby Enterprises	Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo na ufungaji wataa za sola maeneo ya uwanja wa ndege
2.	35/7 19/7/2019	001573	4,000,000	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya fedha za awamu mwanzo kwa ajili ya matengenezo ya nyumba ya wafanyakazi
3.	38/7 25/7/2019	001577	6,000,000	RK General Traders Co. Ltd	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo ya ukarabati wa ukumbi wa mkutano, jiko pamoja na vyoo.
4.	02/8 05/8/2019	001580	10,000,000	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya fedha za awamu ya pili na mwisho kwa ajili ya matengenezo ya nyumba ya wafanyakazi
5.	05/8 07/8/2019	001582	1,500,000	ZMOTION STUDIO	Malipo ya fedha za utayarishaji wa igizo na matangazo ya barabarani.
6.	14/8 09/8/2019	001588	1,445,800	Jumsa Enterprises	Malipo ya fedha za gharama za ununuzi wa vifaa vya umeme na maji
7.	16/8 09/8/2019	001590	1,020,000	Awali Mussa Msafir	Malipo ya fedha kwa ajili ya upambaji na mashamiana
8.	17/8 9/8/2019	001591	390,000	Juma Aman Juma	Malipo ya fedha kwa kikundi cha sanaa ya ngoma ya kibati
9.	18/8 9/8/2019	001592	800,000	Salim Abdalla Seif	Malipo ya fedha kwa kikundi cha sanaa ya maigizo
10.	20/8 09/8/2019	001594	300,000	Ali Juma Kombo	Malipo ya fedha kwa kikundi cha taarab.
11.	38/8 19/8/2019	001602	1,300,000	Seif Humoud Seif	Malipo ya fedha za ununuzi wa matofali.
12.	34/10 16/10/2019	001655	1,384,675	Jumsa Enterprises	Malipo ya fedha za gharama za ununuzi wa vifaa vya umeme na maji

13.	35/10 16/10/2019	001655	789,000	Mbarouk Salim Ali	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji
14.	37/10 16/10/2019	001658	2,134,000	Ibrahim Mkubwa Abdalla	Malipo ya fedha za ununuzi wa vipoza hewa pamoja na mafeni
15.	57/10 25/10/2019	001668	500,000	Jumsa Enterprises	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa nguzo za taa (Papi)
16.	5/12 16/12/2019	001697	3,000,000	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi
17.	22/12 18/12/2019	001709	1,500,000	Mbarouk Salum Ali	Malipo ya fedha za mwanzo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi
18.	12/1 8/1/2020	001730	700,000	Local food Baazar	Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula cha wafanyakazi wa vitengo va mapato
19.	14/1 8/1/2020	001732	281,000	Kassim Ali Suleiman	Malipo ya fedha za marejesho anayolipwa nd. Nema Abdalla Rashid
20.	23/1 17/1/2020	001739	300,000	Ahaabna restraurant	Malipo ya fedha za chakula kilichotumika kwa ajili ya kamati ya PAC
21.	41/1 24/1/2020	001752	2,661,168	Electrothermal Supplier and service	Malipo ya fedha za ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya vipoza joto.
22.	8/2 7/2/2020	TT	4,000,000	Hafka company ltd	Malipo ya fedha ya awamu ya mwisho ya ununuzi wa vifaa vya internet.
23.	24/2 12/2/2020	001769	1,427,185	Adem Store	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kioo cha staff bus (SMZ 127A)
24.	20/3 17/3/2020	001786	2,800,000	M/V/Ndege – Pemba	Malipo ya fedha kwa kazi za usafi wa mazingira.
25.	21/3 16/3/2020	001787	3,000,000	Suleiman Abdulwahid Moh'd	Malipo ya fedha za kodi ya nyumba kwa ajili ya Meneja wa Mamlaka
26.	29/4 22/04/2020	001812	1,425,244	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha za awamu ya mwanzo kwa kazi ya ukarabati wa nyumba ZAA.

27.	30/4 21/4/2020	001813	4,000,000	Issa Hababu Khalfan	Malipo ya fedha za mwanzo kwa kazi ya uwekaji Tarazzo katika jengo la wageni mashuhuri VIP
28.	14/5 08/05/2020	001828	3,000,000	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha za awamu ya pili kwa kazi ya ukarabati wa nyumba ZAA
29.	28/5 20/5/2020	001834	3,180,000	M/V/Ndege – Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usafi wa mazingira.
30.	29/5 20/5/2020	001835	2,315,000	M/V/Ndege – Pemba	Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usafi wa mazingira.
31.	30/5 20/05/2020	001836	4,000,000	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha za awamu ya tatu kwa kazi ya ukarabati wa nyumba.
32.	13/6 15/6/2020	001847	522,350	Rashid M. Soud	Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya magari
33.	22/6 26/06/2020	001854	4,250,000	Suleiman Seif Rashid	Malipo ya fedha za awamu ya nne kwa kazi ya ukarabati wa nyumba
Jumla			**74,525,422**		

KIAMBATISHO NAMBARI 7: Hali ya utekelezaji wa miradi kwenye maeneo huru ya Kiuchumi.

NAMBA	JINA	KINACHO ZALISHWA	UTAIFA	MAHLA ULIPO	HALI YA MRADI	MAELEZO
1	Aaa Fresh	Mchakato wa nyama	Australia	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
2	Almaani Trading Company Limited (Bags Factory)	Ushonaji wa Viatu na begi	Oman	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
3	Al-Mahra Processing	Utengenezaji wa sabuni	Kenya	Amani Industrial Park	Dormant	Unatarajiwa kufutwa
3	Blue Horizon Investment	Uzalishaji wa mafuta ya kula	Kenya	Amani Industrial Park	Dormant	Unatarajiwa kufutwa
4	Comanescu Natural Qualityfood (Smc- Privaty Ltd)	Uzalishaji wa vyakula vikafu (chama)	Romania	Amani Industrial Park	Under Construction	Uko katika majaribio
5	Devi International	Mradi wa mawasiliano	India	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
6	Edcom Limited	Uzalishaji wa vifungashio vya kula	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	Unafanya kazi
6.6	Exotic Edible Oil	Uzalishaji wa mafuta ya kula	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Approved	Unatarajiwa kufutwa
7.4	Hawaii Clearing And Forwarding Co. Ltd(Relaxo)	Utengenezajiwa viatu na mabegi	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	Unatarajiwa kufutwa
8.1	Healing Earth Zanzibar Ltd	Utengenezaji wa Dawa na Vipodozi	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
8.9	Hotelsa Zanzibar Limited	Madawa ya Chemical	SPAIN	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi

9.7	K2-Coconut Tropics Stark	Utengenezaji wa Mafuta ya kula	RUSSIAN	Amani Industrial Park	Operating	-
11	Kadu Salt Refinery Industry Limited	Utengenezaji wa Chumvi	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
11	Metalman Company Limited	Uzalishaji wa bati	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	-
12	Mineral Water Processing & Bottling	Mradi wa uzalishaji maji ya chupa	INDIA	Amani Industrial Park	Operating	Wawasilishe Taarifa ya miezi mitatu
13	Muin Limited	utengenezaji wa mafuta ya kula	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
14	Nsc International Company Ltd	utengenezaji wa mafuta ya kula	CHINA	Amani Industrial Park	Operating	
14	Pama Holding Limited	Other manufacturing n.e.c.	ZIMBABWE	Amani Industrial Park	Approved	Unatarajiwa kufutwa
15	Savannah Rages International (Znz Ltd)	Uuzaji wa nguo za mitumba	ZAMBIA	Amani Industrial Park	Operating	Wawasilishe Taarifa ya miezi mitatu
16	Spot On Warehouse	Uagizaji wa gari na kuuza	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Under Construction	Unatarajiwa kufutwa
17	Sulan Manufactures Ltd	Other manufacturing n.e.c.	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Under Construction	
18	Tree Food Stuff	Uuzaji wa vyakula	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi
18	Yytz Agro-Processing Co. Ltd	Mchakato wa Korosho na kuuza	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	Unafanya kazi
19	Zanbottling Limited	Utengenezaji wa maji ya chupa	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	Wawasilishe Taarifa ya miezi mitatu
20	Zantel Company	Mawasiliano ya simu	UAE	Amani Industrial Park	Operating	Unafanya kazi

21	Zanzibar Fashion Ltd	Ushoni wa nguo	Oman	Amani Industrial Park	Operating	Wawasilishe Taarifa ya miezi mitatu
22	Zanzibar Quality Tailoring	Ushoni wa nguo	Tanzania Zanzibar	Amani Industrial Park	Operating	Wawasilishe Taarifa ya miezi mitatu
22	Zanzibar Safari	Utengenezaji wa mabeseni ya plastic	India	Amani Industrial Park	Dormant	Unatarajiwa kufutwa
23	Zarec Ltd	Ukusha nyaji wa taka na kutengeneza mbolea	Kenya	Amani Industrial Park	Dormant	Unatarajiwa kufutwa
24	Z-Phone Company Limited	Mradi wa mawasiliano ya simu za mkononi	Republic Of Korea	Amani Industrial Park	Approved	Upo hatua za awali bado haujaanza kazi